# Nipashe

Jumatano Novemba 13, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580074

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wanaoambukizwa Ukimwi kwa makusudi kulipwa

UKURASA 3



Ukame, njaa vyakoleza taabu Somalia mashambulizi Al Shabaab yakiendelea

Ukurasa 18

Wanasiasa mna ujasiri wa Nyerere kusema ukweli?

Ukurasa 14

siasa

JUMATANO NOVEMBA 13, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Serikali Romania yakwama bungeni

Ukurasa 20

AMANI MWENEGOHA;

DC mstaafu 'aliyetabiri' mafanikio ya JPM

Na Mashaka Mgeta

NILIPATA bahati ya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Mkoa wa Geita kwa miezi minane, chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, niliiona picha ya mafanikio katika uongozi wake," ndivyo anavyoanza kusimulia Amani Mwenegoha, mkazi wa Wilaya ya Morogoro Vijijini, mkoani Morogoro.

Mwenegoha, alishika wadhifa huo katika kipindi cha kati ya Novemba 2015 hadi Juni 2016. Hivi sasa anajishughulisha na ujasiriamali.

Anasema, akiwa katika utumishi wa umma, alitambua

INAENDELEA UK.16

Amani Mwenegoha, DC mstaafu. PICHA: MTANDAO

Wazo la NCCR-Mageuzi laweza kumaliza mvutano huu

Ukurasa 15

Wanawake waliojitosa wang ae uchaguzi wa Serikali za Mitaa Ukurasa 19

UKURASA 13

# Mkapa afichua mambo mazito

UKURASA 2



- Akiri kuingizwa mkenge EPA
- Asema CCM inadhani iko chama kimoja
- Asimulia safari ya maisha yake miaka 81
- Ataka kuundwa baraza dogo la ushauri
- Ajibu tuhuma kufanya biashara Ikulu
- Mauaji Zanzibar bado yamuumiza kichwa
- Aonya ubinafsishaji viwanda, mashamba
- Ashangaa tuhuma kupendelea wakwe, shemeji



## JPM AANIKA ALIVYONUSURIKA KIFO KWA KUNYWESHWA SUMU

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# CUF yatangaza kujitoa uchaguzi wa S/Mitaa

UKURASA 3


absa

(Huduma za kimataifa(

kukuunganisha na dunia

Kufanya kazi katika nchi 12 barani Afrika na ulimwenguni kunatufanya kuwa benki ya Kiafrika inayoongoza. Tembelea: absa.africa

BARCLAYS

HABARI KITAIFA

# Mkapa afichua mambo mazito

**Na Mary Geofrey**

RAIS mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, ameandika kitabu cha maisha yake, akifichua mambo mazito yaliyoukumba uongozi wake, yakiwamo matumizi mabaya ya fedha za Akaunti ya Madeni ya Nje (EPA).

Kitabu hicho alichokipa jina la 'My Life, My Purpose' kilizinduliwa jana jijini Dar es Salaam na Rais John Magufuli katika hafla maalum iliyohudhuriwa na marais wastaafu na viongozi wengine wengi wa kitaifa na vyama vya siasa.

Kupitia kitabu hicho kilichofanyiwa uchambuzi na Mgola wa Kigoda cha Mwalimu Julius Nyerere kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Rweikiza Mukandala, Mkapa anakiri kuingizwa mkenge katika sakata la EPA.

Anasema awali alisita kutia saini makubaliano hayo, lakini Gavana wa Benki Kuu wakati huyo, Daudi Ballali, alimweleza na kumsihi kuwa kama angekubali, wahusika walikuwa tayari kuchangia mfuko wa kampeni za uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Wahuni walitumia uaminifu wangu kwa chama kunishawishi nikubali. Nilijisikia kuwa nimetumika kusalitiwa na ukweli ni kwamba mimi binafsi sikufaidika na sikupata chochote," anaeleza katika kitabu chake hicho.

Anafafanua kuwa suala la kununua madeni wakati wa uongozi wake, halikuwa la kwanza nchini lakini sakata hilo lilimuumiza kwa kuwa lilianza kusemwa wakati akiwa amemaliza muda wake wa uongozi na jumla ya Sh. bilioni 133 zilichotwa kwenye akaunti hiyo.

Mkapa anasema si sakata la EPA pekee lililowahi kumuumiza katika maisha yake ya uongozi, akibaisha kuwa yapo mambo makubwa zaidi yakiwamo ya watu kumkosoa yeye binafsi badala ya uongozi wake.

Anasema anakubali kukosolewa kisiasa na kisera, lakini kukosolewa yeye binafsi kunamuumiza, akitolea mfano madai ya kumpendelea baba mkwe wa watoto wake katika kubinafsisha mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira.

INAENDELEA UK 8

## ... Asimulia safari ya maisha yake

**Na Mwandishi wetu**

RAIS mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, ameelezea safari ya maisha yake ya miaka 81 tangu akiwa kijiji cha Lupaso, Ndanda hadi kufika jijini Dar es Salaam kuwa kiongozi wa juu wa nchi.

Akiwasilisha uchambuzi wa kitabu chake cha 'Maisha Yangu, Kusudio Langu', kwa niaba ya Mkapa, Makamu Mkuu mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Rwekaza Mukandara, alisema alipata elimu yake katika shule za St. Fransis (sasa Pugu) na Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda.

Baba yake, Mzee Wiliam Matwani, alikuwa mpishi msaidizi katika misheni ya Ndanda, ambaye alifundishwa na wamisionari hadi kuwa katekista na baadaye kufundisha shule za 'Bush'.

"Mama hakuwa na muda wa kujifunza kusoma na kuandika kwani alikuwa msingi wa familia. Akihakikisha analima, kulisha familia na kuelea watoto. Alikuwa mkali lakini msikivu na mpenda haki," alisema.

Ingawa wazazi hawakwenda shule, alisema walipenda watoto wasome na kipato kidogo cha uhakika kila mwezi kilifanya familia ionekane tofauti na kusababisha wivu na chuki.

"Wivu na chuki vilisababisha tukio baya analolikumbuka kwa uchungu. Mwaka 1947 palitokea ukame mkali, watu wakamleta mganga wa kijijini ambaye alidai mama na bibi yake (Mkapa) waliloga kuzuia mvua, hivyo

INAENDELEA UK 8



Rais John Magufuli akizindua kitabu cha Historia ya Maisha ya Rais mstaafu, Benjamin Mkapa (kulia), akishuhudiwa na Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein na Marais wastaafu Ali Hassan Mwinyi, Jakaya Kikwete, katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
06 – 11 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **alhamisi tarehe 14 – 11 – 2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam kuelekea Mafinga,** gari hizo zenye namba za usajili:

| | |
|---|---|
| T 660 BZU / ZD 8121 | T 316 CZS / T 249 AGZ |
| T 628 DFA / ZD 8113 | T 210 BYM / T 146 CHN |
| T 641 DFA / T 137 CHN | T 324 CZS / T 777 AQR |
| T 245 BXH / T 380 DHQ | T 553 BKC / T 385 DHQ |
| T 645 DFA / T 377 DHQ | |

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   - Urefu - mita 33
   - Upana - mita 4.70
   - Kimo - mita 5.4

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port hadi Mafinga Kupitia Iringa,** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215511102


## JPM aanika alivyonusurika kifo

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli ameelezea alivyonusurika kifo kwa kunyweshwa sumu kwa sababu ya kusifiwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Benjamini Mkapa, kuwa ni askari namba moja wa miavuli.

Katika ngwe ya pili ya uongozi wake kuanzia mwaka 2000, Rais (mstaafu) Mkapa, aliwaelezea wateule wake, hasa mawaziri kuwa ni 'askari wa miavuli' na ndipo sifa ya Magufuli kuwa ndiye askari namba moja ilipoanzia.

Rais Magufuli aliitoa siri hiyo jana katika hafla ya kuzindua kitabu cha Mpaka, kiitwacho 'Maisha Yangu, Kusudio Langu' kinachoelezea maisha yake binafsi na uongozi wake hadi kustaafu.

Akizungumza muda mfupi kabla ya kuzindua kitabu hicho, alisema Mkapa alimpongeza kwa kazi nzuri aliyofanya ya ujenzi wa barabara wakati huo Waziri wa Ujenzi. Kabla ya hapo alikuwa Naibu Waziri wa Ujenzi kuanzia mwaka 1995 hadi 2000 chini ya mwanasiasa mkongwe Anna Abdallah.

Alisema baada ya sifa hiyo, alianza kuchukiwa na mawaziri na viongozi wenzake hadi pale aliponyweshwa sumu akiwa mkoani Dodoma na kunusurika kupoteza maisha.

"Namkumbuka Mzee Mkapa pale tulipofanya kazi vizuri alifurahi sana, akatamka kuwa mimi nitakuwa askari mwavuli wake namba moja. Pale alipofanya kazi vizuri ya ujenzi wa barabara nafikiri hili nalo pia ameligusia kupitia ukusa wake wa 117," alisema Rais Magufuli.

"Suala hilo sitakaa nilisahau kwa sababu licha ya dhamira yake njema ya Mzee Mkapa, lilinileteа madhara mimi binafsi. Nilianza kuona dalili za baadhi ya mawaziri, tena wengine wa ngazi za juu kabisa, kuanza kunichukia na muda si mrefu baada ya hapo, nilinyweshwa sumu nikiwa mkoani Dodoma, ambayo almanusura iondoe uhai wangu," aliongeza.

Alisema kwa neema za Mungu alinusurika kifo na baada ya tukio hilo, alimwendea Mzee Mkapa kwa ajili ya kutaka kujiuzulu nafasi yale ya uwaziri lakini alimkatalia na kumtaka amtegemee Mungu na kufanya kazi.

"Katika tukio hili, nilimwona Mzee Mkapa kama mtu anayekupa matumaini hata kama mwenyewe umekata tamaa. Mzee Mkapa nakushukuru sana, nimejifunza kutokuwasifu wateule wangu hata

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Wanaoambukizwa Ukimwi kwa makusudi kulipwa fidia

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

BUNGE limefanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi, ambapo pamoja na mambo mengine imeipa mamlaka Mahakama kutoa amri ya fidia kwa mtu aliyeambukizwa VVU kwa makusudi.

Pia, limepitisha umri wa mtoto kujipima VVU ni 15, huku wabunge wa upinzani wakitaka iwe miaka 12.

Awali akiwasilisha muswada huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Prof. Adelardus Kilangi, alisema inapendekezwa kufanya marekebisho kwa lengo la kujumuisha katika sheria hiyo masharti ya kujipima VVU.

Prof. Kilangi alisema marekebisho hayo yanalenga kuainisha wajibu kwa mtu anayejipima VVU na mtu anayetoa au kusambaza vifaa vya kujipima VVU na kumuwezesha Waziri kutoa miongozo ili kuhakikisha kuna usimamizi wa viwango vya vifaa vya kujipimia VVU vinavyosambazwa au kuuzwa kwa watumiaji.

Alisema muswada huo pia umependekeza kuweka wajibu wa kutunza siri kwa mtu anayemsaidia mtu mwingine kujipima na kufanya kitendo cha kutoa siri kuwa kosa chini ya sheria hiyo.

Alisema marekebisho hayo yamelenga kuweka bayana umri wa mtoto katika masuala ya upimaji wa VVU na kueleza maana ya dhana ya kujipima VVU.

Prof. Kilangi alisema marekebisho hayo pia yanalenga kuwezesha vituo vyote vya huduma ya afya kutoa huduma ya upimaji, bila kujali kuwa vituo hivyo ni vya umma au vya watu binafsi.

"Inapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuruhusu majibu ya vipimo ya mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18 kutolewa pia kwa mzazi, mlezi au mtu mwingine ambaye mwenye vipimo anamuamini. Pia inapendekeza kurekebisha kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza Kanuni za utoaji, usambazaji, matumizi na utupaji wa vifaa vya kujipimia VVU," alisema Prof. Kilangi.

Alisema kifungu cha 23(2) kinarekebishwa ili kuhakikisha kuwa kondomu zinazotengenezwa au kuingizwa nchini zinaidhinishwa na mamlaka zinazohusika na udhibiti wa viwango Tanzania, bila kuwa na haja ya kuzitaja mamlaka hizo kwa majina.

Alisema Kifungu cha 27(3) kinarekebishwa kwa dhumuni la kuongeza adhabu kwa kosa la kutoa taarifa za kupotosha kuhusu tiba au udhibiti wa VVU na Ukimwi.

Prof. Kilangi aliseman marekebisho hayo yanalenga kuzuia watu kutoa matamko kuhusu tiba ya Ukimwi bila ushahidi wa kisayansi.

Mbunge wa viti maalum Chadema, Suzan Lyimo, alisema mkoani Shinyanga asilimia 50 ya watoto wanaopata ujauzito wana umri chini ya miaka 18.

Alisema kigezo cha mtoto kujipima VVU iwe kuanzia miaka 12 na siyo 15 kwani umri huo ni sahihi.

Mbunge wa Malindi (CUF), Ally Saleh, alisema endapo watoto kuanzia umri wa miaka 12 hadi 14 wakiachwa bila ya kupimwa VVU taifa litakuwa linatengeneza bomu watapofikisha miaka 15.

Akitolea ufafanuzi, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema lengo la kuweka umri wa miaka 15 kutokomeza maambukizi ya Ukimwi ifikapo mwaka 2030.

Alisema lengo la serikali ifikapo mwaka 2020 ni fikikia 90, 90, 90, lakini changamoto kubwa ni kuifikia 90 ya kwanza ambayo ni kuhakikisha kila Mtanzania awe amejua hali yake ya maambukizi.


Distributed via ippmedia

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la chama hicho, la kutokushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# CUF nayo yajitoa uchaguzi wa mitaa

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimefuata nyayo za vyama vingine vya upinzani kwa kujitoa kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kikidai mchakato wake si huru na wa haki.

Kimesema kimelazimika kuchukua uamuzi huo baada ya asilimia 90 ya wagombea wake katika uchaguzi huo kuenguliwa na wasimamizi wasaidizi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu msimamo wa CUF, Mwenyekiti wa chama hicho, Prof. Ibrahim Lipumba, aliitaka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kutotumia nembo ya chama hicho kwenye karatasi zitakazotumika katika uchaguzi huo. "Haki haipaswi kutendeka tu, bali inapaswa kuonekana ikitendeka katika mchakato wa uchaguzi mwanzo mpaka mwisho," Prof. Lipumba alisema.

"Kwa kuwa wagombea wetu wameshaondolewa katika ushindani kwa zaidi ya asilimia 90, sisi hatuwezi kushiriki katika uchaguzi huo. Jukumu letu kwa sasa ni kukijenga chama ili kiwe ngangari kinoma, ili tunapotoa uamuzi utekelezeke."

Kiongozi huyo wa CUF, aliwataka wagombea wa chama hicho walioteuliwa kushiriki uchaguzi huo, kuandika barua za kujitoa na kuelekeza nguvu zao kukijenga chama.

Uamuzi huo umetolewa ikiwa ni siku chache baada ya vyama vingine saba vya upinzani kutangaza kujitoa kushiriki katika uchaguzi huo kwa madai sawa na yaliyoelezwa na Prof. Lipumba jana.

Vyama hivyo ni ACT-Wazalendo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), NLD, Chauma, NCCR-Mageuzi na UPDP na Chama Cha Kijamii (CCK).

# LHRC watia neno kijana aliyefungwa minyororo

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, amelaani tukio lililofanywa dhidi ya Shadrack Johanes (26), mkazi wa Old Shinyanga mkoani Shinyanga, kwa kufungwa minyororo chumbani miezi miwili na ndugu zake.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu tukio hilo, Henga alisema kilichofanywa dhidi ya kijana huyo ni ukiukwaji wa haki za binadamu na katiba ya nchi.

Alisema ndugu zake walipaswa kumpeleka katika hospitali zinazotoa matibabu ya afya ya akili ili atibiwe badala ya kumfungia ndani kisa anasababisha uharibifu mitaani.

Alibainisha kuwa ibara za 12 na 13 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, zinapinga vitendo hivyo kwa mtu yeyote kubaguliwa kutokana na sababu ya ulemavu alionao.

Henga alisema ibara hizo zinaweka masharti ya kila mtu kuheshimiwa utu wake na kupewa haki zote anazostahili.

"Sisi (LHRC) tunalaani tukio hili lililofanywa dhidi ya Shadrack kwa kufungwa minyororo chumbani na ndugu zake kwa miezi miwili, huku akiwa uchi wa mnyama," alisema.

"Ukisoma ibara ya 12 ya katiba ya nchi, inasema binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa, na ibara ya 13 inasema kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake, na kijana huyu hakuthamiwa," alisema.

Mama Mzazi wa Shadrack, Nonja Kalala, aliyeamua kumchukua mtoto wake huyo na kumpleka jijini Mwanza kwa matibabu, alisema kwa sasa anaendelea vizuri na wamelazimika kumpatia lishe maalum ili kuimarisha afya yake iliyokuwa imedhoofika kutokana na kufungiwa chumbani kwa muda mrefu.

"Nalishukuru gazeti la Nipashe kwa kumwibua kijana wangu, mimi ninaishi Mwanza, mwanangu alikuwa akiishi Shinyanga na shaghazi yake pamoja na kaka yake, nilikuwa sijui chochote kile juu ya mwanangu kama anafanyiwa ukatili huo," alidai.




HABARI KITAIFA

# Mbunge ataka uzazi wa mpango kwa wanaume

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Khadija Nassir, ameitaka serikali kuanzisha programu za uzazi wa mpango kwa wanaume kwa kuwa utafiti mbalimbali unaonyesha wana uwezo wa kuwapa mimba wanawake tisa kwa siku moja.



Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge huyo alisema utafiti mbalimbali duniani unaonesha kwamba mwanaume mmoja ana uwezo wa kuwapa mimba wanawake tisa kwa siku moja, wakati mwanamke mmoja ana uwezo wa kushika mimba moja kwa miezi tisa.

"Je, serikali haioni sasa kuendelea na program za uzazi wa mpango ni uharibifu wa rasilimali badala yake programu za uzazi wa mpango zifanyike kwa akina baba?"alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk.Faustine Ndugulile, alisema ni dhana potofu kwamba uzazi wa mpango ni wanawake peke yao.

"Suala la uzazi wa mpango linawahusu wanaume vile vile na sisi kama serikali tunahamasisha kinababa na mama kushiriki kwenye uzazi wa mpango salama," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Zubeda Sakuru, alihoji serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wakunga wa jadi ili kupunguza vifo vya mama na mtoto hasa maeneo ya vijijini.

Akijibu, Dk. Ndugulile alisema Tanzania iliridhia mkataba wa Uzazi Salama mwaka 1994, katika mkutano uliofanyika Misri.

"Mkataba huo unaelekeza kwamba kila mama anayejifungua atahudumiwa na mtaalamu mwenye ujuzi, kwa kutilia maanani kwamba matatizo yatokanayo na uzazi hayatabiriki na yakitokea uhitaji kutatuliwa na wataalamu wenye ujuzi katika kuokoa maisha na mama na mtoto mchanga," alisema.

Alieleza kuwa Wizara inatambua wakunga wa jadi kama watu muhimu katika jamii, hivyo Wizara kwa kutambua umaarufu wao katika jamii, inawatumia kufanya uhamasishaji wa wajawazito kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma na ikibidi kuwasindikiza.



Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson (katikati), akiwakabidhi cheti kama ruzuku ya kikundi kati ya vikundi saba, kwa ajili ya kusaidia miradi ya kuwawezesha kiuchumi, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa Relif to Development Society (REDESO), Abeid Kasaizi na Mratibu wa mradi wa shirika hilo, Phulumensi Kavumvuli. **PICHA: MIRAJI MSALA**

Distributed via pressreader

# Kigogo Takukuru aomba kesi kusikilizwa haraka

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi wa kesi inayomkabili Mkurugenzi wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor, umeiomba mahakama kuisikiliza haraka kesi hiyo.

Wakili wa utetezi, Elia Mwingira, ameiomba mahakama itoe amri ya kusikiliza kesi hiyo haraka ili mshtakiwa apate haki yake kwa wakati kwa sababu yupo ndani kwa muda mrefu.

Mwingira, pia alidai mteja wake anayekabiliwa na kesi ya kutakatisha Sh. bilioni 1.477, aliandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), na kwamba mazungumzo hayana mwelekeo mzuri.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri umedai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mbele ya Hakimu Mwandamizi Mfawidhi, Kevin Mhina katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake haujakamilika.

Wakili Wankyo alidai wataelekeza wapelelezi kuhakikisha wanakamilisha upelelezi katika maeneo yaliyobaki.

Baada ya kueleza hayo, Hakimu Mhina aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 26, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Mansoor anakabiliwa na mashtaka manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. bilioni 1.477. Inadaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari 2013 na Mei 2018, mshtakiwa alighushi barua ya ofa ya Agosti 13, 2003 kwa madhumuni ya kuonyesha barua hiyo imetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo huku akijua kuwa sio kweli.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017 maeneo ya Upanga ndani ya Wilaya ya Ilala, mshtakiwa kwa kudanganya alijipatia Sh. milioni 5.2 kutoka kwa Alex Mavika ambaye ni mtumishi wa Takukuru kama malipo ya kiwanja kilichopo Kijiji cha Ukuni Bagamoyo.

Pia inadaiwa kati ya tarehe hizo, Mansoor alijipatia Sh. milioni tatu kutoka kwa Wakati Katondo kama malipo ya kiwanja kilichopo maeneo ya Kijiji cha Ukuni wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

Mshtakiwa huyo pia inadaiwa alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Ofisa wa Takukuru, Gogo Migutah kama malipo ya kiwanja kilichopo eneo hilo hilo.

Katika shtaka ya tano, inadaiwa Mansoor alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa Ekwabi Majungu, ofisa wa Takukuru kama malipo ya kiwanja hicho.

Mansoor anadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017, maeneo ya Upanga jijini Dar es Salaam, akiwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa John Sangwa kama malipo ya kiwanja cha eneo hilo.

Inadaiwa kuwa mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Takukuru, alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Rose Shingela kwa ajili ya malipo hayo.

Katika mashtaka ya utakatishaji fedha, inadaiwa kati ya Januari 2013 na Mei 2018 katika maeneo ya Upanga, mshtakiwa alijipatia Sh. 1,477,243,000 wakati akijua fedha hizo ni haramu na ni zao la kosa tangulizi la kughushi.




HABARI KITAIFA

# Upande utetezi kesi ya kutekwa MO watoa neno

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya kutekwa kwa mfanyabiashara Mohammed Dewji maarufu Mo, umeulalamikia upande wa Jamhuri kuchelewesha upelelezi na kwamba mshtakiwa anateseka mahabusu.

Mshtakiwa, dereva wa teksi Mousa Twaleb, anakabiliwa na kesi ya kumteka mfanyabiashara huyo pamoja na wenzake wanne ambao bado hawajakamatwa na kufikishwa mahakamani hapo.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi.

Wakili wa utetezi, Maufudhu Mbagwa, alidai kuwa Septemba 16, mwaka huu, upande wa Jamhuri uliomba hati za kukamatwa kwa watuhumiwa wengine ambao hawajakamatwa.

Alidai kuwa mwaka mmoja sasa umeshapita tangu mteja wake awe mahabusu na hawajaambiwa hatua ya upelelezi waliyofikia.

Hakimu alihoji sababu ya upande wa Jamhuri kuharakisha kumfikisha mahakamani mshtakiwa wakati washtakiwa wengine bado hawajakamatwa.

Alisema kama inawezekana upande wa Jamhuri unaweza kuendelea na mashtaka dhidi ya mshtakiwa huyo kwa upande wake, ufanye hivyo kuliko kuleta hati ya mashtaka ya watu wengi ambao hawajulikani watakamatwa lini.

Wakili wa Serikali, Glory Mwenda, alidai kuwa anaomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itatajwa Novemba 25, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Watuhumiwa wengine ambao upande wa mashtaka inawatafuta ni raia wanne wa Msumbiji na mmoja wa Afrika Kusini wanaodaiwa kumteka mfanyabiashara huyo.

Washtakiwa hao ambao hawajakamatwa ni Phila Tshabalala raia wa Afrika Kusini, Henrique Simbine, Daniel Manchice, Issac Tomo na Zacarious Junior wote raia wa Msumbiji.

Katika kesi hiyo, inadaiwa kuwa Mei Mosi na Oktoba 10, 2018 katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam na Johannesburg nchini Afrika Kusini, kwa makusudi washtakiwa wote kwa pamoja waliendesha genge la uhalifu.

Pia inadaiwa Oktoba 11, mwaka jana maeneo ya Hoteli ya Colloseum, Kinondoni jijini Dar es Salaam, Twaleb na watu wengine ambao hawapo mahakamani, walimteka MO kwa nia ya kumhifadhi kwa siri na kumweka maeneo ambayo ni hatari.

Pia inadaiwa Julai 10, mwaka jana maeneo ya Mbezi Beach, Kinondoni, Twaleb alitakatisha Sh. 8,000,000 wakati akijua fedha hizo ni kosa la kushiriki genge la uhalifu na makosa ya kupanga.

MO alitekwa nyara Oktoba 11, mwaka jana alfajiri maeneo ya Hoteli ya Colloseum wakati akienda kufanya mazoezi na alipatikana Oktoba 20, mwaka huo huo katika eneo la Gymkhana.

## Ujenzi Bandari Dar wafikia asilimia 60

**Na Mary Geoffrey**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), Bandari ya Dar es Salaam, inaendelea na mradi mkubwa wa uchimbaji wa upanuzi wa gati namba 1-7 na uchimbaji kina katika magati na sehemu ya kugeuzia meli ambao umefika asilimia 60.

Kukamilika kwa mradi huo, kutaifanya Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia meli zenye ukubwa wa hadi mita 305 kutoka uwezo wake halisi wa sasa wa kuhudumia meli zenye ukubwa wa mita 260.

Akizungumza juzi jiji Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema, alisema mradi huo ukikamilika, bandari itakuwa na uwezo wa kuhudumia shehena ya mizigo hadi tani milioni 28 kutoka milioni 15.7 za sasa, kwa mujibu wa takwimu za mwaka wa fedha 2018/19.

Kuhusu gharama za mradi, alisema ni Dola za Marekani milioni 421 ambazo ni fedha za ndani na msaada wa mkopo wa Benki ya Dunia.

"Mradi huu unatarajia kukamilika mwezi wa sita mwakani, na kwa baadhi ya maeneo mengine itakamilika mwanzoni mwa mwaka 2021," alisema Lema.

Alisema mradi huo mkubwa wa upanuzi wa bandari pamoja na miradi mingine iliyopo bandarini hapo itakapokamilika italeta tija katika kukuza uchumi wa nchi na kuongeza mapato ndani ya nchi.

"Mradi huu ni wa kihistoria na una awamu mbili na ya kwanza ni kuongeza ukubwa wa gati na kuongeza kina ili kuhudumia meli kubwa zaidi lakini tutaongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli," alisema Lema.

Alifafanua magati yatakayoongezwa yatakuwa na kina cha mita 14.5 wakati awali yalikuwa na wastani ya mita 8 hadi 8.5.

Lema alisema wamepokea magati matatu likiwamo la kisasa la kushushia meli na gati namba nne inatarajia kuwa na urefu usiopungua mita 327 huku gati namba moja, mbili na tatu zikiwa na urefu wa mita 191.

"Tunatarajia katika mradi huu wa awamu ya kwanza, kuongeza gati lingine kuanzia namba 8-11," alisema Lema. Alisema pia kwa awamu hiyo ya kwanza itawezesha uimarishaji wa miundombinu ya reli ndani ya bandari hiyo kwa lengo la kusafirisha mizigo inayotoka bandarini.

"Baada ya miundombinu ya reli kukamilika, tutahakikisha meli zitakaposhusha mizigo yote inayokwenda nje ya nchi inapakiwa katika meli na kusafirishwa kwa njia ya reli kwenda kuhifadhiwa katika Bandari Kavu ya Kwala," alisema.

## Vigogo Simba kuanza kujitetea Novemba 20

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imesema vigogo wa Klabu ya Simba akiwamo Rais wa zamani, Evans Aveva na wenzake wawili wanaokabiliwa na tuhuma za kughushi na matumizi mabaya ya madaraka, wataanza kujitetea Novemba 20, mwaka huu.

Kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, ambapo Wakili wa Serikali, Sylvia Mitanto, aliomba tarehe nyingine ya kusikilizwa.

Hata hivyo, Hakimu Simba alihoji kwanini kesi ilikuja kwa ajili ya kutajwa wakati ilipangwa kwa kusikilizwa?

Wakili Mitanto alidai tarehe iliyopita waliitaarifu mahakama kuwa wamekata rufani kupinga uamuzi wa mahakama hiyo kuwaona washtakiwa hawana kesi ya kujibu katika Mashtaka ya kutakatisha fedha, na kwamba wanaomba tarehe nyingine kusubiri uamuzi wa rufani.

Hakimu Simba alisema mahakama hiyo itapanga tarehe ya kusikilizwa kwa utetezi na kama kutakuwa na masuala ya rufani waijulishe mahakama. Baada ya kueleza hayo, Hakimu Simba alisema itaanza kusikilizwa utetezi wa washtakiwa Novemba 20, mwaka huu.

Mbali na Aveva, washitakiwa wengine ni aliyekuwa makamu wa rais, Geofrey Nyange maarufu Kaburu na Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili, Zacharia Hansppope wamekutwa na kesi ya kujibu katika mashtaka saba na kuondolewa mashtaka mawili ya utakatishaji fedha.

Katika mashitaka ya kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka. Inadaiwa Aveva na Kaburu wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Marekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays.

Pia inadaiwa wanadaiwa kwa pamoja kughushi nyaraka iliyokuwa ikionesha Simba inalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000 kwa Aveva, kitu ambacho sio kweli.

Aveva anadaiwa katika benki ya CRDB alitoa nyaraka ya uongo ikionyesha Simba wanalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000

Aveva anadaiwa kuwa katika Benki ya Baclays Mikocheni alijipatia Dola za Marekani 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi. Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia Dola za Marekani 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi.

Aveva, Kaburu na Hans Poppe wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya Dola za Marekani 40,577 huku wakijua kwamba siyo kweli Katika mashitaka ya nane, Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonyesha kwamba Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577.



Aliyekuwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Asante Mkapa kwa zawadi hii

**TUNACHOWEZA** kusema ni hongera na shukrani za dhati na za kipekee kwa Rais mstaafu Benjamin Mkapa, kwa juhudi na nia njema ya kutaka Watanzania waendelee kujifunza na kuwa na mawanda mapana ya ufahamu kupitia kwake.

Ametupa zawadi ya kitabu ili tujielimishe masuala ya uongozi kwa kusoma kazi zake, kuzitafakari na kujipima tulipotoka, tulipo na tuendako tunapoitizama Tanzania ya leo na ile aliyoiongoza miaka 24 iliyopita.

Tunakupongeza kwa kuweka kumbukumbu ya kazi zako na uongozi wako kwenye maandiko ili tukujue, tujifunze na kujielimisha kutoka kwenye mkusanyiko wa hadithi ya maisha yako kama raia na pia katika nafasi ya kulitumika taifa kama Rais kuanzia mwaka 1995 hadi 2005.

Kupitia kitabu chako cha My life, My Purpose, 'Maisha yangu, Makusudi yangu,' umetuonyesha ulipotoka, ulipotembea, ulipo na ushauri kwa nchi yako ambayo umeipenda na kuendelea kuipigania hata sasa unapostaafu lakini si kwenye kuwatumikia Watanzania.

Tunaamini kitabu cha Mkapa kitasomwa iwe kwenye shule za msingi na hata kwenye taasisi za elimu ya juu. Ni imani yetu kuwa Rais John Magufuli, wakati akikizindua anawashauri wadau kukitafsiri kwa Kiswahili ili kisomwe na wengi.

Tunaamini kitasomwa na wengi na kufuatiliwa na Watanzania wa aina mbalimbali kwa kuwa kina ujumbe na maudhui yanayowagusa vijana, wanasiasa, wasomi, wanahabari na kwa ujumla kila mmoja popote alipo.

Kitabu hiki kama ambavyo majumuisho yake yametolewa kwa ufupi na Mkuu wa Kigoda cha Mwalimu Nyerere, Profesa Rwekaza Mukandala, kinaelezwa kuwa ni kitabu cha kwanza kuandikwa na kiongozi wa nchi kuhusu maisha yake binafsi.

Hongera, kwa kiongozi wetu ambaye kitabu chake kitaendelea kubaki kuwa tunu ya taifa na zaidi ya sana tutakitumia kujifunza kupitia kwake fikira na falsafa yake ikiendelea kuishi kwenye mawazo yetu. Mkapa katika andiko lake ametukumbusha mengi kubwa ni kulipenda na kuhimiza watu kulisimamia taifa letu. Ametukumbusha kuwa na mshikamano na kukumbuka kuwa daima hatutakuwa na maendeleo kama hatutajitegemea.

Rais mstaafu anasema kama nchi ni lazima tuondokane na utegemezi tujitegemee na kutumia rasilimali zetu kwa maendeleo yetu wenyewe.

Lakini, pia anatukumbusha kuwa nchi yetu inapita katika harakati ambazo tunahitaji sana kuwa na uadilifu na uzalendo. Mkapa anatuonya kuwa kuna baadhi ya watu kwa nia zao wanaweza kukwamisha maendeleo ili kutimiza azma zao.

Anatueleza jinsi ambavyo aliingizwa mkenge kwenye masuala ya fedha za akaunti ya madeni ya nje (EPA) ambayo mtihani wake uliishia kuwa kashfa ya EPA ambayo wengi wanaifahamu, lakini la msingi hapa si kulaumiana ila ni kuonyesha jinsi hamu ya kupata tija binafsi inavyoweza kuliangusha taifa.

Mkapa katika andiko lake anatushauri kuwa na sera na mipango ya kusaidia vijana. Anaeleza kuwa wako vijana wengi mno, lakini kama taifa hatujawa na sera za kuwaendeleza na kuwafanikisha ili wawe na maisha bora.

Rais huyu mstaafu hajawaacha wanasiasa, anawakumbusha kuwa inavyoelekea kila mtu anayejitumbukiza kwenye siasa ana lake jambo. Wapo wanaotaka kupata safari za ughaibuni, lakini pia kuna wafanyabiashara wanaolenga kujinufaisha na kupata mafanikio ya biashara zao.

Yote haya Mkapa anatukumbusha kuyatazama. Anasema ni vyema pia kuwa na Baraza dogo la Bunge kupitia mikataba yetu na ya kimataifa ili kuweka mambo kwa uwazi na kwa manufaa ya taifa letu.

Ni maoni yetu kuwa Mkapa ametufundisha na kutushauri, hivyo basi tuzingatie yote mema anayotushauri kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Salome Kitomari

# Miji inaweza kutunza mazingira kama ilivyokuwa kwa wenzetu

**MOJA** ya mambo ya kujifunza kutoka kwa wengine ni utunzaji wa mazingira katikati ya miji sambamba na maendeleo ya miundombinu.

Distributed via ippmedia

Muungwana alipata fursa ya kutembelea Thailand hivi karibuni, nchi ambayo imepiga hatua kubwa kwenye miundombinu ya kisasa.

Ina mtandao wa barabara za kawaida, kulipia, treni za umeme na maeneo mengine ya watembea kwa miguu.

Licha ya kuwa na barabara kubwa zilizojengwa juu zenye kupitisha magari 16 kwa wakati mmoja yanayokwenda na kurudi, lakini utunzaji wa mazingira umepewa kipaumbele.

Lengo ni kuhakisha kuna hifadhi ya mazingira inanyonya hewa chafu na kutoa hewa safi.

Katika Jiji la Bangkok, kuna makutano ya barabara yasiyohesabika yenye maumbo ya kila aina, yakiwa na barabara zilizojengwa juu ya ardhi, kila moja likiwa na kipaumbele cha utunzaji wa mazingira.

Thailand ni nchi iliyoendelea ikiwa na viwanda vingi na uchumi wake unategemea pia shughuli za kilimo na biashara, bila kusahau usafirishaji. Ni kitovu cha usafiri wa anga, barabara na maji.

Kwa uwekezaji wa miundombinu na majengo mengine mengi, ilikuwa ni vigumu sana kuona misitu au eneo lililohifadhiwa vizuri ili kuleta hali ya ukijani wa kutosha kwenye jiji la Bangkok, lakini imewezekana na kutokana na kuwekwa kwenye vipaumbele vyao.

Muungwana alikaa katika jiji la Bangkok kwa siku nane na siku mbili katika eneo la Prachuap Khiri Khan, mwendo wa saa nne kutoka jijini Bangkok.

Kote huko alishuhudia jitihada za utunzaji mazingira kwa kuhakikisha uwekezaji wa miundombinu unakwenda sambamba na upandaji wa miti na utunzaji wa maeneo ya misitu midogo ndani ya miji hiyo.

Utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa nyakati hizi ambazo kuna changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Ni kwa mantiki hiyo Muungwana anaasa kwamba kasi ya ujenzi wa miundombinu inayoendelea jijini Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi, inapaswa kuhakikisha miti inayokatwa kupisha ujenzi inapandwa upya kwa ajili ya kutunza mwonekano maridhawa na mvuto kwa jiji na miji mingine.

Jiji la Dar es Salaam halina maeneo ya misitu na miti ya kutosha kwa ajili ya kunyonya hewa ukaa inayozalishwa na shughuli za kibinadamu, badala yake linategemea misitu ya Kisarawe ambayo nayo inavamiwa na shughuli za kibinadamu.

> **Kwa uwekezaji wa miundombinu na majengo mengine mengi, ilikuwa ni vigumu sana kuona misitu au eneo lililohifadhiwa vizuri ili kuleta hali ya ukijani wa kutosha kwenye jiji la Bangkok, lakini imewezekana kutokana na kuwekwa kwenye vipaumbele vyao.**

Kama wengine walivyoweza kutunza mazingira kadri maendeleo yanavyozidi kusonga mbele, ndivyo inavyopaswa Watanzania wafanye wakitambua umuhimu wa mazingira kwa afya zao na viumbe vingine kwa ujumla.

Unapotembelea Bangkok utaona maghorofa mengi yenye urefu tofauti lakini hatua chache utaona miti mingi ambayo inasaidia kutunza mazingira na wakati huo huo inaweka madhari nzuri.

Zipo bustani nyingi za kila aina kwenye barabara zote, hakuna barabara iliyojengwa bila kuwekwa bustani, na barabara za kwenda nje ya jiji katikati kuna miti mingi ambayo inasaidia kunyonya hewa ya ukaa inayotolewa na magari.

Ni la kuiga hata kwetu kwa mfano katika eneo la Kariakoo lililomea maghorofa mengi bila ya miti, hata kama kuna eneo linaloweza kupandwa mti husika.

Kuna maeneo kwa mfano katika Jiji la Bangkok yaliyo na ardhi oevu lakini yametunzwa vyema, tofauti na maeneo yetu ambayo yamevamiwa na watu wamejenga kama ilivyo eneo la Jangwani, Kinondoni, Msasani na kwingine.

Inawezekana maeneo hayo kutunzwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho, kwa kuhimiza jamii husika kupanda miti.

Aidha, wenye maghorofa walazimishwe kupanda miti mingi nje ya maeneo yao, huku wasimamizi wa mazingira wakihakikisha hakuna uvamizi wa maeneo yanayohitaji kutunzwa kwa manufaa ya wote.

Uharibifu wa mazingira unaweza kufanywa na wachache lakini madhara yake ni kwa jamii nzima na ndiyo maana ya mabadiliko ya tabianchi tunayoshuhudia, yaani ukosefu wa mvua, mafuriko, vimbunga na mengineyo.

## BARUA / MJADALA

# Mwenendo huu si wa kiungwana kabisa

***Mhariri***
***Habari za majukumu!***

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaotupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani.*

*Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili.*

*Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimueleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake.*

*Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*

*Ni muhimu watu hao wakaelewa kwamba ndani ya usafiri wa umma, kila mtu anakuwa na mipango yake kichwani kama anaenda kazini, na anahitaji utulivu kama anarudi kutoka kazini kwa sababu ya uchovu wa siku nzima na changamoto nyingine alizokutana nazo katika mizunguko yake.*

*Hahitaji kusikia kelele za namna mnavyotongozana au jinsi ulivyomchongea jirani yako kwa mumewe au jinsi ulivyomshushua shoga yako mbele ya watu.*

***Jupilo Jifenenge- Rangitatu***



Vijana wakiangalia pikipiki ikiwa chini baada ya kugongwa na daladala, katika eneo la njia panda Goba, jijini Dar es Salaam juzi. Dereva wa pikipiki alipata majeraha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanasiasa wawe chachu ya kuepuka lugha ya kuudhi

**Sabato Kasika**

MTINDO wa baadhi ya wabunge kurushiana vijembe na maneno ya kuudhi ni miongoni mwa mambo ambayo huwa yanaibuka na kusababisha mivutano ya kikanuni, katika vikao vya Bunge, jijini Dodoma.

Wapo baadhi ya wabunge ambao wamewahi kukaririwa na vyombo vya habari wakitumia lugha ya kuudhi, kwa kusema bungeni kwamba hawaongei na mbwa bali wanazungumza na mwenye mbwa.

Mara mwingine anatamka kuwa kuna chama cha upinzani kina wabunge, ambao wana “mimba zisizotarajiwa bungeni.” na mwingine kutamka kuwa serikali ina tatizo kwa kuwa kuna “akili ndogo inatawala vichwa vikubwa.”

Wapo wengine ambao wamekaririwa na vyombo vya habari wakitamka bungeni kwamba wana vyeti vya matibabu kutoka hospitali ya vichaa ya Mirembe, mara wabunge wanataka kuonekana katika televisheni ili wapate wachumba.

Lugha hiyo ya kuudhi inayokataliwa bungeni, inaambatana na kusema kwamba “mpumbavu ukimchukua ukimchanganya na ngano kwenye kinu atabaki na upumbavu wake.”

Nimetaja sehemu tu ya lugha za kuudhi, ambazo zimewahi kutumiwa na baadhi ya wawakilishi wa wananchi katika chombo hicho cha kutunga sheria ili wajiepushe na lugha hizo zisizo za kistaarabu.

Kimsingi Spika wa Bunge, Job Ndugai amekuwa akionya kuhusu lugha hizo bungeni na kuwasihi wabunge kuacha kuzitumia na badala yake wazingatie Kanuni ya 64 inayozuia lugha za kuudhi bungeni.

Distributed via ippmedia

Lugha za kuudhi, hasa katika vikao vya Bunge, ambazo zimekuwa zikitolewa na baadhi ya wabunge, zimesababisha baadhi yao ‘kutimuliwa’ au kusimamishwa kwa muda kuhudhuria vikao vya Bunge.

Ni vyema sasa wabunge waache mihemko ya itikadi za vyama vya siasa na badala yake wajadili jambo kwa hoja na kama kuna haja kukosoa, basi ukosaji nao uwe wa kiungwana badala ya kuudhiana.

Wapo baadhi ya wabunge, ambao wana michango mingi bungeni, lakini hawatumii lugha ya kuudhi wala matusi, na wameendelea kujijengea heshima mbele ya umma wa Watanzania.

Kwa maana hiyo ni vyema wabunge wawe wa CCM au upinzani, wakaheshimiana kwa kutumia lugha ya staha wanapojadili hoja kwa manufaa ya nchi, siyo ya vyama wanavyowakilisha.

Binafsi huwa ninajiuliza, wabunge kutoa lugha za kuudhi kwa wenzao wakati wa kujadili mambo muhimu ya wananchi, huwa wanafanya hivyo kwa malengo ya kupata umaarufu, au ni kudharau wapigakura wao?

Suala la kutumia lugha ya staha, ambayo ni ya kibunge wakati wa kuchangia mijadala bungeni ni la muhimu, vinginevyo itakuwa ni sawa na kuwadharau wapigakura.

Kuendelea kutumia lugha ya matusi, kejeli na maudhi kwa baadhi ya wabunge ni kuendelea kuliondolea hadhi Bunge.

Pamoja na hilo, wabunge wanatakiwa kujikita katika kuchangia hoja zenye kutatua matatizo ya wananchi ili kutimiza wajibu wa kila mbunge wa kuwakilisha wananchi.

Matumizi ya lugha ya kuudhi huwa hayaishii bungeni tu bali hata kwenye kampeni za uchaguzi kumekuwapo na lugha hizo, ambazo wakati mwingine huwa zinaitwa siasa za majitaka.

Wakati wa kampeni baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakirushiana maneno makali huenda wakiamini kwamba ni njia ya kushusha umaarufu wa wenzao na kumbe wanajiharibia mbele ya umma.

Iwe bungeni au kwenye majukwaa ya kampeni za kisiasa, wanasiasa wanatakiwa kujenga hoja na hata kama ni kukosoa, basi wakosoane kistaarabu bila kutumia lugha za kuudhi.

Mtindo wa kutumia lugha za kuudhi au siasa za majitaka vinaweza kusababisha uhasama miongoni mwa wanasiasa na wafuasi wao na hivyo kugawa na kushindwa kushirikiana na kwa sababu tu za kisiasa.

Matumizi ya lugha za kuudhi yaliwahi kumkera hata aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Jaji Joseph Warioba pale alipokaririwa na vyombo vya habari akisema, baadhi ya wabunge walitoa lugha za kuudhi dhidi ya tume hiyo katika Mkutano wa 13 wa Bunge hilo.

Kwamba katika mjadala wa muswada huo, baadhi ya wabunge walisema hakuna ulazima wa tume hiyo kuwapo bungeni, huku baadhi wakieleza kuwa wajumbe wa tume hiyo siyo wataalamu pekee wa masuala ya Katiba.

Wabunge hao pia walipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2013, baada ya kufanyiwa marekebisho kwa baadhi ya vifungu vilivyokuwa vikilalamikiwa, kikiwamo cha wajumbe wa tume hiyo kutoingia kwenye vikao vya Bunge la Katiba.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Mkapa afichua mambo mazito

INATOKA UK 2

Anasema madai mengine yaliyomuumiza ni ya suala la Next Group Solution wakati wa kubinafsisha Shirika la Umeme (Tanesco), akituhumiwa kumpendelea shemeji yake.

Anasema suala lingine ni kukosolewa kuhusu matumizi ya mali akiwa Ikulu, hasa pale yeye na mke wake, Anna Mkapa, walipochukua mkopo katika Benki ya NBC ili kununua nyumba.

"Ukweli ni kuwa, wakati ule tulikuwa tunaishi Ikulu, tulichukua mkopo kwa masharti nafuu ya biashara. Kabla sijaondoka Ikulu, nilimaliza malipo ya mkopo huo kwa mshahara wangu wa mwisho na mafao yangu, tukapewa hati ya nyumba hiyo," Mkapa anadai kwenye kitabu hicho.

Mkapa pia anazungumzia kashfa ya sakata la rada, akisisitiza kuwa ilikuwa ni lazima kuinunua ili kuimarisha ulinzi, lakini ununuzi ulijawa na udanganyifu. Anasema fedha zilizolipwa na za ziada zilirudishwa kwa serikali.

Kashfa hiyo ni ya ununuzi wa rada ya kuongoza ndege kutoka Kampuni ya Bae System, Uingereza iliyoibuka mwaka 2011. Sh. bilioni 73 zilirejeshwa kama chenji ya rada, lakini waliohusika hawakuchukuliwa hatua yoyote.

AONYA UBINAFSISHAJI

Katika kitabu chake hicho, Mpaka anaonya kuhusu ubinafishaji wa mashamba na viwanda kwa raia wa kigeni akishauri:

"Nafikiri ni muhimu kutizama upya suala la umiliki wa uchumi ili watu wengi zaidi wahusike, kuendelea kusajili kwa umiliki, hasa wa viwanda na mashamba makubwa na kampuni za Asia au kihindi, kunaweza kuleta wivu na shida kubwa huko baadaye."

Mkapa pia anaeleza wasiwasi wake kuwa huenda katika siku za usoni kukatoe shida kutokana na hali mbaya ya maisha ya wananchi kwa kuwa umaskini huenda bega kwa bega na uvunjifu wa amani.

"Hivyo, lazima tujiulize kama tumejikita kwenye utulivu wa amani," Mkapa anashauri katika kitabu chake hicho.

**KUTOTHAMINIWA**

Katika hotuba yake wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu hicho jana, Mkapa alitoa ushauri kwa viongozi wajao waonyeshe nia na bidii kwa majukumu wapewayo.

Alisema wanapaswa kuwa tayari kushirikisha wengine, wasifanye kazi kwa kukurupuka, wafuate na kutii sheria, wawe tayari kusikiliza na wawatafute walezi.

Mkapa alisema amejifunza kwamba, baada ya kustaafu marais wastaafu wanathaminiwa na kimataifa zaidi kuliko nyumbani, jambo ambalo hata Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, pia aliliona.

Sambamba na hilo, alisema kuna haja kuwa na baraza dogo la Bunge, litakalofanya mapitio ya



miswada iliyopitishwa na chombo hicho kabla ya utekelezaji.

Pia alionyesha shaka yake kwa alichokiita 'kukosekana kwa itikadi na fikra pevu kwa mustakabali wa taifa'. Alifafanua maudhui yake kwa kauli:

"Tunahitaji ukombozi wa pili kisiasa, kiuchumi na kiutamadini, tunahitaji kama taifa na mtu mmoja mmoja kuona aibu kuwa ombaomba, tunahitaji kujitegemea na kuthamini, endelevu na maendeleo."

Katika sura ya kimataifa, Mkapa alieleza kusikitishwa na kile alichokitaja kuwa ugoigoi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), chombo kilichoasisiwa katika zama za uongozi wake, huku akifafanua eneo la udhaifu kuwa ni maendeleo kukosekana, huku siasa ikitawala.

**CCM HAIMRIDHISHI**

Kuhusu chama chake ambacho pia kimeshika uongozi wa nchi, Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkapa alikikosoa kwa wajihi wa kujihisi kama bado kipo katika fikra za chama kimoja, akishauri kinahitaji mageuzi ya wakati.

Mkapa aliyewahi kuwa mwenyekiti wa chama hicho kwa muongo mmoja, alishauri kuwapo majadiliano kuliko msuguano anaoushuhudia.

Alieleza anachokishuhudia ni kuwapo kwa watu wanaoingia kwenye siasa kusaka maisha na uchumi kuliko kutumikia watu na taifa, dhana aliyoieleza kuwapo pia katika vyama vingine.

Katika hilo, aliwataja baadhi ya wahusika kuwa ni kada ya wafanyabiashara wanaosaka na kulinda maslahi, wasomi wanaotafuta posho na safari za nje na wabunge wasiojali maslahi ya wanakowakilisha.

Alifafanua: "Wengi wanajali safari za nje, hakuna mabiashano ya wabunge kuhusu sera na utekelezaji wake," Mkapa alitamka.

**MAUAJI ZANZIBAR**

Katika kitabu chake hicho, Mkapa anaeleza kuwa uhusiano wa muungano ulikuwa mgumu na tete, lakini alifanikiwa kutatua baadhi ya vikwazo.

Anataja chanzo Rais wa Zanzibar wakati huo, alipotaka kurekebisha katiba kuruhusu kutawala kwa kipindi cha tatu.

Pia, huko visiwani anaeleza masikitiko yake ya vifo vya watu 22 vilivyotokana na msuguano huo Pemba mwaka 2001, anavifafanua kwamba 'vilimshtua na kumhuzunisha'.

"Hili litaendelea kuwa doa katika urais wangu, ingawa sikuwapo lilipotokea," Mkapa anasema.

**VYOMBO VYA HABARI**

Kuhusu uhusiano na wanahabari, Rais Mkapa kupitia kitabu chake hicho, anakiri kujitokeza sintofahamu iliyompatia tafsiri mbaya, ambayo rasmi anajitokeza kujitetea kuwa hakutafsiriwa kwa usahihi kwani kilichomponza ni hulka yake ya hisia zake kuwa ngumu kufahamika mara moja, akimaanisha hakuwa tofauti nao.

**KWA NINI KITABU?**

Awali katika hotuba yake iliyoendana na kumbukizi ya miaka 81 ya kuzaliwa kwake jana, Mkapa alisema ilikuwa ngumu kuchukua uamuzi wa kuandika kitabu chenye lengo kueleza heshima na unyeti wa nafasi ya uongozi wa nchi, ambao umeshashikwa na marais watano tu tangu miaka 58 ya uhuru wake.

Alisema alitaka kutumia fursa hiyo ya uandishi kuushukuru umma kwa kumpatia nafasi hiyo yenye heshima, ikiwamo anachokiona cha kipekee kufanya kazi kwa karibu na muda mrefu na Mwalimu Nyerere, huku akionyesha uhalisia wa uzoefu wake.

"Mtakapokuwa mnasoma kitabu hiki mtaona namna nilivyotenga kurasa za kumuelezea Mwalimu Nyerere, niliyojifunza kwake, maoni yake, haki za binadamu na bashasha kwa watu aliokuwa akiwaongoza," alifafanua.

Distributed via ippmedia

Alitaja mada mojawapo ni 'kujitegemea', ambayo pia hakusita kumpongeza Rais Magufuli kwa kuitimiza katika mikakati yake ya kuipatia nchi maendeleo.

"True development is self development' (maendeleo ya kweli ni ya kujitegemea). Hii haina maana tusiombe misaada, bali tuombe misaada kwa ajili ya kuendeleza jitihada ambazo tumezifanya," Mkapa alieleza.

Alieleza matarajio yake kwamba kitabu hicho kitaweka msingi wa viongozi wa sasa na wajao kujifunza uamuzi unaohusiana na uongozi wao, matatizo na vikwazo vyake.

Hafla hiyo ya aina yake ilihudhuriwa na marais wastaafu wenzake, Ali Hassan Mwinyi na Jakaya Kikwete. Pia Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

Wengine ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa; Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma; Spika wa Bunge, Job Ndugai; Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi na viongozi wa dini.

Pia mawaziri wakuu wastaafu na aliyekuwa Waziri Kiongozi Zanzibar, Maalim Seif Hamad Sharif na viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa nchini.

# JPM aanika alivyonusurika kifo

INATOKA UK 2

kama wanafanya mazuri mengi. Kwa sababu najua yasijewapata yaliyonipa mimi baada ya wewe kunisifu," alisema.

Alisema hata hivyo wakati mwingine anasau anawasifu na baadaye anaenda kukumbuka yaliyompata.

SAFARI YA UONGOZI

Rais Magufuli, alimtaja Mkapa kuwa kiongozi ambaye aliinua ndoto ya uongozi wake wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka mwaka 1995 akigombea ubunge katika jimbo la Biharamuro Mashariki, kwa sasa Chato.

Alisema Mkapa alimshika mkono juu na kuwambia wananchi kuwa 'nileteeni kijana huyu'.

"Wakati huo nilikuwa na nywele nyeusi, kipara hakikuwapo na huyu mzee aliniiunua na sijui kwa nini alinichagua. Lakini kauli yake ilinifanya nichaguliwe," alisema Rais Magufuli.

Alisema Mkapa hakuishia hapo, akiwa mbunge alimchagua kuwa Niabu Waziri wa Ujenzi na baadaye Waziri wa Ujenzi.

Alisema wakati wa uongozi wake alijifunza kuwa Mkapa akielezwa jambo au akikushauri likiharibika hakuachi atakuwa na wewe na atakutetea.

"Nakumbuka wakati wa ujenzi wa barabara tulivunja nyumba za Kimara, walipeleka mahakamani lakini hakutengua uamuzi wa ujenzi huo licha ya kushauriwa," alisema Rais Magufuli.

Alisema pia Mkapa aliruhusu Waziri wa Fedha, wakati huo Basil Mramba, kutenga Sh. bilioni 1.85 kila mwezi kwa ajili ya ujenzi wa barabara licha ya kuwa hoja hiyo ilipigwa vikali na mawaziri wenzake.

Alisema kuanzia hapo alianza kufungua mlango wa ujenzi wa barabara kwa fedha za ndani na hivyo Watanzania hawana budi kumshukuru Mkapa kwa uamuzi huo wa kujenga barabara kwa fedha za ndani.

Alisema wakati akitaanza mchako wa kuwania urais wa Tanzania, alimfuata Mkapa kwa ajili ya kumwomba kumuunga mkono lakini wakati huo viongozi wengine walikuwa wameshaenda kwake.

## ... Asimulia safari ya maisha yake

INATOKA UK 2

walipigwa na kuteswa sana hadi waliponasuliwa na Padri Mzungu. Bibi wa mama alifariki," alisema.

**SAFARI YA ELIMU**

Mkapa na mwenzie mmoja walichaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari kutoka kwenye darasa la watoto 25 hadi 30, na kwamba kuchaguliwa ilikuwa bahati nasibu.

"Shule ya Sekondari ya Ndanda ilikuwa umbali wa kilomita 60, walitembea kwa miguu bila viatu siku mbili wakiwa wamebeba vitu vyao vilivyofungwa kwa mkeka. Baadaye alipata sanduku la chuma," alisema.

Baada ya kufika shuleni, alisema walimu walikuwa wamisionari walikazia sala na kazi na wanafunzi walipika chakula chao wenyewe.

"Kwa kuwa Mkapa alikuwa mdogo sana, alipewa kazi ya kuosha vyombo. Kawaida alivibeba kichwani mpaka mahali pa kuoshea na kuvirudisha. Anasema kubeba vyombo hivyo ndiyo sababu ana upara hadi leo," alisema Prof. Mukandara.

Alisema mwaka 1952 akiwa na umri wa miaka 15 alikwenda seminari darasa la nane, lakini baada ya muda mfupi aliona upadri si wito wake na alirudi Ndanda kuendelea na shule.

"Mwaka 1957 alichaguliwa kwenda St. Fransis College (Pugu), ikiwa ni shule kuu ya Katoliki Tanzania," alisema.

**Safari ya Siasa**

Akiwa Pugu, Mkapa alipata mwamko wa siasa na aliunga mkono harakati za kudai uhuru na kuandika barua kwa Mhariri wa gazeti la The Tanganyika Standard ambalo sasa ni Daily News na barua ilichapishwa lakini alitumia jina bandia.

"Mkapa alishinda mitihani ya kujiunga na Chuo Kikuu Makerere akiwa kati ya wanafunzi watatu bora katika darasa la wanafunzi 51. Alikumbana na mambo mapya ikiwamo kucheza dansi ya kisasa na aliendelea na harakati za kisiasa," alisema Mukandara.

Anasema alijiunga na Bodi ya Uhariri ya Gazeti la Transition, alikuwa mwanachama hai wa kikundi cha TANU, alishiriki siasa za chuoni, aligombea urais na kwamba ingawa hakushinda ila wanafunzi wa kike walimpa kura nyingi kutokana na kujieleza kwake.

# Serikali yaziahidi taasisi za afya

**Na Mary Geoffrey**

SERIKALI imeahidi kuendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na taasisi za afya nchini, zenye lengo la kusaidia kuongezeka kwa wataalamu na kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Hayo yalielezwa jana jijini Dar es Salaam na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Mohammed Kambi, wakati akifungua kongamano la sita la Kimataifa la Mafunzo ya Madaktari wa Ubongo, Mgongo, Mishipa ya Fahamu na wanaohudumia wagonjwa mahututi.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia madaktari wa mifupa na upasuaji wa ubongo kupata ujuzi mpya kutoka kwa wataalamu wenzao.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha huduma zote za kibingwa katika eneo la ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu zinapatikana nchini kwa kiwango kile kile kama mataifa ambayo tuliyokuwa tukipeleka wagonjwa. Naamini hilo limewezekana kutokana na uwekezaji mkubwa ambao umefanywa na Serikali ya awamu ya tano katika taasisi yetu ya Tiba ya Mifupa (MOI)," alisema Prof. Kambi.

Prof. Kambi alisema kongamano hilo limekua likifanyika kila mwaka nchini, kwa lengo la kuwapa mbinu mpya na za kisasa za upasuaji wa ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu madaktari wa Tanzania na nchi nyingine za Afrika ili waendelee kutoa huduma za kiwango cha kimataifa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema kongamano hilo limekuwa na matokeo chanya kwa sababu kila mwaka washiriki wamekua wakipata mbinu mpya na za kisasa za upasuaji wa ubongo, mgongo, mishipa ya fahamu na huduma kwa wagonjwa mahututi ili kuhimarisha utoaji huduma na kumaliza rufani za kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

"Kupitia kongamano hili madaktari bingwa wetu watapata fursa ya kujifunza mbinu mpya ya kutumia kifaa cha kisasa (Neuro monitoring machine) cha kuangalia mishipa ya fahamu wakati wa upasuaji na baada ya upasuaji na matokeo ya upasuaji kuwa asilimia 100 hii ni hatua kubwa kwetu na nchi nzima," alisema Dk. Boniface.

Kongamano hilo la sita limehudhuriwa na zaidi ya madaktari 100 kutoka mataifa mbalimbali ya Africa, Ulaya na Marekani na kuratibiwa kwa ushirikiano kati ya Taasisi ya MOI pamoja na Chuo Kikuu cha Weill Cornell cha Marekani.

Aidha, litakuwa la siku mbili za mafunzo ya nadharia na siku tatu za mafunzo kwa vitendo na washiriki watafanya upasuaji chini ya uangalizi wa wakufunzi kutoka mataifa ya Ulaya, Marekani na MOI.

# Makambako wakunwa ujenzi wa zahanati

**Na Elizabeth Zaya, MAKAMBAKO**

WANANCHI wa Kijiji cha Lupila Kata ya Kitisi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, mkoani Njombe wamesema kukamilika kwa ujenzi wa zahanati katika kijiji hicho inayojengwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) kutakuwa ni mkombozi kwa wakazi wa kijiji hicho.

Zahanati hiyo ya kijiji cha Lupila inajengwa na Tasaf kwa ufadhili wa umoja wa nchi zinazozalisha na kusambaza mafuta duniani (OPEC).

Wakizungumza kijiiini hapo mbele ya maofisa wa Tasaf waliotembelea kijijini hapo kukagua miradi ya maendeleo, wanakijiji hao walisema ukosefu wa kituo cha afya katika kijiji hicho umekuwa ni mateso makubwa kwao.

Walisema wamekuwa wakitumia muda mrefu kufuata huduma ya afya mbali katika Hospitali ya Makambako na kulazimika kupoteza siku nzima au mbili na kuacha shughuli zao.

"Na kutokana na hospitali hiyo kuwa tegemezi kwa Makambako na maeneo ya karibu, wakati mwingine ukienda hutibiwi siku hiyo, unaambiwa urudi tena kesho yake, na hiyo ni kumwona daktari tu, yaani tunataabika sana," alisema Mwenyekiti mstaafu wa kijiji hicho, Yona Mhiche.

Aliongeza: "Hivi sasa Tasaf wanatujengea zahanati hapa kijijini kwetu, yaani tunaona kama ni muujiza kwetu kwa sababu itakuwa kwa mara ya kwanza kuweka historia, tunashukuru sana na tunaiombea kwa Mungu idumu."

Alisema kukamilika kwa zahanati hiyo na kuanza kutumika kutasaidia wananchi zaidi ya 7,000 kijijini hapo kupata huduma ya matibabu.

Kwa upande wake mmoja wa wanakijiji, Zaina Sanga, alisema kutokana na ukosefu wa kituo cha afya katika kijiji hicho, baadhi ya wanawake wamekuwa wakijifungulia njiani.

"Mwaka jana mdogo wangu alipata uchungu kwa ajili ya kujifungua ilikuwa ni saa tatu usiku, tulipambana tukachangisha na kuanza safari ya kumpeleka hospitali Makambako, lakini kabla ya kufika alizidiwa ikabidi tulazimike kuweka mazingira vizuri tukamsaidia akajifungua, " alisema Zaina.

Aliongeza: "Baada ya kujifungua tulimkimbiza hospitali na bahati nzuri yeye na mtoto wake walichunguzwa na kubainika kwamba walikuwa salama."

Ofisa ufuatiliaji wa miradi ya Tasaf katika Halmashauri ya Makambako, Edwin Mlowe, alisema ujenzi wa zahanati hiyo unatarajiwa kumalizika Desemba mwaka huu.




Wakazi wa Dar es Salaam wakipimwa afya bure na kupewa ushauri jijini humo, mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Wakazi Dar washauriwa, wapima afya bila malipo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Jiji la Dar es Salaam wamepata fursa ya kupimwa afya bure pamoja na kupewa ushauri wa afya.

Wakazi hao walipewa fursa hiyo na Kampuni ya Bima ya AAR Healthcare Tanzania mwishoni mwa wiki, ambapo upimaji afya uliendeshwa na wataalamu wa huduma ya afya wa kampuni hiyo kwa kutoa vipimo vya BMI (Uwiano wa urefu na uzito), sukari na shinikizo la damu.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Ofisa wa Maendeleo ya Biashara wa AAR Healthcare, Jema Baruani, aligundua kuwa watu wengi huwa hawajui na wala hawachukulii umuhimu wa kupima afya zao mara kwa mara, hivyo husababisha shida zaidi za kiafya hapo baadaye.

"Kama wadau wakuu wa afya nchini, ni jukumu letu kutangaza na kuhamasisha watu kufanya uchunguzi wa afya zao mara kwa mara huku tukiwapatia ushauri utakaoweza kuwasaidia na kuweza kudhibiti shida za kiafya ambazo zinaweza kuwa ngumu kutibika hapo baadaye."

"Zoezi hili ni sehemu ya majukumu yetu ya kijamii, kwani tunaamini tunalo jukumu la kutoa suluhisho la huduma bora za afya nchini," aliongezea Baruani.

Mtoa huduma wa afya wa AAR Heathcare, Dk. Kasanga Bashir, alisema: "Kulingana na takwimu za tangu 1980, kumekuwa na ongezeka kubwa na hatari ya magonjwa yasiyoweza kuambukiza kama kisukari hasa kwa wanawake. Lengo letu kuu leo ni kutoa elimu na ushauri kwa wakazi kwa magonjwa yasiyoweza kuambukiza ambayo ni moja ya shida kubwa inayosababisha vifo miongoni mwa wakazi nchini."

Zaidi ya wakazi wa Dar es Salaam 150 walipokea huduma ya afya na ushauri wa kiafya bure.



# Waziri kutembelea ujenzi kituo polisi

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, ameahidi kutembelea na kukagua ujenzi wa kituo cha polisi katika Wilaya ya Ikungi ambao umechukua muda mrefu na kusababisha mkuu wa kituo hicho (OCD) kuishi kwenye maghala ya mkoloni.

Masauni alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, aliyehoji ni lini Wilaya ya Ikungi itajengewa kituo hicho kwa kuwa tangu kuanzishwa kwa wilaya hiyo mwaka 2013, OCD anaishi kwenye maghala ya mkoloni.

"Ujenzi ulishaanza jengo la OCD, ni lini sasa serikali itakamilisha ujenzi wake ambao umesimama tangu miaka mitatu iliyopita," alihoji.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema "Nimhakikishie katika mambo ambayo tutafanya ni kutembelea kituo hiki kwa pamoja tushauriane juu ya utaratibu wa kukamilisha kituo hichi."

Katika swali la msingi, Mbunge wa Kigoma Kusini (CCM), Hasna Mwilima alihoji serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vitendea kazi Jeshi la Polisi katika eneo la Uvinza kama vile magari, ofisi pamoja na makazi.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema serikali imejipanga kujenga nyumba za makazi kwa askari nchi nzima ili kutatua uhaba uliopo.

Alifafanua jeshi hilo lina jumla ya Wilaya 168 za Kipolisi ikiwa ni pamoja na Wilaya za Kiserikali ambapo alidai kati ya hizo wilaya 127 zina majengo kwa ajili ya ofisi na vituo vya polisi vya wilaya ikiwamo Wilaya ya Uvinza.

"Serikali imeendelea kufanya jitihada mbalimbali kuliboresha Jeshi la Polisi kwa awamu. Mathalani serikali imejenga na inaendelea kujenga nyumba za makazi kwa askari nchi nzima katika ngazi ya mkoa na ni mpango wa serikali kujenga ofisi na nyumba za makazi nchi nzima," alisema.

Alisema Wilaya ya Uvinza ina magari mawili ambayo ni T Land Cruiser PT 1415 linalotumiwa na OCD na Leyland Ashock kwa matumizi mbalimbali ya kipolisi.

# Deni la wazabuni lafikia bil. 325/-

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa hadi sasa kiasi kinachodaiwa na wazabuni ni Sh. bilioni 325 na ifikapo mwaka 2020/21 deni hilo litakuwa limelipwa, huku maofisa masuhuli wakitakiwa kufuata vigezo vya ulipaji vilivyowekwa na mlipaji mkuu wa serikali.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kulipa madeni ya wazabuni ambayo yamekuwa ya muda mrefu na kusababisha kufilisiwa.

"Wengi wa wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali Tabora hawajalipwa tangu mwaka 2013, wazabuni wengi wamekopa kwenye benki leo hii wengine wameuziwa nyumba na wana kesi mahakamani, serikali ina mpango gani wa kuwalipa madeni yao?" Alihoji.

Aidha, alisema kwa sasa walipaji madeni wanalipa ya hivi karibuni badala ya kulipa ya zamani yaliyosababisha watu kuuza nyumba zao.

Akijibu swali hilo, Dk. Kijaji alisema serikali kila mwaka imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya kulipa madeni hayo ambapo kwa mwaka 2016/17 ilitengwa bajeti ya Sh. bilioni 625 na zililipwa Sh. bilioni 746.

"Mwaka 2017/18 tulitenga Sh. trilioni moja na zililipwa Sh. trilioni 1.06, 2018/19 zimetengwa Sh.bilioni 600 na zimelipwa. Tumeendelea kulipa madeni haya kinachonishangaza ni kuwepo kwa wazabuni wadogo wadogo ambao hawajalipwa tangu mwaka 2013," alisema.

Aliwaagiza makatibu tawala wa mikoa kuwasiliana na wazabuni wa mikoa ili kuhakikisha hayo madeni hayo bado ni halali na ifikapo mwaka 2020/21 madeni yote yatakuwa yamelipwa.

Kuhusu kulipwa madeni ya hivi karibuni, Naibu Waziri huyo alisema kuna vigezo vya ulipaji wa madeni na kimoja wapo ni madeni ya zamani kupewa kipaumbele kulipwa na kuwataka maofisa masuhuri kufuata vigezo vilivyowekwa na mlipaji mkuu wa serikali.





Katika swali lake la msingi, Mbunge huyo alisema kumekuwa na malimbikizo ya madeni ya wazabuni wanaoidai serikali nchini kwa muda mrefu sana.

Alihoji serikali imefikia hatua zipi katika kuhakikisha inalipa madeni ya wazabuni nchini.

Akijibu, Naibu Waziri huyo, serikali imeendelea kulipa madeni yaliyohakikiwa na kukubaliwa kupitia bajeti inayoidhinishwa na Bunge na kati ya mwaka 2016/2017 na robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020, serikali imetoa zaidi ya Sh. trilioni 2.52 kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi, wazabuni, makandarasi/wahandisi washauri, watoa huduma na madeni mengineyo.

Alifafanua kati ya kiasi hicho, jumla ya Sh. bilioni 379.07 zimetolewa kulipa madeni ya wazabuni na kwamba serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kupunguza madeni, ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kwenye bajeti kila mwaka kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa na kukubaliwa.

Alisema katika ulipaji wa madeni yaliyohakikiwa, serikali imeandaa mkakati wa kulipa madeni yaliyohakikiwa na kuzuia ulimbikizaji wa madeni.

Alieleza madeni yanayohusika kwenye mkakati huo ni yaliyozalishwa na Wizara, Idara zinazojitegemea (MDAs) na Sekretarieti za Mikoa (RSs) yakiwamo madeni ya watumishi, wazabuni na watoa huduma, pamoja na madeni ya makandarasi.

Hata hivyo, alisema ili kukabiliana na changamoto ya madeni, serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa kwa kuzingatia mwelekeo ulioandaliwa wa kulipa madeni hayo kulingana na upatikanaji wa mapato.

Distributed via Inmagna

# Mbunge ahoji utatuzi wa mgogoro wa ardhi

MBUNGE wa Viti Maalum (Chadema), Mary Muro, amehoji serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro uliopo katika viwanja vya Mwanalugali mjini Kibaha ambao umesababisha maeneo hayo kutoendelezwa.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema mgogoro huo unatokana na wenye ardhi hiyo kutolipwa fidia wakati wa upimaji mwaka 2000.




"Kutokana na mgogoro huu viwanja vimeshindwa kugaiwa, je, serikali inatoa msaada gani kwa wananchi hao ambao wameshindwa kuendeleza maeneo yao na kuwasababishia umaskini mkubwa?" Alihoji.

Akijibu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema Halmashauri ya Kibaha inakusudia kuomba kibali kwa Kamishna wa Ardhi ili kufuta baadhi ya viwanja viweze kuuzwa ili kumaliza mgogoro huo.


"Serikali imekamilisha uthamini na kubaini watu 42 wanaidai fidia zaidi ya Sh. milioni 500 na serikali imepanga kulipa fidia hiyo kwa kutumia zitokanazo na mauzo ya viwanja ambavyo vilitolewa kwa wananchi tangu mwaka 2004, lakini mpaka sasa havijalipiwa kodi ya serikali," alisema.

Aidha, alisema serikali inakusudia kubadili matumizi ya eneo moja la ibada ambalo wananchi wanadai fidia ili wananchi wamilikishwe maeneo yao.

"Halmashauri inakusudia kuomba kibali kwa Kamishna wa ardhi ili kufuta baadhi ya viwanja ili viweze kuuzwa na kutunisha mfuko wa fidia na vingine kukabidhiwa ili kumaliza mgogoro uliopokuwapo wa muda mrefu," alisema.




Habari na Augusta Njoji





## RC awafagilia DC, DED kwa utendaji

**Na Allan Isack, KITETO**

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amesema ameridhishwa na utendaji kazi wa Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magessa na mkurugenzi mtendaji wa halmashauri hiyo, kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo wilayani humo.

Mnyeti alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na wananchi wa Mji Mdogo wa Kibaya kwenye ziara yake ya kikazi ya siku tano wilayani humo.

Alisema Magessa ni mchapakazi mzuri akishirikiana na Mkurugenzi wake Kambona hivyo amewaomba wananchi wa Kiteto kutoa ushirikiano kwa viongozi hao ili kufikia malengo ya kuihudumia jamii.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakimlalamikia mkuu huyo wa wilaya kutokana misimamo yake ya kupinga mambo ambayo siyo mazuri kwenye jamii.

"Napenda kuwa kumbusha wananchi kuwa viongozi hawa ni wachapakazi na wamefanya mambo makubwa kwenye wilaya hii nyie mkiona hawafai maeneo mengine wanatamani wawe viongozi wao," alisema Mnyeti.

"Pamoja na changamoto zilizopo Kiteto kama ningekuwa natoa maksi za utendaji kazi basi viongozi hawa ningewapa asilimia 95, kati ya asilimia 100, kutokana na kazi hii waliyofanya kwa kipindi kifupi kwenye wilaya hii," aliongeza Mnyeti.

Alisema ubora wa viongozi hao, umetokana na usimamiaji mzuri wa miradi ya maendeleo hivyo wanapaswa kupongezwa kwa jitihada zao.

Mnyeti alisema viongozi wengine wa wilaya na halmashauri zilizopo katika mkoa wa Manyara wanapaswa kuiga mfano kutoka kwenye wilaya ya Kiteto ili waweze kufikia malengo ya kuwahudumia wananchi.

"Wakuu wa wilaya na wakurugenzi wengine waliopo katika mkoa wa Manyara wanapaswa kuiga mambo mazuri yaliyofanywa na wilaya ya Kiteto," alisema Mnyeti.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Tamim Kambona alisema lengo la halmashauri hiyo, ni kuhakikisha wanasimamia miradi ya maendeleo ipasavyo ili iweze kuwanufaisha wananchi hususani maeneo ya vijijini.

> **"Wakuu wa wilaya na wakurugenzi wengine waliopo katika mkoa wa Manyara wanapaswa kuiga mambo mazuri yaliyofanywa na wilaya ya Kiteto," alisema Mnyeti.**

# Teknolojia kutumia mbwa upekuzi nyara za serikali

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Wanyamapori Afrika (AWF), wameanzisha mpango wa matumizi ya teknolojia ya kuwatumia mbwa kufanya ukaguzi na upekuzi wa nyara za serikali katika mipaka na viwanja vya ndege.

Hayo yalisemwa juzi na Naibu Kamishna Mhifadhi wa (TAWA), Dk. James Wakibara, wakati akizungumza katika ufungaji wa mafunzo kwa kikosi maalumu cha mbwa wanaonusa.

Washiriki nane walitoka mikoa mbalimbali hapa nchini na washiriki wengine sita walitoka katika nchi Cameroon na mafunzo hayo yalifanyika katika Chuo cha Usa River kilichopo wilayani Arumeru.

Alisema wamefikia hatua ya kuanzisha mpango huo wa matumizi ya teknolojia ya vikosi vya mbwa katika maeneo ya mipaka, viwanja vya ndege na bandari ili kurahisisha utendaji kazi wa kudhibiti uingizwaji holela wa nyara za serikali ambao umekuwa ukifanywa na watu wasio waaminifu.

Wakibara aliongeza kuwa mpango huo utasaidia kuendesha operesheni katika maeneo ya wananchi kujua nyara za serikali zilizopo ikiwamo pembe za ndovu zilizofichwa pia kusimamia mipaka ya nchi kuwa salama.

"Tumeamua kushiriki kikamilifu kuwaandaa askari wetu kwa kuimarisha kikosi cha mbwa ili kuhakikisha usimamizi wa mipaka ya nchi inakuwa salama. Tunaamini uwepo wa matumizi ya teknolojia hii itasaidia kudhibiti uhalifu unaohusu rasilimali za wanyamapori hususan wakati wa usafirishaji," alisema Wakibara.

Mkuu wa Kitengo Maalumu kutoka TAWA, John Kaaya, alisema vikosi hivyo walianzisha kwa kutoa mafunzo maalumu kwa washiriki.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mafunzo hayo mwaka 2015, wamefanikiwa kuwa na kikosi cha mbwa kilichopo jijini Dar es Salaam ambacho kinashughulika na kukagua mizigo na bidhaa zinazopitishwa katika viwanja vya ndege, bandari na mipaka.

Aliongeza kuwa tangu kuanzishwa kwa programu hiyo, wamekuwa wakichukua watumishi mbalimbali wa serikali kuwapatia mafunzo ya aina mbili ya mbwa wanusao na wale wanaofuatilia nyayo au harufu za majangili katika maeneo yaliyohifadhiwa.

Alisema Tanzania kuna wanyamapori wengi, hivyo kuna uhalifu wa wanyamapori na ujangili ambao umeshamiri, ndio maana walianzisha mafunzo hayo, ili kudhibiti vitendo vya ujangili wa wanyamapori kwa kutumia teknolojia ya mbwa.

Aidha, alisema matumizi ya teknolojia hiyo, walianza na Mkoa wa Dar es Salamu, na baada ya kufanikiwa kwa kiwango kikubwa walipanua wigo kwa kuhamia mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Alisema kwa upande wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini teknolojia hiyo, wanaitumia kwenye mpaka wa Namanga, mpaka wa Holili na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Mkurugenzi wa Uhifadhi Wanyamapori na Sayansi AWF, Dk. Philip Muruthi, alisema mpango huo ni muhimu kwa kuwa Bara la Afrika limebarikiwa kuwa na maliasili nyingi zikiwamo wanyamapori na misitu.

Alisema changamoto kubwa inayoathiri rasilimali hizo, ni uwindaji haramu unaofanywa na majangili kwa lengo la kujipatia fedha, hivyo alitaka uthibiti wa matukio hayo ufanyike kwa kasi kubwa ili kuokoa maliasili zinazopotea.

Alisema wameamua kushirikiana na serikali ya Tanzania, kuwapa mafunzo askari hao, kwa kipindi cha wiki tisa namna ya kufanya kazi na mbwa hao ili kudhibiti ujangili kwa kuwatumia mbwa hao.

Distributed via ippmedia



Wafanyakazi wa Kiwanda cha Happy Sausage, wakiendelea kupaki soseji kwenye mifuko, kwa ajili ya kwenda sokoni, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# CWT yaitaka h/shauri kuiga mfano Simanjiro

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania, (CWT) Deus Seif, amezitaka halmashauri zote za wilaya nchini kuiiga mfano kwa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, ambayo imelipa maslahi yote ya walimu kwa wakati na kuwaboreshea mazingira ya kazi.

Hayo aliyasema wakati wa maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani ambayo yalifanyika katika Mji mdogo wa Orkesumet.

Alisema halmashauri zote za wilaya nchini zinapaswa kuiga mfano huo kutoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro kwani wamefanikiwa kulipa madai ya walimu kwa wakati.

Alisema amefarijika kusikia halmashauri ya wilaya hiyo, inawajali walimu kwa kuwapandisha madaraja kwa wakati na kulipa madai yao.

"Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, ametueleza kuwa fedha za likizo za mwisho wa mwaka zipo tayari hivyo maofisa elimu waandae orodha ili malipo yafanyike," alisema Seif.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, alisema wapo tayari kulipa fedha za malipo ya likizo ya mwisho wa mwaka kwa walimu wote wanaodai.

Alisema wanasubiri taarifa kamili kutoka kwa maofisa elimu ya msingi na sekondari ili waweze kutekeleza adhima yao.

Mwenyekiti wa CWT wilayani Simanjiro, Abraham Kisimbi, alisema chama hicho, kinaishukuru serikali kwa kuwajali walimu, hivyo, wao kama watumishi wa umma ni kuhakikisha kwamba wanatimiza wajibu wao ipasavyo.

"Madai mengi ya walimu yamefanyiwa kazi, hivyo sisi kama watumishi serikali tunatakiwa kuendelea kufundisha kwa bidii ili ufaulu uzidi kuongezeka," alisema Kisimbi.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Silvanus Tairo, alisema wapo kwenye mchakato wa kukabidhi taarifa hizo ili walimu hao watimiziwe hilo.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Augustine Bayo, alisema tayari wameshaandaa mpango wa kulipa madeni ya walimu wa kilichobaki ni orodha ya majina ya walimu wanaodai kufikishwa katika ofisini ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo.

Ofisa Elimu ya Watu Wazima Halmashauri ya Wilaya ya hiyo, Thomas Lazaro, alisema kwa nyakati hizi, ni muda mwafaka kwa walimu kubuni vyanzo vya mapato na siyo kudai maslahi kwani serikali imetimiza wajibu wake.

# KCMC kujenga kituo cha moyo

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

SERIKALI imezindua mchakato wa maandalizi ya ujenzi wa kituo cha magonjwa ya moyo na mishipa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC.

Kituo hicho kitahudumia wagonjwa zaidi ya 15,000 kutoka mikoa ya Kanda ya Kaskazini na baadhi yao kutoka Kanda ya Kati. Ujenzi wa kituo hicho ulizinduliwa jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege.

"Kwa muda mrefu sasa KCMC imebaki kuwa juu na imekuwa kimbilio la wengi katika kupata matibabu ya uhakika. Tunaoushirikiano madhubuti kwa pande zote serikali ikiwa na jukumu la kulipa mishahara ya watumishi kwenye hospitali hii, KCMC kupitia chuo chake cha utabibu imetoa madaktari, wataalamu wengine wa kada mbalimbali kwenye sekta ya afya ambao wanaendelea kulitumikia taifa letu la Tanzania.

"Nachukua fursa hii kuwahakikishia kwamba serikali itaendelea kuenzi na kutambua mchango wa Hospitali ya KCMC na tutaendelea kushirikiana ili kutoa huduma bora za afya kwa Watanzania. Sote ni mashahidi na leo tunayaona maendeleo makubwa ya hospitali hii ya rufani ya kanda," alisema Kandege.

Kabla ya kuweka jiwe la msingi la maandalizi ya ujenzi wa kituo hicho, Naibu Waziri Kandege, alizindua vipimo vya uchunguzi wa magonjwa vya MRI , CT-scan na digital X-ray katika Hospitali ya Rufani ya KCMC.

Mashine za uchunguzi wa magonjwa ya MRI na CT-Scan, kazi yake ni kuonyesha mahali penye tatizo mwilini na zinatambulisha ukubwa wa tatizo katika eneo fulani mwilini ambalo halionekani kwa macho.

Katika hotuba yake, Kandege alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kuwa zaidi ya watu milioni 12 hufariki dunia kila mwaka kutokana na magonjwa ya moyo na kwamba ongezeko la maradhi hayo linasababishwa na mfumo wa maisha, ulaji wa vyakula pamoja na watu kutofanya mazoezi.

Akitoa maelezo mafupi kuhusu mashine hizo, Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Dk. Gilleard Masenga, alisema zimegharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.5 zitapunguza adha kwa wagonjwa ambao walikuwa wanalazimika kwenda hadi Arusha kutafuta huduma hizo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo, alisema kwa mikoa ya kanda ya kaskazini, tatizo la magonjwa hayo ni kubwa, huku akiwasihi Watanzania kujitokeza kuendelea kusaidia ujenzi huo.


Distributed via ippmedia

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege (wa pili kulia), akishiriki zoezi la uwekaji wa jiwe la msingi la maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa cha Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wajipanga kuunda Saccos kujikomboa

**Na Paul William, MOSHI**

KATIKA kuhakikisha wanachama wa chama cha walaji (MDC) mkoa wa Kilimanjaro wananufaika kiuchumi, wamekubali kwa sauti moja kuanzisha chama cha kuweka na kukopa (Saccos), kwa lengo la kupanua wigo wa kufanya biashara na kujikomboa.

Hayo yalibainishwa na Katibu wa MDC, Joseph Silayo, wakati akisoma maazimio ya wajumbe katika mkutano mkuu wa mwaka 2019 ambako alisema wanachama hao ambao ni wafanyabiashara wamefikia hatua hiyo ili kutimiza malengo ya kukuza biashara zao kama njia mojawapo ya kujiimarisha kiuchumi.

Alisema kuanzishwa kwa ushirika wa kuweka na kukopa kutawawezesha wanachama wa MDC kukuza biashara kutokana na uhakika wa upatikanaji wa mitaji ambayo itapelekea biashara nyingi za wanachama kuimarika na kupanuka.

"Mkutano huo wa wanachama wamekubali ianzishwe saccos ili itoe mitaji kwa wanachama ili wawe wafanyabiashara na hili litaanza mapema mwakani 2020 na kupitia ushirika huu kutakuwa na ongezeko la wanachama," alisema Silayo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya MDC, Joseph Komu, alisema chama hicho sasa kipo katika mchakato wa kupata wanachama wapya ambao ni vijana ili waweze kukiongoza vyema chama hicho kutokana na wanachama wengi kuwa wazee.

Alisema MDC ndicho chama cha walaji kilichopo hai kwani vingine vimekufa na ndiyo maana wanajitahidi kutafuta mbinu mbadala katika kuhakikisha uhai wa chama hicho unaendelea kuwapo kama ilivyokuwa ni kusudio la kuanzishwa kwake.

Kwa mujibu wa Komu, MDC yenye jumla ya wanachama 42 wanaojihusisha na biashara mbalimbali imejizatiti kuwaletea mafanikio yanakuwapo kwa kuongeza rasilimali watu pamoja na fedha kadri ya uhitaji wa wanachama wake watakavyohitaji kwani sheria za ushirika hazina ukomo wa idadi ya wanachama.

"MDC ndicho chama cha walaji kilichobaki na hata rasilimali zake bado zipo na zinajiendesha sehemu nyingine vimekufa ila sisi tunataka kuongeza idadi ya wanachama kwanza ndipo tuweze kukimbizana na mikakati yetu," alisema.

**"Mkutano huo wa wanachama wamekubali ianzishwe saccos ili itoe mitaji kwa wanachama ili wawe wafanyabiashara na hili litaanza mapema mwakani 2020 na kupitia ushirika huu kutakuwa na ongezeko la wanachama," alisema Silayo.**

# 'Tupieni jicho zaidi waliomaliza shule'

**Na Paul William, MOSHI**

IWAPO jamii itafanya ufuatiliaji na mienendo ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba pamoja na kidato cha nne katika kipindi hiki wanapojiandaa kujiunga na masomo zaidi, itawaepusha watoto hawa, kuingia majaribuni na kuharibu ndoto zao.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Shule ya Moshi Airpot, Padri Innocent Massaule, wakati akitoa tathmini ya matokeo ya darasa la saba ya shule hiyo.

Aliitaka kuthamini elimu watoto wanayopatiwa badala ya kuivuruga kwa mambo yasiyo na tija.

Alisema kuwa, watoto hao wakilelewa katika malezi bora na ya kumcha Mungu itasaidia kukamilisha ndoto zao kupitia elimu badala ya kuharibikiwa na kujiingiza kwenye uhalifu.

"Watoto kwa sasa wamekuwa wakitumia muda mwingi katika kujifunza mambo ambayo hayawahusu na kupelekea kuathiri ukuaji wao kitaaluma, hivyo jamii tunajukumu kubwa la kuhakikisha tunasimamia na kulinda maadili ya watoto hao," alisema Padri Massaule.

Alisema kuwa katika matokeo hayo ambapo shule imeshika nafasi ya tatu kiwilaya na nafasi ya 19 kimkoa ni wajibu wa jamii kuendeleza taaluma waliyopata wanafunzi ili wakawe mabalozi wazuri na kutimiza ndoto zao.

"Matokeo haya ndicho kipimo cha maadili mema tunayoyajenga kwa sasa tunaamini tutakwenda kufanya vizuri zaidi ya hapa katika matokeo yatakayofuata," alisema Padri Massaule.

Mmoja wa wazazi Judica Mushi, mbali na kupongeza shule hiyo kufanya vizuri aliwataka wazazi kuwa na kasumba ya kufuatilia mienendo ya wanafunzi badala ya jukumu hilo kulikabidhi kwa walimu peke yao.

"Walimu wanafanya kazi yao na sisi wazazi ni lazima tuhakikishe tunajua vyema mienendo ya watoto wetu sababu dunia imebadilika si kama zamani itapelekea kupunguza kunyoosheana vidole," alisema.



Ukurasa 14

**Wanasiasa mna ujasiri wa Nyerere kusema ukweli?**

Ukame, njaa vyakoleza taabu Somalia mashambulizi Al Shabaab yakiendelea



Ukurasa 18

siasa

JUMATANO NOVEMBA 13, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 20

**Serikali Romania yakwama bungeni**



Ukurasa 15

**Wazo la NCCR-Mageuzi laweza kumaliza mvutano huu**

AMANI MWENEGOHA;

# DC mstaafu 'aliyetabiri' mafanikio ya JPM

**Na Mashaka Mgeta**

"NILIPATA bahati ya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Mkoa wa Geita kwa miezi minane, chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, niliiona picha ya mafanikio katika uongozi wake," ndivyo anavyoanza kusimulia Amani Mwenegoha, mkazi wa Wilaya ya Morogoro Vijijini, mkoani Morogoro.

Mwenegoha, alishika wadhifa huo katika kipindi cha kati ya Novemba 2015 hadi Juni 2016. Hivi sasa anajishughulisha na ujasiriamali.

Anasema, akiwa katika utumishi wa umma, alitambua

INAENDELEA UK.16



Amani Mwenegoha, DC mstaafu. **PICHA: MTANDAO**

**Wanawake waliojitosa wang ae uchaguzi wa Serikali za Mitaa** Ukurasa 19

KARDINALI PENGO:

# Wanasiasa mna ujasiri wa Nyerere kusema ukweli?

• Mwalimu alikiri kwenda Bagamoyo!

**Na Raphael Kibiriti**

JUMATANO Oktoba 30, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo aliongoza Adhimisho la Misa Takatifu iliyokuwa imeandaliwa na Umoja wa Wanamawasiliano Wakatoliki wa jimbo hilo (UMAKADA).

Umoja huo uliandaa adhimisho hilo kama shukrani kwa ajili ya maisha ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, ikiwa ni sehemu ya Kumbukumbu ya miaka 20 toka alipofariki Oktoba 14, 1999, kwenye Hospitali ya Mtakatifu Thomas, nchini Uingereza.

Mwalimu alikuwa vilevile muumini wa kanisa hilo, sasa akiwa na hadhi ya Mtumishi wa Mungu, katika taratibu za kanisa hilo.

Mwandishi alikuwa mmoja wa waliohudhuria adhimisho hilo na katika mahubiri ya Kardinali Pengo, aliguswa zaidi na kipengele kilichoangazia ujasiri wa Mwalimu wa kusema ukweli juu ya nafsi yake kwa gharama yoyote.

Pamoja na mengine, kipengele hicho kilimgusa mwandishi kwa sababu taifa sasa linaelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba 4 mwaka huu, ambapo wananchi watachagua viongozi wao katika ngazi ya serikali za mitaa.

Viongozi watakaochaguliwa ni pamoja na wenyeviti wa vitongoji, vijiji, mitaa na wajumbe wa serikali za mitaa.

Aidha, mwakani (2020), taifa litaingia kwenye uchaguzi mkuu wa kumchagua Rais, Wabunge na Madiwani, pia Rais wa Zanzibar, Wawakilishi na Madiwani, kwa upande wa Zanzibar.

Chaguzi hizo ambazo pamoja na wengine, zinawahusisha vilevile wanasiasa kama alivyokuwa Mwalimu Nyerere.

Kimsingi wanasiasa hawa, lakini raia wengine kutoka kada tofauti za maisha, wana la kujifunza kutokana na mahubiri hayo ya Kardinali Pengo, hususani juu ya kipengele hicho cha ujasiri wa kusema ukweli aliokuwa nao Baba wa Taifa.

Ujasiri ambao haukujali hofu juu ya nafsi yake au nafasi yake ya uongozi wa kisiasa, kijamii, kiuchumi hata wa imani yake.

“Mfano wa mwisho wa uinjilishaji wa Mwalimu ambao ningependa kuutoa jioni ya leo ni huu... juzijuzi nilikuwa namsikiliza Mwalimu katika yale anayoongelea, akaongea kwa uwazi kabisa jinsi alivyokuwa Bagamoyo na wazee,” anasema na kuongeza akimunukuu Mwalimu:

“Majority (wengi) ya wale pengine wote waliokuwapo walikuwa ni Waislamu, isipokuwa mimi tu ndiyo Mkristo au labda kama alikuja John Rupia, alikuwa ndiyo Mkristo mwenzangu tuliyekwenda pamoja naye.”

Kardinali Pengo akaendelea kunukuu alichosema Baba wa Taifa akieleza jinsi walivyochinja mbuzi, kumwaga damu ili kummaliza (Edward) Twining na wazee kumwambia aruke.

“Haya, Mwalimu anayaeleza vizuri kabisa, sasa sijui wengine kama mnaweza kuona jambo la uinjilishaji katika hilo, sijui... mimi kwangu sitaki kutoa hukumu juu ya yale aliyofanya Mwalimu na ametueleza mwenyewe kwa uwazi,” anasema na kuongeza:

“Sitaki kutoa hukumu, lakini swali langu ni hili, je yeye (Mwalimu Nyerere) ni mwanasiasa peke yake aliyekuwa anakwenda Bagamoyo? na mpaka leo hatuna wanasiasa Wakatoliki wanaokwenda huko!”




Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Toka mwanzo Mwalimu alitoa kipaumbele katika masuala mazima ya usawa, haki, kutooneana katika jamii na alifanya hivyo akiongozwa na dhana ya upendo, nia yake ikiwa wote twende pamoja.



Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo

Kardinali Pengo aliendelea kusaili katika mahubiri yake hayo juu ya hili la wanasiasa na wengine hasa katika kipindi hiki taifa linapoelekea kwenye chaguzi za kupata viongozi wake.

“Na kwa nini nauliza hilo, nauliza wengekuwapo, au wapo hawa waenda huko Bagamoyo au mahali pengine, wengine wanasema Sumbawanga, sijui wapi kwenda kujipatia uwezo wa kupata kura nyingi na kupita, wapo wangapi wanaokwenda huko wangekuwa tayari kutamka kama Mwalimu alivyotamka juu ya nafsi zao? hilo ndilo swali langu kubwa.”

Askofu huyo Mstaafu anaendelea kuhoji iwapo hawapo wanasiasa wanaoenda Bagamoyo ama mahali pengine na kama wapo anasaili kama miongoni mwao wangekuwa tayari kuwa na ujasiri wa kueleza hayo.

“Kuhukumu juu ya madhambi ya mtu ni Mungu anajua, lakini kuwa na ujasiri wa kutamka ukweli mimi niliendo Bagamoyo, wakachinja beberu, nikaruka kaburi lake...nilikuwa peke yangu mkristo, sijui wangapi leo wanaweza kuwa na ujasiri wa kusema ukweli huo juu ya nafsi zao,” anasema na kuongeza:

“Na ninapouliza hilo siyo kwamba labda ni wanasiasa tu, huenda siyo wanasiasa tu, je inawezekana labda wakawepo mapadri wanaokwenda huko... tuseme mimi kama nitakwenda huko, nitakuwa na ujasiri wa kuja kuwaeleza kama mwalimu alivyokuwa na ujasiri wa kueleza hilo.”

Aliwasisitiza wanasiasa na wengine kuwa tayari kusema ukweli hata kama ni kwa gharama ya nafsi zao kisiasa, kijamii, Kiuchumi na kiimani kama Mwalimu Nyerere alivyofanya enzi ya uongozi wake.

**PAULO RUPIA**

Kabla ya adhimisho hilo la Misa, ambalo lilihudhuriwa pia na watu wa kada mbalimbali wakiwamo viongozi wastaafu wa serikali, ambao baadhi yao walifanya kazi kwa karibu na Baba wa Taifa, kuliendeshwa Mada kumhusu kiongozi huyo wa Tanzania.

Mada hizo zilizoongozwa na Padre Vitalis Kasembo, Mkurugenzi wa Utume wa Walei wa jimbo Kuu, ziliangazia nafasi ya Mwalimu Nyerere kama Mwinjilishaji katika jamii, vilevile nafasi yake kama mwanamawasiliano katika Jamii.

Akichangia mada hiyo, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu enzi za utawala wa Rais Ali Hassan Mwinyi, Balozi Paul Rupia, alisema Mwalimu Nyerere alikuwa ni kiongozi mwenye maono ya mbali kwa ajili ya ustawi wa Tanzania.

“Toka mwanzo Mwalimu alitoa kipaumbele katika masuala mazima ya usawa, haki, kutooneana katika jamii na alifanya hivyo akiongozwa na dhana ya upendo, nia yake ikiwa wote twende pamoja,” anasema na kuongeza:

“Hivyo leo hii kama taifa tunapovuna amani tuliyonayo nchini, ni mbegu ya upendo aliyoipanda wakati ule, hivyo tunapaswa kama nchi tumuenzi, tumuishi kwa kuitafsiri vizuri amani tuliyonayo.”

**PADRE JOSEPH MASENGE**

Akizungumza katika adhimisho hilo, mbali na kushukuru kwa mahubiri yake, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Mlezi wa UMAKADA, Padre Joseph Masenge, alimuomba Mwadhama aendelee kuwamegea Watanzania yenye ustawi aliyoyonayo kila fursa inapojitokeza kama alivyofanya siku hiyo.

# Wazo la NCCR-Mageuzi laweza kumaliza mvutano huu

• Ni wa mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa

Na Sabato Kasika

CHAMA cha upinzani cha NCCR-Mageuzi, kimejiondoa kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa kufuatia majina ya wagombea wake kukatwa.

Pamoja na kujiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho, mwenyekiti wa chama taifa, James Mbatia, anaviomba vyama vya upinzani nchini kutafuta njia ya maridhiano na serikali ili kuendelea kuilinda amani ya nchi.

Ndivyo kiongozi huyo alivyokaririwa na vyombo vya habari jijini Dodoma akisema hayo wakati akitangaza chama chake kujiondoa, kwamba katika majina 35,567 waliyopitishwa na chama hicho, yaliyorejeshwa ni 149.

"Jambo hilo halikubaliki, hivyo tumeamua kujitoa katika kinyang'anyiro hicho. Baada ya kufanya kikao cha Kamati Kuu tumeagiza wagombea wetu wajitoe na wadhamini, waliowadhamini ambayo ni matawi, tumeagiza waondoe udhamini au wagombea wajiondoe wenyewe, anasema Mbatia.

Mwenyekiti huyo anaongeza kusema: "Sisi hatushiriki uchaguzi huu wanatakiwa kufuata kanuni, hatuwezi tukaliache Taifa linapelekwa ovyo, hii ni hatari sana," anasema.

Ingawa kiongozi huyo anasema mengi, lakini kubwa ambalo naamini ni muhimu lizingatiwe na wanasiasa wote ni kutafuta njia ya maridhiano na serikali ili kuendelea kulinda amani ya nchi.

Hii inatokana na ukweli kwamba jamii tulivu na yenye amani ni muhimu katika kufanikisha shughuli za maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla, hivyo amani haina budi kulindwa na watu wote.

Mvutano ambao umejitokeza baada ya serikali kuamuru wagombea wa upinzani waliokatwa majina warudishwe kwenye kinyang'anyiro ni wazi kwamba kuna haja ya kutafuta njia ya maridhiano.

Kinachoendelea sasa hakiwezi kulifikisha taifa pazuri, bali ni kukaa meza moja ya mazungumzo ili kila upande utoe dukuduku na hatimaye kufikia muafaka na kisha kuendelea na mchakato wa uchaguzi.



Mwenyekiti wa NCCR-MAGEUZI, James Mbatia. **PICHA: MTANDAO**

### MAAGIZO YA TAMISEMI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, anawaagiza wasimamizi wa uchaguzi kuhakikisha wagombea wote walioteuliwa na kudhaminiwa na kufanikiwa kurejesha fomu za uteuzi kwa wasimamizi wasaidizi wanaoshiriki katika uchaguzi huo.

"Hapa hakuna mtu kukimbia kwenye 'cage' (ulingo), hakuna mtu kuweka mpira kwapani, wote waliochukua fomu na kurejesha fomu wataenda kushiriki uchaguzi Novemba 24, mwaka huu, kama wamezoea kukimbia safari hii hakuna kukimbia," anasema Jafo.

Anasema, kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi za serikali za mitaa, Tangazo la Serikali namba 371 na kanuni ya 49, wagombea wote walioteuliwa na kudhaminiwa na vyama vyao na kufanikiwa kurejesha fomu zao za uteuzi kwa msimamizi msaidizi wa uchaguzi katika kipindi kilichokuwa kimepangwa cha kuchukua na kurejesha fomu, wanapewa sifa ya kupigiwa kura na wananchi katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

> "Kimsingi kila chama kina haki ya kuelezea msimamo wake, lakini jambo la muhimu hapa ni kuweka mbele maslahi ya taifa, siyo ya vyama vya siasa kwa ajili ya kulinda amani.

Lakini pia anawataja wagombea, ambao hawatashiriki katika uchaguzi huo ni wale waliobainika kuwa na makosa yakiwamo ya kutokuwa raia wa Tanzania, kujidhamini wenyewe, kujiandikisha mara mbili, wasiodhaminiwa na vyama vyao vya siasa na kurejesha fomu watu zaidi ya mmoja kutoka chama kimoja.

"Vyama vya siasa ndiyo vilivyojitoa katika uchaguzi huo na siyo wagombea," anasema bila kutoa ufafanuzi kutokana na sheria ya sasa nchini kutoruhusu wagombea binafsi na inaelekeza wagombea wote wa nafasi za uongozi wa kisiasa kupitia vyama vya siasa.

### MSIMAMO WA BAADHI YA VYAMA

Maagizo ya Jafo yanapingwa na vyama vya upinzani huku vingine vikiweka masharti ndipo vishiriki katika uchaguzi huo, vinginevyo vitaendelea kukaa pembeni vikishuhudia kinachoendelea.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kinasema, wasimamizi wa uchaguzi huo wameshapoteza uhalali wa kusimamia uchaguzi huo kwa kuwaengua wagombea bila sababu za msingi.

Kinataka uchaguzi usimamiwe na watu huru ili mchakato uwe huru, kwamba takwimu za CCM kupita bila kupingwa siyo halali na kudai kuwa kama waziri Jafo angekuwa na nia njema asingetangaza kuwa CCM imepita bila kupingwa wakati anajua kuna waliozuiliwa bila sababu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo

Ndivyo alivyokaririwa na vyombo vya habari akisema, Naibu Katibu Mkuu wa Chadema John Mnyika na kupiga marufuku nembo ya chama hicho kutumika katika uchaguzi huo.

Wakati Chadema ikisema hayo, Chama cha ACT-Wazalendo nacho kimesema hakiwezi kuhalalisha uharamu kwa kuwa mchakato wote, katika hatua zote za kuchukua na kurejesha fomu ziliathiriwa na ofisi za wasimamizi kufungwa wiki nzima.

Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, anakaririwa na vyombo vya habari akisema:

"Hatuwezi kuingia kwenye mtego aliotuwekea, mchakato uanze upya, iundwe kamati huru yenye uwakilishi wa vyama vyote, mchakato wa kuchukua kurejesha uanze upya ili uchaguzi ufanyike katika mazingira ya kuaminiana, amani na uhakika," anasema Zitto.

Zitto anasema, uhalisia ni kuwa wagombea watashiriki uchaguzi, lakini wasimamizi watawatangaza watu waliowaacha kwenye mchakato wa awali, hivyo hataki chama chake kishiriki uchaguzi huo.

"Kama waliweza kufuta watu bila sababu za msingi, basi hawashindwi kuwatangaza waliowaacha awali kama washindi. Walisema wagombea wa upinzani wameshindwa kujaza fomu, sasa fomu walizonazo zimerekebishwa saa ngapi?" Anahoji.

Kimsingi kila chama kina haki ya kuelezea msimamo wake, lakini jambo la muhimu hapa ni kuweka mbele maslahi ya taifa, siyo ya vyama vya siasa kwa ajili ya kulinda amani.

Suala la kukaa pamoja ili kumaliza mvutano huo limesemwa na Mbatia wakati akitangaza chama chake kujitoa, akiviomba vyama vya upinzani nchini kutafuta njia ya maridhiano na serikali, ili kuendelea kuilinda amani ya nchi.

Vilevile ni muhimu kutambua kuwa nyumba inayojengwa ni moja, ambayo ni Tanzania, hivyo hakuna haja ya kugombea fito, badala yake ni kukaa meza moja kwa ajili ya maridhiano, kwani penye wengi hapaharibiki neno.

# DC mstaafu 'aliyetabiri' mafanikio ya JPM

INATOKA UK.13

namna Rais Magufuli alivyoweka wazi dhamira ya kujenga Tanzania yenye uchumi unaotokana na viwanda, kupiga vita rushwa, kuboresha sekta mtambuka zikiwamo elimu, afya na kuongeza ufanisi, nidhamu na uwajibikaji serikalini.

"Alionyesha wazi dhamira yake ya ongezeko la kodi, kudhibiti matumizi ya serikali, kupambana na ubadhirifu wa mali za umma na kuhakikisha rasilimali za Watanzania zinawanufaisha raia hasa maskini, katika kuinua hali zao kimaisha," anasema.

**ILANI YA CCM**

Mwenegoha anasema hatua nzuri za utekelezaji wa ilani ya CCM ni miongoni mwa viashiria vya uaminifu wa Rais Magufuli kwa chama anachokiongoza, huku akitoa mfano wa baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na kuwagusa wananchi wengi wakiwamo wakazi wa Morogoro Vijijini.

**RELI YA KISASA (SGR)**

Anasema miongoni mwa miradi inayogusa maisha ya wakazi wa Morogoro Vijijini ni ujenzi wa reli ya kisasa maarufu kama SGR ambayo, licha ya kuwa ilani haikutaja kwamba itaendeshwa kwa umeme, lakini ubunifu wa Rais Magufuli umesababisha matumizi ya nishati hiyo na kuhalalisha 'ukisasa' wa reli hiyo.

**ATCL**

Kwa mujibu wa Mwenegoha, sekta ya anga ni miongoni mwa maeneo muhimu yanayochochea utalii na kuongeza kipato, hivyo hatua iliyofikiwa katika ununuzi wa ndege zinazofikia nane, inapaswa kuwa sababu ya kudhihirisha ubora wa Rais Magufuli katika uongozi wake.

Anasema ufufuaji na uimarishaji wa ATCL ni moja ya vipaumbele vilivyoainishwa kwenye ilani ya CCM na kwamba ilipoanza kununuliwa ndege aina ya bombardier, iliaminika kwamba ingetosha 'kwa kuanzia' katika awamu ya kwanza ya utawala wake.

"Kumbe (Magufuli) aliona mbali zaidi na kununua ndege za masafa ya kimataifa. Nimekuwa mmoja wa watu wanaosafiri kwa kutumia ndege zetu ikiwamo aina ya dreamliner... ni jambo lenye kutupatia ufahari, raha," anasema.

**BWAWA LA UMEME LA JULIUS NYERERE**

Ukiacha mbali umuhimu wa bwawa lenyewe, Mwenegoha anasema kitendo cha kuliita bwawa la Julius Nyerere inatoa heshima kubwa kwa mwasisi wa nchi yetu, Mwalimu Julius Nyerere ambaye pia alisimamia msingi wa kutumia rasilimali za nchi kwa maslahi ya walio wengi.

Anasema ujenzi wa bwawa hilo unahusiana na maagizo ya ilani ya CCM katika kuimarisha vyanzo vya umeme yakiwamo maji.

Anabashiri kwamba kukamilika kwa mradi huo kunaweza kuifanya Tanzania kuwa na mitambo ya kuyeyusha dhahabu maarufu kama Goldsmelter inayohitaji zaidi ya megawati 400 za umeme.

"Hali ikiwa hivyo, makanikia yaliyomsumbua sana hayatapelekwa tena nje ya nchi na hivyo kudhibiti utoroshaji kijanja wa dhahabu yetu," anasema.



Mradi wa Daraja la Juu la Tazara (Flyover) uliojengwa chini ya Rais Magufuli. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Kumbe (Magufuli) aliona mbali zaidi na kununua ndege za masafa ya kimataifa. Nimekuwa mmoja wa watu wanaosafiri kwa kutumia ndege zetu ikiwamo aina ya dreamliner...

Anaongeza, "kwetu sisi wa Morogoro Vijijini, bwawa hili limetutatulia kero za muda mrefu za barabara mbovu tangu tulipopata uhuru, zikiwamo za Ubenazomozi-Ngerengere-Tununguo-Kiganila-Mvuha-Dutumi mpaka Kisaki ambayo sasa imejengwa kwa kiwango cha kupitika wakati wote.

Anasema wakazi wa eneo hilo wanatambua pia mipango iliyopo ya kuweka barabara hiyo na ile ya Morogoro-Matombo-Mvuha kuwa katika kiwango cha lami.

"Ninaamini kuwa barabara hizo zikishawekwa lami, zilizosalia zitajengwa kufikia viwango vya kupitika wakati wote kwa ushirikiano wa wananchi, wabunge, halmashauri na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura)," anasema.

Anazitaja barabara nyingine za eneo hilo kuwa ni pamoja Mngazi-Singisa, Dakawa-Bwakila Juu, Dutumi-Kolelo-Kasanga, Msalabani-Tawa mpaka Kibogwa na Kibungo Juu mpaka Nyingwa.

Nyingine ni Mkuyuni (Madamu)-Kinole-Tegetero, Ngerengere-Kwaba-Mkulazi-Kidunda anayosema inaweza kujengwa katika mpango wa ujenzi wa bwawa la maji la Kidunda.

**FURSA ZA MAENDELEO**

Anasema miradi inayopitia Morogoro Vijijini ukiwamo ujenzi wa bwawa hilo, inatoa fursa pana kwa wakazi wa maeneo hayo kunufaika kiuchumi.

"Ninaamini kutakuwepo mtandao wa barabara za lami utakaofungua fursa za biashara na kiuchumi ikiwa ni pamoja na kilimo cha mbogamboga, matunda, ufugaji wa samaki, kuku na mifugo kwa ajili ya masoko hasa ya Morogoro, Dodoma na Dar es Salaam.

Anasema, kutokana na hali hiyo ipo haja kwa wawakilishi wa wananchi bungeni, Prosper Mbena na Omary Mgumba ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo, kusaidia katika kuwaandaa wananchi hasa vijana, kuzitambua na kuzitumia fursa hizo.

Anasema katika kutekeleza hilo, jamii hasa vijana wanapaswa kusaidiwa ili wapate mafunzo ya ufundi stadi yanakayowawezesha kunufaika katika sekta ya viwanda vidogo vidogo vinavyochangia kuifanya nchi kuwa na uchumi wa kati.

**AFYA**

Katika sekta ya afya, Rais Magufuli ameweka historia mpya ya kujenga vituo vya afya vyenye hadhi zaidi ya 300 nchi nzima, vingine vimekamilika na vingine bado vinajengwa ikiwa ni pamoja na hospitali za mikoa na wilaya.

Kwa mujibu wa Mwenegoha, Morogoro Vijijini ni miongoni mwa maeneo yaliyonufaika kwa utekelezaji huo, kutokana na ujenzi wa hospitali ya wilaya kwenye eneo la Mvuha.



Rais John Magufuli (wa nne kulia), akizundua moja ya miradi kabambe katika Hospitali ya Bugando jijini Mwanza.

"Tangu uhuru, wananchi wa maeneo yale tumekuwa tukitegemea hospitali ya wilaya iliyoko Morogoro Mjini, wakati huo ikitoa huduma kwa wenzetu wa Morogoro Mjini na Mvomero tulipokuwa Wilaya moja," anasema.

Anasema iliwalazimu kusafiri umbali wa takribani kilomita 100 kupata huduma za afya, hivyo ujenzi wa hospitali huko Mvuha ni wenye kukidhi moja ya mahitaji yao muhimu.

**ELIMU**

Mwenegoha anasema pamoja na changamoto zilizopo, lakini mpango wa kutoa elimu bila malipo umefungua milango kwa wanafunzi wengi kunufaika, hasa wale wa kutoka familia zilizo na uchumi duni.

Anatoa mfano kwamba, alipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, alishuhudia 'mafuriko' ya watoto wa darasa la kwanza wapatao 1,200 kujiunga katika Shule ya Msingi ya Ibamba iliyopo kata ya Uyovu.

Anasema changamoto iliyojitokeza ni kuwashawishi wazazi kushiriki katika ujenzi wa madarasa ya ziada, kwa vile serikali ilishatoa agizo la kutochangia shughuli zinazohusiana na elimu.

> Ujenzi wa bwawa hilo unahusiana na maagizo ya ilani ya CCM katika kuimarisha vyanzo vya umeme yakiwamo maji.

Anabainisha kwamba Rais Magufuli aliposikia juu ya jambo hili kupitia Vyombo vya habari na Serikali ya Mkoa aliamuru Hazina watume fedha za ujenzi wa madarasa sita mara moja.

Hata hivyo, Mwenegoha anasema baada ya Rais Magufuli kupata taarifa hizo hasa kupitia vyombo vya habari, aliagiza ujenzi wa madarasa hayo ufanyike kwa miezi mitatu na Hazina ilituma Sh. 192,000,000 kwenye akaunti ya shule husika huku halmashauri ya wilaya hiyo ikichangia Sh. 4,000,000.

"Fedha hizo kutumwa ndani ya muda mfupi kulionyesha viwango vya juu vya ufanisi ambavyo Rais Magufuli aliendelea kuviweka kwa miaka minne na kujali wananchi wanyonge kama wale wa Ibamba," anasema.

*0754691540*

## Tshisekedi, Museveni wakubaliana mifumo madhubuti ya ushirikiano

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, amekuwa katika ziara ya siku mbili nchini Uganda ambako alikutana na mwenyeji wake Rais Yoweri Museveni kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa kibiashara wa mwaka 2019.

Wizara ya mambo ya nje ya Uganda imetoa maelezo kuwa wakuu wa mataifa hayo mawili walikutana ili kukamilisha mkakati wa kushirikiana katika masuala ya afya, amani na usalama, nishani, biashara na uwekezaji pamoja na masuala mengine ya maendeleo.

Katika suala la usalama na amani ambayo ni changamoto kubwa kwa mataifa hayo mawili, viongozi hao wameazimia kutafuta suluhu ya kuyaangamiza makundi ya wapiganaji na waasi Mashariki mwa DRC.

Marais hao wanaamini kuwa hiyo ndiyo itakuwa hatua ya kwanza kuleta maendeleo ya viwanda, biashara na uwekezaji eneo hilo.

Viongozi hao wametoa wito kwa wenzao katika Kanda ya Maziwa Makuu kuunga mkono juhudi zao.

Baada ya kukutana kwa siku nne, ujumbe wa DRC uliojumuisha maofisa wa ngazi za juu pamoja na wawakilishi 110 wa wafanyabiashara, waliorodhesha na wenzao wa Uganda masuala ambayo waliyataka viongozi wayazingatie ili kuimarisha biashara kati ya nchi hizo mbili.

Masuala mawili yaliyosisitizwa ni usalama na miundombinu ya barabara.

Walipopokea masuala hayo, marais Museveni na Tshishekedi waliahidi kuanzisha operesheni kabambe kuangamiza makundi ya wapiganaji Mashariki mwa Congo.

Hii wameeleza viongozi hao itatoa fursa kwa wafanyabiashara kutoka pande zote mbili kuendesha shughuli zao na kwa hiyo kuchangia kwa amani, usalama na uthabiti eneo hilo.



Rais Felix Tshisekedi wa DRC (kushoto), akisalimiana na mwenyeji wake Rais Yoweri Museveni wa Uganda. **PICHA: MTANDAO**

Kadhalika Tshisekedi amefichua azimio lake la kuligeuza eneo la Mashariki mwa nchi yake kuwa ndicho kitovu cha viwanda.

Amebaini maeneo sita ambayo yanalengwa ili kulifanikisha hilo na pia katika biashara na uwekezaji sambamba na kujenga barabara za moja kwa moja kutoka Uganda, badala ya kutegemea tu zile zinazopitia Rwanda.

Kulingana na takwimu za serikali, Uganda iliuza bidhaa za thamani ya dola milioni 538 kwa nchi ya DRC huku nchi hiyo yenye utajiri mkubwa wa madini na mbao iliuzia Uganda bidhaa za thamani ya dola milioni 117.

Baadhi ya wafanyabiashara wametaja ushuru, michakato ya uhamiaji ikiwemo ada za Viza za usafiri na pia barabara kuwa changamoto zinazostahili kupewa kipaumbele ili kuboresha biashara kati ya Uganda na DRC.

Biashara ambazo zinatarajiwa kufanywa na mataifa hayo mawili zinakadiriwa kuwa na thamani ya dola milioni 532 kwa mujibu wa ofisi ya taifa ya takwimu Uganda.

Waziri wa mambo ya nje wa Uganda anasema kuwa ushirikiano huo ni mzuri kwa kuwa unazipa nchi hizo mbili wigo mkubwa wa kukua kimaendeleo na kufanya kazi pamoja.

AMANI MASHARIKI YA DRC

Ingawa maeneo karibu yote ya DRC yamekuwa yakikumbwa na changamoto za usalama kama vita ama kushambuliwa na waasi mara kwa mara, eneo la Mashariki ya nchi hiyo ndiyo lililoathirika zaidi.

Akiongea na BBC siku chache kabla ya kuondoka madarakani mwishoni mwa mwaka 2018, rais mstaafu wa nchi hiyo, Joseph Kabila amesema katika mambo ambayo angekuwa na muda zaidi kuyashughulikia ni kurudisha amani kwa taifa hilo. Mashariki mwa DRC kuna makundi ya kijeshi ya waasi na kikabila mengi kupindukia.

Baadhi ya makundi yanaundwa na raia wa nchi hiyo, lakini kuna makundi mengine makubwa ambayo yanafadhiliwa ama kupambana na serikali za nchi jirani. **BBC**

# Ukame, njaa vyakoleza tabu nchini Somalia, Al Shabaab wakishambulia


Distributed via ippmedia

Vikosi vya kulinda amani nchini Somalia, vikiimarisha ulinzi baada ya shambulizi la al Shabaab kwenye kambi ya mafunzo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Anil Kija**

WANANCHI wa Somalia wanatafuta njia ya kutokea kwa jambo ambalo kimsingi wamezoea lakini halizoeleki, yaani mchanganyiko wa ukame na vita vya kigaidi vya kundi la Al Shabaab.

Hali hiyo ni kama imepotea katika anga za kimataifa kwani hakuna majeshi ya nje ila vikosi vya Umoja wa Afrika (AU) vikisaidiwa na Umoja wa Mataifa (UN).

Hapohapo Marekani ina kambi ya kurushia ndege nyuki (drone) kufanya mashambulizi dhidi ya mikusanyiko inayohusu Al Shabaab kama maeneo ya kutoa mafunzo ya kijeshi, au mikutano ya makamanda.

Hata hivyo, uwezo wa kundi hilo wa kufanya mashambulizi ya kushtukiza haujapungua; mwaka huu imeleta simanzi nyingi.

Mashambulizi ya Al Shabaab yanasikika zaidi pale wageni wanaposhambuliwa, kwa mfano hapo Septemba 30 walishambulia msafara wa magari ya maofisa wa Umoja wa Ulaya (EU) na kambi ya jeshi la Marekani ya kuhifadhi ndege nyuki.

Mashambulizi ya ndege hizo, licha ya kuwa zinaruka na kurudi kambini kule zinapopiga, yanapangwa na makao makuu ya Jeshi la Marekani na kuongozwa kitaalamu kutokea vituo maalum huko Marekani.

Kuziweka kambini Somalia ni kuhifadhi tu kupunguza umbali wa kuruka, lakini ni vita ya kielektroniki inayopigiwa Marekani.

Karibu kila mwezi kuna mashambulio au angalau shambulio moja kubwa, na wakati mwingine wanayaunganisha endapo vipigo vya jeshi la Marekani vimezidi, halafu wanalipa kisasi kwa mfano Mogadishu ambapo wanapenda kushambulia ofisi za serikali au viongozi kama meya au waziri.

> Al Shabaab inapata mapigo lakini imepeleka vilio visivyohesabika nchini humo, kwani mashambulizi yake yanapeleka misiba kila kukicha na mara nyingine ni misiba mikuu.

Inaweza kuwa mpaka wa Kenya ambako wanapenda kulipua magari ya polisi, au jijini Nairobi ambako zaidi wanapendelea kupiga mahoteli na kuua watalii, waandishi wa habari, n.k.

Taarifa zinasema mashambulizi ya ndege nyuki za Marekani yameongezeka kuliko mwaka jana.

Waliposhambulia mjini Kismayu hapo Julai 12 dhidi ya hoteli ya Asasey watu 26 walikufa na 56 kujeruhiwa, na miongoni mwa waliokufa alikuwepo raia mmoja wa Uingereza, raia watatu wa Kenya na watatu wa Tanzania.

Lakini aliyetajwa zaidi ni mwandishi wa habari wa Kisomali mwenye uraia wa Canada, aliyefariki pamoja na mumewe akaliliwa na waandishi wa habari maeneo mengi nchi za Magharibi.

Al Shabaab ilipeleka gari la kujitoa mhanga lililoshindiliwa mabomu kuvunja lango ya hoteli hiyo na kulipuka, kuharibu eneo hilo na kuleta mahangaiko, wakati wapiganaji wa Al-Shabaab waliovalia mikanda ya risasi wakipenya na kupiga kila kona.

Mitandao inasema kuwa taarifa za kiinteligensia zinasema kuwa Al Shabaab imekuwa ikiunda Mahakama maeneo inayoshikilia ili kuwanyonga inaokuta na makosa ya kukiuka sheria za jadi zinazosimamiwa na kundi hilo.

Baadhi ya wachambuzi wanaozungumza na maofisa usalama wa nchi za jirani wanasema sababu ni kuwa kundi hilo linataka kuonyesha kuwa lina nguvu, licha ya kupoteza mamia ya wapiganaji kutokana na vita ya ndege nyuki ya Marekani.

Pia kuna mfululizo wa mapambano na askari wa jeshi la Somalia linalojengeka taratibu katika miezi kadhaa sasa.

Al Shabaab pia inapata msaada wa kisaikolojia wa vyombo vya habari nchini Marekani na kwingineko.

Kuna mfano malalamiko kuwa mashambulizi ya ndege nyuki yanaua raia wa kawaida, rai iliyo na maana kuwa ndege hizo zisitumike. Marekani ipeleke askari, au iache vita.

Shirika la uandishi wa habari za upelelezi (Bureau of Investigative Journalism) lilisema kuwa mwendo wa mashambulizi kwa ndege nyuki umeongezeka kwa kasi mwaka huu, kuwa mwaka jana kulikuwa na mashambulizi ya Marekani 47 na mwaka huu yalishafika 50 na inaaminika yameua wapiganaji 300 wa Al Shabaab mwaka huu kwa data zilizokusanywa na kusanifiwa na shirika hilo.

Ni vita ambayo Rais Donald Trump wa Marekani anaiweza, ya kutumia pesa, si kupoteza maisha ya askari katika vita ambayo haina mwisho, kwani inapiganwa kama sehemu ya imani.

Al Shabaab inapata mapigo lakini imepeleka vilio visivyohesabika nchini humo, kwani mashambulizi yake yanapeleka misiba kila kukicha na mara nyingine ni misiba mikuu.

Mara baada ya Al Shabaab kushambulia hoteli moja Nairobi Januari 15 mwaka huu, Marekani iliinua mashambulio ya ndege nyuki dhidi ya vituo vya kundi hilo au mizunguko yao ardhini kama inavyoonekana kutoka angani, na kuua wapiganaji takriban 52 kwa wakati mmoja, lakini kuna raia wa kawaida waliopoteza maisha.

Ni hapo watetezi wa haki za binadamu wanalalamikia ndege nyuki wakati makundi ya kigaidi yanajua lazima yachanganyike na watu ili kujihami.

Katika miaka ya karibuni, shambulio kubwa zaidi la Al Shabaab lilifanyika Oktoba 14 mwaka 2017, linaloaminika kuwa shambulio kubwa zaidi la kundi hilo tangu kuundwa kwake.

Gari la mizigo lililosheheni baruti zilizotegwa kulipuka lililipuliwa katika makutano ya barabara karibu na hoteli ya Safari wilaya ya Hodan, halafu lori la mafuta lililokuwa limeegeshwa karibu na hapo likalipuka pia.

Mkanganyiko huo ukazusha moto mkubwa wakafa watu takriban 500.

Wachunguzi wa habari wanasema Al Shabaab wanafanya mashambulizi kwa kudhamiria na kuvizia, hivyo ingawa Kismayu inapakana na maeneo yanayoshikiliwa na Al Shabaab katika mashamba au mbuga, ambazo mara nyingi zina ukame wa kufa mtu, haushambuliwi sana.

Cha kushangaza ni kuwa alipokufa mwandishi wa habari Hodan Nalayeh, Wasomali walioko nje ndiyo waliopata nafasi ya kueleza masikitiko yao na maombolezo.

Imamu Omar Suleiman ambaye anasalisha huko Texas, Marekani akalaani tukio hilo na habari hizo zinatangazwa katika redio zilizoko maeneo huru Somalia. Inakuwa vita kati ya uhuru na udhalimu, siyo na Marekani.

Wakati Al Shabaab inanyonga watu vijijini na kushambulia mijini kuua maofisa wa serikali na hasa wageni wanaoendesha shughuli za kibinadamu au biashara, kutafuta habari inavyoendelea nchi hiyo, mabadiliko ya tabianchi yanaongezea taabu.

Raia wengi nchini humo wako katika makambi kutokana na vijiji na miji kuteketezwa kwa sehemu kubwa katika vita, halafu jitihada za kilimo zinaharibiwa na mafuriko, kuwahitaji kuhamia maeneo ya mwinuko zaidi.

Mwezi Septemba ulikuwa mbaya kutokana na mafuriko, kwani mawimbi ya vimbunga baharini sasa yanakuwa na uwezo wa kufika ndani ya Somalia kama ilivyo kwingine ukanda huu wa Afrika.

Maafa makubwa zaidi kwa upande huo yalikuwa mwaka 2010 hadi 2012 ambako taarifa zinasema watu karibu 260,000 walikufa katika ukame ulioipiga Somalia, na watu 220,000 walikufa kutokana na ukame mwingine mwaka 1992.

Ukiangalia unakuta kuwa mazingira ya ukame yanaleta maafa makubwa kutokana na udhaifu wa miundombinu kuharibiwa mifumo ya utawala, na pia nchi za Magharibi kutokuharakisha misaada kwa kuhofia kuwa makundi ya wapiganaji nao watachota huko kwani wanashikilia sehemu nyingi zinazokumbwa na ukame.

Ni hali inayokumba nchi za Afrika zenye vita visivyoisha na kuathirika na mabadiliko ya tabia nchi, kuwa matokeo yake ni vifo vya mamia ya maelfu ya watu hasa nyakati za ukame, Somalia ikiwa inaungana na Nigeria (ya kaskazini) na Sudan Kusini.

Yemen inaikaribia Somalia janga hilo.

# Wanawake waliojitosa wang'ae uchaguzi wa Serikali za Mitaa

**Na Elizabeth Zaya**

ZIKIWA zimebaki siku chache kufikia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, hapo Novemba 24, wadau mbalimbali wamewashauri wanawake kujitosa kuwania nafasi kwenye uchaguzi huo.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni miongoni mwa wadau ambao wanajitokeza kutoa rai hiyo kwa wanawake, wakiwataka wabadili mtazamo kwa kupambana na wanaume kuwania nafasi hizo.

Naemy Sillayo ni Meneja Ufuatiliaji Rasilimali kutoka LHRC, ambaye anasema anaona bado wanawake hawajitokezi vya kutosha kugombea nafasi za uongozi kwenye nyanja mbalimbali.

Anasema wanawake ni kundi kubwa ambalo limekuwa likijitokeza kwa wingi kupiga kura kuchagua viongozi.

"Sasa pamoja na moyo wa kujitokeza kuchagua viongozi wao, lakini idadi ya wanawake wanaojitokeza kugombea ni ndogo," anasema na kuongeza:

"Tunafahamu kuna mwitikio kwa kundi hili kujitokeza kupigakura, lakini hatulioni kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi hususani za kisiasa kama linavyojitokeza kupiga kura."

Anabainisha hali hii haiko tu katika uchaguzi wa serikali za mitaa ama uchaguzi mkuu, kote huko idadi yao si ya kuridhisha.

Meneja huyu anasema kama LHRC wanatamani kuona idadi kubwa ya wanawake ikijitokeza kuwania nafasi mbalimbali kwenye chaguzi zijazo.

Anabainisha uwapo wa wanawake wengi katika nyanja mbalimbali za uongozi, kunachagia maendeleo kwa kasi.

"Tunafahamu namna wanawake walivyo na uwezo mkubwa wa kulea na kutunza familia... nguvu ile ile wanayoitumia kutunza familia zao, ndiyo wanatakiwa waitumie kugombea nafasi za uongozi," anasema na kuongeza:

"Tunaamini tukipata viongozi wanawake wengi kuanzia ngazi za mitaa hadi juu katika ngazi za maamuzi, mambo mengi yatakwenda vizuri."

Meneja huyu anabainisha kwamba wanawake wanapokuwa wengi kwenye vyombo vya maamuzi changamoto mbalimbali za kijamii zitapata ufumbuzi kwa sababu wao kama akina mama na walezi wa familia watazisemea kwa uchungu ili zitatuliwe.

### UADILIFU NA UOGA

Ni sifa nyingine ya mwanamke kuwa kiongozi kwa mujibu wa Sillayo.

Uoga wa kufanya mambo yanayoweza kuliingiza taifa katika shida kama vitendo vya rusha na mengineyo.

"Mwanamke ameumbiwa asili ya uaminifu, ni muoga muadilifu. Kwa hiyo, tukifanikiwa kuwa nao kwa wingi katika vyombo vya mamuzi, taifa litakuwa salama, hakutakuwa na wahujumu uchumi wengi," anasema na kuongeza:

"Kinachoendelea sasa nchini katika masuala ya uhujumu uchumi ni ushahidi, wengi wanaoshtakiwa



Naibu Spika Dk. Tulia Ackson (wa pili kushoto), akiwa katika moja ya mikutano ya kuhamasisha ustawi wa wanawake. **PICHA: MTANDAO**

> Tunafahamu namna wanawake walivyo na uwezo mkubwa wa kulea na kutunza familia... nguvu ile ile wanayoitumia kutunza familia zao, ndiyo wanatakiwa waitumie kugombea nafasi za uongozi.

katika kesi za namna hiyo ni wanaume."

### VIKWAZO

Sillayo anataja mfumo dume uliojengwa katika vyama vya siasa kama moja ya vikwazo vinavyowakwamisha wanawake wengi kuwania nafasi mbalimbali za kisiasa.

Anasema mfumo uliopo ndani ya vyama vingi vya siasa, haumpi mwanamke kipaumbele kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, zikiwamo za juu.

"Hakuna mwanamke ambaye ameshika nafasi ya juu kama ile ya mwenyekiti, makamu mwenyekiti au katibu mkuu takribani katika vyama vyote vya siasa," anasema na kuongeza:

"Kwa hiyo unaweza kuona picha kamili ilivyo, na kutokana na vyama hivyo kujijenga kimfumo dume hata mwanamke akijitokeza kugombea katika nafasi za juu, huwa anaonekana ni wa ajabu, na vita ambavyo atapambana navyo ni vikubwa mno na ndiyo maana huwa hawagombei kabisa."

### WAUME

Kwa wanawake walioolewa waume wanatajwa kuwa kikwazo kingine kwa wanawake kuwania uongozi.

Anasema wanaume wengi huwa wanawakatalia wake zao kugombea nafasi za uongozi kwa kuhofia kwamba nguvu zote watawekeza katika shughuli za siasa badala ya kujali familia.

"Unakuta mwanaume anamkataza mke wake kugombea hata kama ameonyesha nia, hofu yao kubwa wanasema kwamba mwanamke anapaswa kujikita zaidi katika kulea familia na si kuhangaika na mambo ya siasa, unakuta wanasema kazi hizo ni za wanaume waachiwe wao," anasema.

### TLB

Rehema Hamis ni mratibu Idara ya Wanawake na Watoto wa Chama cha Wasioona Tanzania (TLB).

Naye anasema la waume kukataa wake zao wasiwanie uongozi ni moja ya sababu hizo.

"Wanaume wengi hawataki kuona wake zao wanasimama kupambana na wanaume kugombea mambo ya uongozi...wanahisi mke asipofanikiwa kushinda atakuwa amemwaibisha hata yeye, lakini pia lile suala kwamba nguvu nyingi atazielekeza kazini kwake na hivyo kusahau familia," anasema.

### WANAWAKE WENYEWE

Rehema anasema sababu nyingine inayosababisha wanawake wasijitokeze kugombea ni kutoungwa mkono na wanawake wenzao

"Hata sisi wanawake wenyewe huwa tunaangushana... wanawake wengi hawaamini kwamba wakimchagua mwenzao atafanya kazi nzuri kama ilivyo kwa mwanaume," anasema na kuongeza:

"Kwa hiyo hata ukipitishwa kwenye kura ya maoni hawakupigii kura, pia kuna wivu, wako radhi wasiende kupigakura hiyo kabisa au wakaamua kumchagua mwanaume ambaye mnashindana naye."

### ILANI YA UCHAGUZI YA WADAU KWA WANAWAKE INASEMAJE?

Ilani ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, iliyotolewa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kwa kushirikiana na Mtandao wa Wanawake na Katiba na Mfuko wa Kuwezesha wanawake (Women Fund Tanzania), ambayo imesambazwa kwa vyama vyote vya siasa, inasisitiza ushiriki wa wanawake katika chaguzi zote.

Aidha, ilani hiyo inavitaka vyama vya siasa kuwa walinzi wa ndoto za wanawake kwa kuwa ndivyo vyenye mamlaka ya kuamua nani aingie na nani aachwe na nani awezeshwe kushinda katika chaguzi.

Mbali na hilo, ilani inavitaka vyama vya siasa kuziba mapengo ya jinsia ndani ya uongozi wa vyama na kujiwekea kanuni zinazowajibisha viongozi wa vyama kutokunyanyasa wanawake, ndani na nje ya vyama.

Ilani hiyo pia, inaimulika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kuhakikisha inatoa miongozo yenye kuvilazimisha vyama kuzingatia haki za wanawake katika ushiriki wao kwenye uongozi wa kisiasa.

Vilevile inawahimiza wapigakura kuwachagua wagombea wanawake.

### VYAMA VYA SIASA

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa ya Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, tayari Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa upande wake kimetoa mwongozo kuhakikisha wanachama wake wanamchagua kiongozi ambaye atathibitika kuwa ni bora, bila kujali hali yake wala jinsia.

Waitara anabainisha hilo baada ya kuulizwa kuhusu nafasi ya mwanamke katika Kongamano la Amani, lililofanyika wiki iliyopita jijini Dar es Salaam.

### NCCR MAGEUZI

Mkuu wa Idara ya Kampeni na Uchaguzi wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Martin Mung`ong`o, anasema chama hicho kimezingatia usawa wa mwanamke katika chaguzi zote.

"Na sisi tuliwapa semina kabisa wanawake ili wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi kwenye uchaguzi ujao na watapewa nafasi," anasema.

### KATIBA

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kuhusu kutoa kipaumbele kwa mwanamke, ibara ya 67(1)( a) na (b), inaeleza kwamba, idadi ya wabunge wanawake wasipungue asilimia 30 ya wabunge wote wa kuchaguliwa na vyama vya siasa kwa kuzingatia uwiano wa kura.

Ilani hiyo ya wadau kutetea haki za wanawake, inataka pia katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, nao utoe kipaumbele kwa wanawake hao.

# Serikali Romania yakwama bungeni

• Ni ya tatu katika miezi saba, miaka 30 baada ya kuanguka kwa Ujamaa



Rais Klaus Iohannis wa Romania. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

NCHI ya Romania ambayo zamani ilivuma sana wakati wa Rais Nicolae Ceauscescu aliyekuwa anapendwa sana na wanamapinduzi wa Afrika licha ya kutokuwa na sifa kama za kina Fidel Casto wa Cuba au swahiba wake Ernesto 'Che' Guevara (mzaliwa wa Argentina) au Ho Chi Minh (Uncle Ho) wa Vietnam, kimsingi imesahaulika katika hisia za kizazi kilichopo, ila katika mpira.

Hata hivyo,ni nchi inayosikika kiasi fulani katika vyombo vya habari kwa wakati huu kutokana na mkanganyiko wa kina wa kisiasa nchini humo.

Majuzi serikali ya tatu (yaani baraza la mawaziri) iliyoundwa katika miezi saba iliyopita imebidi iachie ngazi baada ya kukimbiwa na washirika wake, ikakosa wingi wa kura bungeni.

Kuelewa kinachotokea |Romania inabidi kuangalia kwa haraka utawala wa Nicolae Caeuscescu na jinsi ulivyoanguka, na mpangilio wa kisiasa wa taifa hilo kuanzia mwaka 1989 wakati utawala wa Kikomunisti (yaani mfumo wa Kijamaa) ulipoanguka.

Mfumo wenyewe haukutokana na kufanyika uchaguzi huru na haki halafu wafuasi wa chamacha Kikomunisti wakashinda, ila ni wakati wa kumalizika kwa Vita Kuu ya pili duniani mwaka 1945, ambako majeshi ya Urusi yaliingia Romania na kusafisha mabaki ya utawala wa kifashisti uliowekwa na dikteta Adolf Hitler wa Ujerumani.

Aliweka vibaraka kila majeshi ya Ujerumani yalipoteka na kushinda, iwe ni Ufaransa (ambako alipachikwa Field Marshal Phillipe Petain) au Romania.

Tatizo la kwanza ni jinsi utawala wa Ceauscescu ulivyoanguka, kuwa mazingira mabovu ya uchumi, hasa kuanguka kwa thamani ya sarafu ya nchi hizo kutokana na kutokuwepo uwekezaji kutoka nje (kama ilivyokuwa Tanzania wakati ule) kulisababisha upungufu mkubwa wa chakula na mahitaji mengine.

> Ni katika hali hiyo ambako umoja wa kitaifa uliopo hauparaganyiki, na tofauti za kihisia kuhusu sera zinakuwa za kiitikadi, kama Ujamaa na Ubepari, na siyo za utaifa, ukabila.

Pindi ikasikika kuwa Rais Ceauscescu na mkewe Elena,ambaye alikuwa amemteua kuwa naibu waziri mkuu, wanaishi maisha ya kifahari sana,jambo ambalo (kama ilivyokuwakatika mapinduzi ya Ufaransa 1879 na Ethiopia, kupinduliwa Mfalme Haile Selasie 1974) machafuko makubwa yakaanza na serikali ikakosa nguvu ya kuyazuia.

Ceauscescu hakukimbia; alikamatwa, akashtakiwa, akahukumiwa, akapigwa risasi.

Ina maana kuwa mapinduzi ya Romania ya kuingia katika demokrasia yalitokea katika mazingira ya mgawanyiko mkubwa na mitafaruku ya kisiasa ya kukata na shoka na hapakuwa na uongozi halisi wa kitaifa uliowezesha kufikiwa mabadiliko.

Ina maana kuwa kilichofuata ni mithili ya Mnara wa Babeli, kuwa kila kundi lililokuwa na umoja wa aina fulani pale mwanzoni lilibadilika na kuwa chama, kama ilivyokuwa Tanzania mwaka 1992.

Kufikiwa haraka kwa mfumo wa vyama vingi kulizuia upinzani kukua na kufikia mwelekeo fulani wa kitaifa na badala yake vikaundwa vikundi vyenye mielekeo maridhawa, na vimekuwa vikitegemea wahamiaji kutoka serikalini wenye sifa ya kitaifa kupata ahueni kwa uchaguzi.

Mfumo wa utawala nchini Romania una pande mbili,moja inayoundanisha nchi ambayo ni uchaguzi wa rais (na hiyo kutumiwa kwa madaraka yake) halafu Bunge, ambako rais anamteua kiongozi mwenye uwezo wa kupata wingi wa kura bungeni kupitisha miswada ndiye aunde serikali.

Ina maana kuwa vyama vya siasa nchini humo vimekuwa katika harakati ngumu ya kutafuta kujipanga kwa ajili ya uchaguzi wa rais ambao unatazamiwa kufanyika Novemba 10, na uwezekano ni kuwa baada ya hapo kuna duru ya pili kati ya wagombea wawili wanaoongoza kwa kura.

Si kawaida katikauchaguzi kama huo apatikane kiongozi afike wingi wa kura wa asilimia 50 na ziada kidogo kamakatiba ya nchi inavyotaka.

Kwa upande mwingine, serikali inaundwa na kiongozi wa chama anayeweza kukusanya wingi wa wabunge waliochaguliwa watakaoiunga mkono serikali yake, hivyo kwa sasa rais ni wa kutoka upande wa vyama vya kihafidhina, halafu waziri mkuu anatoka upande wa wanaharakati wa demokrasia, usawa.

Moja ya maeneo muhimu katika siasa za Romania ni migawanyiko ya kitaifa, kuwa inaelekea nchi hiyo imekuwa kimbilio au mchanganyiko wa mataifa mengi katika historia yake, na jambo la kushangaza ni kuwa kila kundi limebaki na hisia zake za utaifa.

Katika mchanganuo au mantiki ya siasa, kubaki na utambulisho wa kitaifa uliokuwepo awali (inafanana na utambulisho wa kikabila katika nchi za Afrika) kunatokana na kutokuwapo kwa kipindi kirefu cha umoja wa kitaifa bila mitafaruku hadi kuingia mfumo wa demokrasia ya vyama vingi.

Ni katika hali hiyo ambako umoja wa kitaifa uliopo hauparaganyiki, na tofauti za kihisia kuhusu sera zinakuwa za kiitikadi, kama Ujamaa na Ubepari, na siyo za utaifa, ukabila.

Kwa upande wa Romania kuna maeneo mawili yaliyosababisha mitafaruku ya kitaifa kutawala kujieleza kisiasa nchini humo, kuwa wakati wa utawala wa kukomunisti hapakuwa na umoja halisi wa kitaifa kwani serikali za kidikteta zina tabia ya kutegemea ndugu wa karibu kudhibiti njama, hila, majaribio ya mapinduzi, n.k.

Kutokana na mtafaruku wa kiuchumi, kijamii na kisiasa uliofikia kupinduliwa na jeshi baada ya maandamano na kuuawa wananchi, hasa huko Srebrenica, halafu akauawa kwa kupigwa risasi kuongozi mkuu wa nchi kwa miaka karibu 25, hali hiyo ilileta simanzi kwa watu wake wa karibu.

Ni hali inayojenga mshikamano wa kitaifa au kikabila, kwani umoja unazuia kupuuzwa katika siasa, au kuonewa.

Pia kuna hali ya kuongezeka nguvu kwa itikadi ya kitaifa iliyopata viti vingi katika uchaguzi wa Bunge la Ulaya kama ilivyokuwa katika nchi kama Italia, Austria na kwingineko, hivyo uchaguzi wa rais mwezi huu unakuwa njia ya kujipanga upya.

Kulingana na matokeo yatakavyokuwa, hasa kujua nani ameshinda uchaguzi wa rais, na hali hiyo inaashiria nini kuhusu nguvu za vyama tofauti bungeni, uwezekano uliopo ni kuwa rais mpya anaweza kulivunja Bunge na uchaguzi mwingine ufanyike, apate wingi zaidi wa Bunge linaloendena na sera zake.

Rais Klaus Iohannis amekuwa msumbufu sana kwa Waziri Mkuu Viorica Dancila kwa kucheza kete za chama hiki kuunga mkono serikali au kujitoa, ikwame bungeni.

Kutokana na uchaguzi wa wabunge wa Ulaya, mrengo wa kulia una nguvu zaidi hivi sasa, lakini kuna matatizo mengine mrengo wa kushoto anakotoka waziri mkuu aliyeachia ngazi, kuwa kama ilivyo kwa Italia hivi karibuni, kiongozi wa chama chenye viti vingi bungeni anatuhumiwa kwa rushwa.

Ni vile vile kamaIsrael, ambako hakuna chama chenye nguvukama Likud ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu lakini kuunda serikali ya mseto mrengowa kulia kumeleta tabu kwani baadhi ya wakuu wa vyama husika hawataki kuwapo katika serikali anayoiongoza.

Moja ya sababu ni kuhofia kupoteza kura kutoka kwa baadhi yawafuasi wao ambao wanampinga Netanyahu kwa tuhuma dhidi yake, sera ziwe kitu kingine.

Ndiyo maana wafuasi wa Rais Iohannis wamethubutu kumpatia tabu Dancilawakati wote wa uwaziri mkuu wake tangu Januari 2018, ilipoundwa serikali nyingine ya mrengowa kushoto baada ya uchaguzi wa Bunge wa mwaka 2016.

Kuikwamisha serikali hii ya mrengo wa kushoto ni kujiweka tayari kwa mahusianotofauti, kwani vyama vya kati vyenye wabunge wachache vinauwezo wa kuwezesha vyama vikubwa vya mrengo huu au ule kuunda serikali.

Vinaweka masharti ya nani awe kiongozi wa serikali hiyo kwa misingi ya kuwa na uhakika kuwa atatekeleza sehemu isiyo ndogo ya madai yao, ambayo ina maana kufikia matumaini ya wapiga kura wao, iwe ni kwa misingi ya kiitikadi (ustawi wa jamii) au wa kitaifa- ambayo ina maana ushiriki wa eneo mojawapo nchini katika ustawi, tofauti na maslahi ya jumla.

Romania ina vyama 36, vingi vikiwa na kiti kimoja bungeni, vingine havina wabunge, na ni chama cha kijamaa pekee kilichovuka wabunge 150 uchaguzi wa mwisho (viti 154 kati ya 329 vya Bunge) kikifuatiwa na chama cha kiliberali chenyeviti 69.

Lakini Rais Iohannis ambaye ni wa chama cha kiliberali ana ufuasi mkubwa miongoni mwa vyama takriban vyote vilivyobaki kuacha kile cha kijamaa, hivyo alipata kura nyingi zaidi duru ya pili katika uchaguzi wa rais kuelekea mwisho wa mwaka 2014.

Umoja katika chama cha kijamaa chenye wabunge wengi ni hafifu kwani ni muungano wa vyama viwili, cha kidemokrasia na cha kijamaa zaidi kilichohitaji hicho kingine kujiweka sawa, na kujiparura kiitikadi.



# Familia yaomba wadau kumsaidia mtoto elimu

Na Nebart Msokwa, MBEYA

FAMILIA ya Neva Mwakazizi ya Kijiji cha Mlowo Wilaya ya Mbeya, imewaomba wadau wa elimu na wasamaria kuwasaidia kumsomesha mtoto wao, Trans Mzumbwe (16) anayeishi na ulemavu.

Ndugu hao wanaomba kusaidiwa wakisema Trans anatamani kufahamu kusoma na kuandika.

Akizungumza na Nipashe nyumbani kwake mama mzazi wa kijana huyo, Mesia Shusa alisema mtoto wake huyo ameshindwa kusoma pamoja na umri huo kutokana na mazingira ya eneo hilo kuwa ya milima.

Alisema alijifungua mtoto huyo kwa mmoja wa wakunga wa jadi wa kijiji hicho na kwamba wakati anajifungua alibaini kuwa mtoto huyo ana matatizo ya miguu na kichwa.

Alisema katika maeneo ya kijiji hicho pamoja na vijiji jirani hakuna shule yoyote ambayo inapokea watoto wenye ulemavu na hivyo ndiyo maana alishindwa kumsomesha.

"Kwa sasa ananisumbua anataka kwenda shuleni na anataka afahamu kusoma na kuandika, tumejaribu kumpeleka katika shule yetu ya Msingi Mlowo wanasema hawana vyumba vya watoto wenye mazingira maalumu," alisema Shusa.

Alisema kwa sasa mwanaye huyo amepata msaada wa kiti cha magurudumu lakini bado hawawezi kumpeleka shule kutokana na uchumi kuwa mdogo na hata mazingira kuongeza ugumu.

**"Kwa sasa ananisumbua anataka kwenda shuleni na anataka afahamu kusoma na kuandika, tumejaribu kumpeleka katika shule yetu ya Msingi Mlowo wanasema hawana vyumba vya watoto wenye mazingira maalumu," alisema Shusa.**

# Wasiojua KKK wapatiwa tiba

Na Nebart Msokwa, MBEYA

KATIKA juhudi za kutokomeza changamoto ya wanafunzi kumaliza darasa la saba bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK), serikali imeanza kutoa mafunzo maalumu ya namna bora ya kuwapima wanafunzi, yanayotolewa kwa walimu na maofisa elimu.

Mafunzo hayo yanayofanywa na Baraza la Taifa la Mitihani (Necta), yalianza kwa majaribio jijini Mbeya juzi na maofisa wa baraza wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Charles Msonde.

Zaidi ya walimu na maofisa elimu 50 wa jiji hilo walishiriki.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo, Dk. Msonde alisema moja kati ya mambo yanawasikitisha wajumbe wa sekretarieti wa baraza hilo ni wanafunzi kushindwa kupata maarifa wakiwa shuleni wakati walimu ambao pia ni maofisa mitihani wapo.

Alisema kazi ya mwalimu au ofisa mitihani ni kufundisha wanafunzi na kuwapima kupitia mitihani, hivyo hakuna sababu ya mwanafunzi kushindwa kupata maarifa endapo atafundishwa na kupimwa kwa mitihani iliyotungwa vizuri.

"Unapofundisha wanafunzi na kuwatungia mitihani tafsiri yake ni kwamba unafanya tathmini ya uelewa wao, mwanafunzi akifanya vibaya unajua kuwa tatizo lake lipo kwenye kipengele fulani hivyo ni rahisi kumkazania kwenye eneo hilo mpaka aelewe," alisema Dk. Msonde.

Alieleza kuwa baraza hilo limeamua kwenda kwa walimu ambao ndio maofisa mitihani ili kujua namna wanavyofundisha na namna wanavyotunga mitihani ya kuwapima ili kuboresha penye mapungufu na kuondoa tatizo hilo.

Alisema endapo walimu watazingatia kufanya tathmini za aina hiyo hasa kwenye madarasa ya chini kabisa, haitatokea wanafunzi kutojua kusoma na kuandika na kwamba watamaliza darasa la saba wakiwa na maarifa ya kutosha.

Ofisa Elimu Msingi wa Jiji la Mbeya, Oscar Kapinga, alisema walimu walioshiriki mafunzo hayo ni wale wanaofundisha kuanzia darasa la pili na walimu wakuu wa shule mbalimbali ndani ya jiji hilo.

Alisema mafunzo hayo yanawahusu zaidi walimu wanaofundisha masomo ya darasa la pili ili kuhakikisha mwanafunzi anaingia darasa la tatu akiwa anazimudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

"Baada ya mafunzo haya tutafanya tena mafunzo ya namna ya kuboresha huu mfumo kwa walimu wengine ndiyo maana yamewashirikisha pia maofisa elimu na wadhibiti ubora," alisema Kapinga.

Vilevile, alisema katika mtihani wa darasa la saba wa mwaka huu jiji hilo limepanda kutoka katika nafasi 68 mwaka jana mpaka nafasi ya 24 kutokana na ushirikiano mzuri kati ya walimu na wadau wengine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, aliushukuru uongozi wa Necta kwa kuanzisha mafunzo hayo ambayo yatasaidia kuboresha usomaji na ufundishaji nchini.

Alisema Mbeya kwa sasa ni miongoni mwa mikoa inayofanya vizuri kwenye mitihani kwa maelezo kuwa ipo kwenye 10 bora kwa kushika nafasi ya saba kitaifa.

Alisema mafunzo hayo yatawaongezea walimu maarifa katika upimaji wa wanafunzi na kuimarisha ufaulu.



Wananchi wakisaidiana kusukuma mzigo wa kuni kwenye baiskeli katika daraja la Mto Mbalizi, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya jana. Matumizi makubwa ya mkaa ni moja ya chanzo cha uharibifu wa misitu na mazingira. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Awaonya watumishi kuwa jela inanukia

Na Nebart Msokwa, MBARALI

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewatahadharisha watumishi wa umma kuepuka kutafuna fedha za miradi ya maendeleo na kuahidi kuwa watachukuliwa hatua za kisheria zikiwamo kushtakiwa na kifungo.

Chalamila alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa anazungumza na wananchi wa Kata ya Utengule- Usangu wilayani Mbarali.

Alikuwa Mbarali kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ukiwemo mradi wa ujenzi wa kituo cha afya cha kata hiyo ambacho kinagharimu zaidi ya Sh. milioni 400.

Alisema ni bora mtumishi akanywa maji ya 'betri' kuliko kula fedha hizo ambazo zinapatikana kutokana na kodi za wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Chalamila alisema watu ambao wamepewa dhamana na serikali ya kusimamia ujenzi wa miradi hiyo ni lazima wawe makini kwa kuhakikisha miradi hiyo inalingana na thamani halisi ya fedha zinazotolewa.

"Fedha hizi ni za Watanzania ndiyo maana tunasisitiza watu wazisimamie vizuri na kuhakikisha hakuna ubadhirifu unaotokea. Yeyote anayejaribu kucheza nazo ni lazima akione cha moto," alionya Chalamila.

Aidha, alisisitiza kauli yake ya kuwatembezea bakora wananchi wote wanaodai kuwa serikali haijafanya maendeleo yoyote tangu nchi ilipopata uhuru wakati kuna mambo makubwa ambayo yamefanyika.

Mlisema kuna baadhi ya watu wanastahili kucharazwa bakora ili waone maendeleo yaliyofanywa na serikali ikiwamo katika sekta ya afya, elimu na miundombinu ya barabara ambayo imejengwa kwa fedha nyingi.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo imepata bahati ya kujengewa vituo vingi vya afya vya serikali na kwamba vipo 14 vilivyojengwa katika halmashauri zote za mkoa huo.

"Lakini kuna fedha zimetolewa kwa ajili ya Hospitali za Wilaya na Wilaya ya Mbarali ni miongoni ambapo ilipewa Sh. bilioni 1.5 ambazo zinatakiwa kujenga majengo saba ya hospitali hiyo," alisema Chalamila.

Diwani wa Kata ya Utengule – Usangu, Samora Msonsa, alisema pamoja na kutoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho lakini pia wananchi wamechangia michango yao na nguvu.


Alisema vilevile halmashauri imechangia kiasi fulani kwa ajili ya mradi huo pamoja na Mbunge pia aliwasidia hivyo mradi huo umebaki kidogo kukamilika.

"Changamoto iliyopo ni kwamba baadhi ya majengo yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi yamekwama kutokana na wananchi kushindwa kutoa michango kwa wakati, sasa tunaomba serikali itusaidie," alisema Msonso.

Alieleza kuwa wananchi walikuwa wanachangishana fedha kutokana na mapato wanayopata kwenye kilimo, lakini kwa mwaka huu wameshindwa kuchangia baada ya hali ya hewa kuwa mbaya na hivyo wakashindwa kuzalisha vizuri.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, alisema kwa sasa kituo hicho kilishafunguliwa na kinafanya kazi.

Alisema wanaendelea na ukamilishaji wa baadhi ya majengo yaliyojengwa na wananchi ili yamalizike.





# Wabunge wataka mchakato sarafu moja EA kukamilika

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WABUNGE wa Bunge la Afrika Mashariki na wa Bunge la Tanzania, wametakiwa kuhakikisha mchakato wa kuwa na sarafu moja ya Afrika Mashariki unakamilika mapema ili kuzifanya fedha za nchi za jumuiya hiyo kuwa na thamani sawa.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Jukwaa la Dira Afrika Mashariki, Israel Ilunde, wakati akizungumza na wanahabari jijini hapa katika kongamano lililowakutanisha wadau mbalimbali wakiwamo wabunge, asasi za kiraia pamoja na viongozi wa vyama vya wanafunzi wa vyuo mbalimbali.

Alisema ili Tanzania iweze kufaidika na sarafu yake kuwa na thamani kama ilivyo ya Kenya, ni lazima kuharakisha mchakato wa kuwa na sarafu moja ambayo itawasaidia Watanzania kunufaika zaidi na fursa za Jumuiya hiyo.

"Tusipokuwa na fedha moja tutakuwa kila wakati tunalalamika biashara zinakuwa ngumu, maana unabeba fedha yako ambayo inathamani ya chini kwenda nchi ya jirani unajikuta bado chenji haitoshi," alisema Ilunde na kuongeza.

"Rais John Magufuli anahangaika kuimarisha uchumi, tunadhani dawa pekee ni Wabunge wa Afrika Mashariki na waliopo Tanzania kuhakikisha kuwa tunaharakisha kuwa na sarafu moja ya Afrika Mashariki, lakini pia tuharakishe jumuiko la Afrika Mashariki ili tuweze kuwa na protoko ambazo zinaweza kuwa pamoja."

Aliwataka Watanzania hasa vijana kutumia vizuri mitandao ya kijamii kuvumbua fursa zinazopatikana katika Afrika Mashariki ili waweze kunufaika nazo, vinginevyo watakuwa wanaangalia nchi jirani zikinufaika na wao kubakia kulalamika.

Akifungua kongamano hilo Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika, Steven Masele, alisema ili kufikia Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kisiasa yenye utawala mmoja na mwelekeo mmoja wananchi wanatakiwa kushirikishwa kikamilifu.

Hata hivyo, aliwataka kuangalia namna ya kujadili suala la jumuiya hiyo kuwa na sarafu moja ambayo utakuwa inawanufaisha Watanzania pamoja na nchi nyingine tofauti na ilivyosasa kila nchi kuwa na sarafu yake.

Mkurugenzi wa Shirikia la Kijerumani la Friedrich Ebert Stiftung (FES), Andreas Quasten, aliwataka Watanzania kuwa wabunifu wa masuala mbalimbali na si kusubiri wengine waanzishe ili wao waje kuchangia.

# Madhehebu yakumbushwa kuwahimiza waumini amani

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

SERIKALI imeyataka madhehebu ya dini nchini kuendelea kuwahimiza waumini wao kulinda amani na mshikamano wa Taifa pamoja na kufanyakazi kwa bidii ili kuinua uchumi wa familia zao.

Ushauri huo ulitolewa jijini hapa na Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga, kwa niaba ya serikali wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Tanzania ni Taifa Baba, kilichoandikwa na Kiongozi Mkuu wa Kanisa Halisi la Mungu Duniani, anayeitwa Baba wa Uzao.

Odunga aliyataka madhehebu ya dini kuendelea kuhubiri juu ya amani na mshikamano wa Taifa hili pamoja na kuwataka waumini hao kufanyakazi kwa bidii ili kujipatia kipato cha familia zao.

"Nimefurahishwa sana kwa namna ambayo Kanisa Halisi la Mungu Baba linaenda sambamba na azma ya serikali ya kuchochea uchumi wa viwanda na kuyataka madhehebu mengine yaige mfano huu mzuri," alisema.

Odunga pia aliwapongeza viongozi wa kanisa hilo kwa jitihada za kufundisha juu ya amani, upendo na uzalishaji mali kwa kuwa mambo hayo matatu ni muhimu sana katika kuchochea kasi ya kukua kwa uchumi wa viwanda hapa nchini.

Aidha, alisema taifa letu lilifanikiwa kujengwa katika hali ya amani bila kubaguana wakristo na waislamu wote wanaishi pamoja na viongozi wa dini wanajukumu la kuhakikisha tunu hiyo inalindwa kwa kushirikiana na serikali.

Akitoa ufafanuzi mfupi juu ya kitabu hicho, Baba wa Uzao, alisema kitabu hicho kimebeba ujumbe, na uthibitisho wa kimaandiko matakatifu ya namna ambayo nchi ya Tanzania imependelewa kuwa na mazingira mazuri ya kuishi.

Alifafanua kuwa kitabu hicho chenye kurasa 39, kinatoa elimu juu ya watu kuishi kwa upendo na kufanyakazi ili kujipatia kipato cha familia zao.

"Kwa miaka mingi tuliaminishwa kwamba Afrika ni bara la giza na kwamba Tanzania ni taifa maskini, hali ambayo ilifanya tuishi kwa utumwa wa fikra, lakini majira yametimia juu ya taifa hili na kuondoa mabaya yote na sasa Tanzania imetukuzwa na mambo makubwa yanatokea yakushangaza dunia nzima," alisema.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na vitu ambayo havipatikani katika sehemu nyingine yeyote ulimwenguni, ikiwa ni pamoja na utajiri wa madini adimu, wanyama, kuwepo kwa hali ya hewa nzuri inayoruhusu mazao mengi kulimwa na uwepo wa Mlima Kilimanjaro




Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula (kushoto), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa mikopo midogo ya nyumba inayotolewa na Benki ya TPB, jijini Dodoma jana. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi na Mkurugenzi wa Masoko na Ukuzaji Biashara, Deogratius Kwiyukwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Matapeli ulipaji wa fidia ardhi watahadharishwa

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amesema kuwa serikali itawafunga jela matapeli watakaojichomeka kwenye malipo ya fidia ya wananchi waliopitiwa na ujenzi wa uwanja wa ndege ambao walikuwa na mashamba yao katika eneo la Kitelela jijini Dodoma.

Tahadhari hiyo imetolewa kutokana na serikali kuonyesha nia ya kuanza kuwalipa wananchi hao waliokuwa wakifanya shughuli za kilimo katika eneo la Kitelela jijini Dodoma.

Katambi alitoa onyo hilo alipokuwa akizungumza na wananchi hao kwenye mkutano uliofanyika Mtaa wa Kitelela Kata ya Miyuji jijini Dodoma ambao ulikuwa kwa ajili ya kuwataka kufanya uhakiki ili kuanza maandalizi ya kulipwa fidia zao. Alisema mapema wiki hii wananchi wataanza kuhakikiwa kwa ajili ya kulipwa fidia zao.

Alisema kuwa serikali ipo makini na haitakubali matapeli hao kujiingiza kwenye malipo hayo, hivyo kama wapo ni vema wajiondoe wenyewa.

"Mimi sina haja ya kuchungulia huko kwenye majina yenu, sasa Rais wetu akingundua ujue jela lazima uende huko ukatumikie kifungo," alisema.

Akizungumza kuhusu uthamini huo, alisema unafanyika kutokana na wananchi hao kudai malipo yao ya fidia toka mwaka 2011, waliposimamishwa kufanya shughuli za kilimo na kujenga.

Katika eneo hilo ambalo serikali inajenga uwanja wa ndege wa kimataifa, jumla ya wananchi 1,053 wanatakiwa kufanya uthamini huo ambao utafanyika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma.

Akizungumza na wananchi hao, aliwataka kufanya uhakiki wao kwa umakini, ili kuepukana na migogoro isiyo rasmi ikiwamo kutojiingiza kwa watu wasiohusika.

Katibu wa Kamati ya Ufuatiliaji, Haruni Mwenda, alisema kuwa kwa kipindi cha miaka tisa wamekuwa wakidai fidia hizo lakini hivi sasa wanaishukuru serikali kwa kuanza kuwalipa.

"Kwa kuwa Rais wetu ni kiongozi wa wanyonge na msikivu sasa tunaamini anayenda kutulipa ili mradi huo mkubwa wa ujenzi huo wa mamilioni ya fedha uweze kufanyika," alisema.



# Marekani kusaidia kuboresha elimu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KAMPUNI ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (VM Ware), kutoka California Marekani, imeonyesha nia ya kushirikiana na Zanzibar katika kuimarisha sekta ya elimu nchini.

Mkurugenzi Mwandamizi wa Mipango na Mikakati anayesimamia elimu, sayansi na teknolojia VM Ware, Thomas Mackay, aliyasema hayo wakati akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ofisini kwake Vuga.

Thomas alisema taasisi yake imejitolea kusaidia nguvu za kitaaluma katika miradi ya elimu kutokana na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Zanzibar katika kuimarisha miundombinu ndani ya sekta hiyo muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Alisema mazingira ya visiwa na ukarimu yameushawishi uongozi wa kampuni hiyo kujitolea kufundisha mbinu na mikakati itakayoibua fursa za kitaaluma vijana na wasomi wa Zanzibar kupata mwanga zaidi.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi hiyo inatoa mafunzo katika mataifa mbalimbali na mkakati wao kwa sasa ni kuona fursa hiyo adhimu inawanufaisha wananchi wa Zanzibar.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema wazo la uongozi wa kampuni hiyo limekuja wakati ambao Zanzibar imeanza hatua za awali katika kuhakikisha Tehama inawafikia walio wengi mijini na vijijini.

Balozi Iddi alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi za kitaifa na kimataifa inaendelea kujenga miundombinu ya madarasa ya masomo ya mtandao wa teknolojia katika ngazi ya msingi ili kuwarahisishia ufahamu wa awali wanafunzi wake wa kujiandaa na taaluma hiyo waingiapo elimu ya juu.

Alieleza kuwa mfumo wa sasa wa Tehama unaotumika duniani unarahisisha kazi za mwanadamu katika harakati zake za kimaisha na kuifanya dunia hivi sasa kuwa kiganja badala ya kijiji.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Simai Mohamed Said, alisema teknolojia hiyo inayobadilika kwa kasi duniani haiwezi kuiacha nyuma sekta ya elimu ambayo ni mzizi wa maendeleo.

Simai alisema katika kuthamini ujio wa viongozi hao wa kampuni hiyo vikao maalum vimeandaliwa vitakavyo washirikisha watendaji wa masuala ya Tehama wa taasisi za umma na binafsi kujadili fursa zitakazopatikana kutokana na ujio huo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kushoto), akizungumza na Ujumbe wa Viongozi wa Kampuni ya Kimataifa ya Elimu na Sayansi kupitia Mfumo wa Kisasa wa Mtandao wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (VM Ware), kutoka California nchini Marekani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kukosa ushiriki chanzo lishe duni

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

USHIRIKI mdogo wa jamii katika masuala ya lishe na chakula bora, umepelekea kuwapo changamoto nyingi katika utekelezaji wa mradi wa lishe katika shule za maandalizi na msingi visiwani Zanzibar.

Mkurugenzi wa Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi katika Wizara ya Elimu, Safia Ali Rijaal, aliyasema hayo wakati akizungumza katika mkutano wa kitaalamu wa kujadili mradi wa lishe.

Mkurugenzi huyo alisema kuna baadhi ya kasoro ambazo walitarajia tayari ziwe zimeshakamilika, lakini kutokuwa na utayari kwa baadhi ya wanajamii kasoro hizo bado hazijapatiwa ufumbuzi.

Aliwataka wadau wa mradi huo wakiwamo maofisa wa halmashauri, wakurugenzi wasaidizi, maofisa wa wilaya, masheha na wananchi kushirikiana pamoja na kujitolea ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa mradi huo.

Alisema ni vyema kila muda kutambua kuwa mradi huo ni wazazi nao kutambua kuwa mradi huo unawasaidia watoto wao, hivyo ni vyema jamii kutoa mchango wao ikiwamo suala la mapishi, maji, kujenga majiko pamoja na utafutaji wa kuni za kupikia.

Aidha, aliwaomba watendaji wakuu wa Wizara ya Elimu, Afya na Kilimo kuwa kitu kimoja kwa kuangalia namna gani mradi huo unatekelezeka.

Mratibu wa Mradi wa Chakula katika Shule za Msingi, Salum Mohd Abdullah, alisema mradi huo kwa kiasi umefanikiwa kutokana na baadhi ya wazazi katika baadhi ya maeneo kuwahimiza watoto wao kwenda shule kama malengo ya mradi ulivyokusudiwa.

Alisema, mradi huo umezingatia hali za kimaisha ukiwa na lengo la kumfanya mwanafunzi aweze kufanya vizuri katika masomo yake kubaki shule wakati wote wa masomo na kuwainua kiwango cha kitaaluma.

Kwa upande wao wawakilishi wa wakurugenzi na maofisa kutoka mikoa inayohusika na mradi huo walisema mwitiko wa wazazi kuwahamasisha watoto wao kwenda shule ni mzuri, lakini bado baadhi ya shule hazina sehemu za kuhifadhia chakula hicho.

Aidha, kinahifadhiwa kwa kamati za shule, pia usafi hauridhishi pamoja na jiko la kupikia halipo salama. Shule 27 zimo katika mradi huo wa lishe shuleni ambazo ni 16 za Unguja na 11 ni za Pemba.

Mradi wa lishe shuleni umeanzishwa kwa lengo la kumaliza utoro kwa wanafunzi ambapo kisingizio kikubwa kilikuwa watoto hawaendi shule kutokana na njaa na wazazi wao hawana fedha za kuwapa ili kununua chakula.

## Apendekeza mikakati kudhibiti unyanyasaji

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, ameonya kuwa watoto wanakabiliwa na madhila ya ukatili na kushindwa kupata haki zao kutokana na kudhulumiwa na kukosa kupata mahitaji yao ya msingi.

Akiwasilisha mada kuhusu haki za watoto kwenye Mkutano Mkuu wa 20 wa Majaji wa Dunia huko nchini India, alisema matatizo hayo yanachangiwa na kukosekana ufahamu kuhusu ulinzi wa haki ya watoto, aibu na vikwazo katika familia zenye migogoro kwa misingi ya imani na kukosa msaada wa uchumi wa familia.

Waziri huyo alisema kuna haja ya kuanzisha utaratibu maalum wa kupambana na unyanyasaji wa aina zote dhidi ya watoto kupitia sheria ya kimataifa inayolinda watoto itakayotekelezwa duniani kote.

"Ukatili dhidi ya watoto uko kila mahali duniani ndiyo maana dunia inapaswa kuungana pamoja katika kupigania na kulinda ustawi wao na kuunda sheria na mifumo madhubuti ya kukabiliana na ukiukwaji wa haki zao," alisema.

Alieleza kuwa ana imani kuwa mkutano huu, umedhamiria kushawishi dunia kuwafanya watoto kuwa huru dhidi ya ubaguzi wa wanaotendewa pamoja na kuwanusuru na majanga yanayotokana na vurugu.

"Bunge moja la dunia linahitajika kwa lengo la kulinda watoto, vizazi vijavyo na jamii kwa ujumla dhidi ya vita vinavyoendelea katika nchi mbalimbali pamoja na matishio ya ugaidi," alisema Mwalimu.

Alieleza kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Tanzania imeridhia mikataba mbalimbali na matamko kadhaa ya kimataifa ya kulinda haki za mtoto.

Alisema kutokana na mikataba hiyo Zanzibar imeweka sera mbalimbali na sheria zinazoendana na mikataba hiyo na kutolea mfano sheria ya mtoto ya mwaka 2011, ya elimu ya mwaka 1982 na sheria ya adhabu ya mwaka 2018 ambazo zimeelezea haki zote za msingi za mtoto na ulinzi wake.

Akielezea haki ya kupata elimu Waziri Khamis, alisema imepewa umuhimu wa kipekee na ndiyo maana sera ya elimu na afya ya Zanzibar, zinazoeleza kuwa elimu bila malipo na matibabu bure kwa kila mtoto na wananchi kwa ujumla. Aidha, aliilezea sheria ya kazi ya mwaka 2005 inayomlinda mtoto na ajira za utotoni pamoja na kuelezea namna Zanzibar inavyochukulia suala la mtoto kwa umakini mkubwa na ndio maana imewekewa wizara maalum.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya jitihada za makusudi katika kukuza haki za watoto kwa kuanzisha dawati maalum la jinsia na watoto kuhudumia waathirika wa unyanyasaji wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia ambayo yapo katika vituo vya polisi.

# Miradi Tasaf sasa yaongeza kiwango uchumi

**Na Elizabeth Zaya, MAKAMBAKO**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) kupitia mpango wake wa kunusuru kaya masikini pamoja na uboreshaji wa miradi mbalimbali inayofadhiliwa na umoja wa nchi zinazozalisha na kusambaza mafuta duniani(OPEC), umeongeza kiwango cha uchumi na kupunguza umaskini kwa wananchi katika Halmashauri ya Mji Makambako.

Akizungumza na wanahabari, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, Paulo Malala, alisema miradi hiyo imesaidia kwa kiwango kikubwa wananchi kuanzisha shughuli zao za maendeleo na kujikomboa na umaskini

Alisema ujio wa mpango wa kunusuru kaya maskini na wananchi kujipatia ajira za muda katika miradi mbalimbali ya OPEC imechangia wananchi kujipatia kipato.

"Tasaf wana mpango wa kunusuru kaya maskini ambao unasaidia kuzipatia kaya zinazothibitika kuwa ni maskini ruzuku ya fedha kidogo kwa ajili ya kusaidia watoto kununua mahitaji mbalimbali ya shule, hospitali, chakula na mahitaji mengineyo, lakini miradi ya OPEC ya uboreshaji wa miundombinu ya afya, barabara, elimu na shughuli za kilimo na ufugaji, wananchi wanapata ajira za muda na kujiongezea kipato," alisema Malala.

Aliongeza: "Na shughuli zote hizo katika miradi ya Tasaf na OPEC wanaozifanya ni walengwa kutoka kaya maskini japo manufaa yanaenda kwa jamii yote wanaokuwa wanaizunguka miradi hiyo katika eneo husika hasa kwenye miradi ya shule, zahanati, barabara na maji."

"Kupitia miradi hiyo wananchi wengi ambao walikuwa hawana uwezo wa kupata milo mitatu kwa sasa wanapata, wanafuga, wanalima na wanaishi kwenye nyumba za kisasa, kwa tathmini hii hapa ndio tunasema miradi hii imeondoa umaskini na imekuza uchumi kwa wananchi wetu, tunaishukuru sana serikali kupitia Tasaf na iendelee kuboresha maisha ya watu."

Ofisa habari wa Tasaf, Estom Sanga, alisema Halmashauri ya Mji wa Makambako imepokea miradi 330 ya Sh.bilioni 13.1 ambayo imetumika katika uboreshaji wa miundombinu, ufugaji, elimu na afya.

**Diwani wa kata hiyo, Balikeka Ramadhani, aliishukuru halmashauri kwa kusaidia kutoa fedha hizo pamoja na za kutoka Serikali Kuu na wananchi wake kuonyesha moyo, hivyo ni jambo muhimu kwa watoto wao ambao walikuwa ukitembea umbali mrefu kufuata elimu.**

# Serikali yawalaani waliokata mikarafuu

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WILAYA ya Wete kisiwani Pemba, imelaani kitendo kilichofanywa na watu wasiojulikana kwa kukata mikarafuu mibichi yenye karafuu, katika shamba la mkulima, Ahmada Ali, lililopo Shumba Vyamboni huko Taifu wilayani Wete.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Wilaya hiyo, Kaptein Khatib Khamis Mwadini, alisema hicho ni kitendo cha uhujumu uchumi wa nchi.

Alieleza wamegundua kuwa waliofanya hivyo ni kwa ajili ya kupata kuni kwa kuuza, jambo ambalo sio utaratibu na unarudisha nyuma maendeleo ya nchi na taifa kwa ujumla.

"Hivi sasa kumezuka mtindo wa baadhi ya wananchi ambao hawapendi maendeleo ya nchi hii kukata miti ya mikarafuu ilhali ikiwa na karafuu, hii sio tabia nzuri na inarudisha nyuma maendeleo yetu," alieleza.

Kaptein Khatib alieleza hadi sasa bado hakuna mtu aliyeshtumiwa kuhusika na hujuma hiyo ila uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na Polisi watafuatilia na atakayepatikana na hatia hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

"Lakini kwa sasa tutakuwa na zoezi maalum la kukamata na kuchukua kuni mbichi za mkarafuu ambazo zinakatwa bila ya kibali kinachotolewa na Idara ya Misitu," alisema Kaptein Khatib. "Nitoe wito kwa wananchi wote wa Kisiwa cha Pemba kuwa zao la karafuu ni zao la kiuchumi, hivyo tunatakiwa tulitunze na tulithamini na mtu yeyote ambae anakwenda kinyume na taratibu za serikali hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake," alisema.

Aliwataka wananchi wote ambao wanajishughulisha na ununuzi wa karafuu kwa kikombe kuacha mara moja kazi hiyo kwani serikali itachukua hatua kali dhidi ya atakayepatikana akifanya jambo hilo.

"Kwa sasa tutapambana nao wale ambao wanajifanya wao wana mamlaka ya kununua karafuu mbichi na hata kavu kwa wananchi wengine, kwani hawa ndio wanaofanya watu waibe karafuu za watu," alisema Kaptein Khatib.

Hata hivyo, alisema wilaya yake imeshamkamata kijana mmoja katika Shehia ya Piki akinunua karafuu mbichi na kesi yake iko mahakamani na kuwataka wananchi kushirikiana na serikali ya wilaya ili kupinga vitendo hivyo.

"Kwa sasa tumeshamfikisha kijana mmoja wa Shehia ya Piki ambaye yeye aliuziwa karafuu mbichi kutoka kwa mwanafunzi wa darasa la tatu na hivi sasa kesi yake inaendelea mahakamani," alisema DC.

Aliwaomba wafanyakazi wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kushirikiana na serikali pamoja na wananchi kuhakikisha karafuu zote zinazochumwa ndani ya wilaya hiyo au nje ya wilaya zinauzwa katika vituo ambavyo vinatambulika na serikali.

Mkulima wa karafuu, Ali Mussa Shehe, mkaazi wa Kizimbani Wete, alisema suala la ukataji wa mikarafuu linawarudisha nyuma kimaendeleo, hivyo ipo haja kwa serikali kuweka ulinzi katika mashamba ya mikarafuu ili kudhibiti wizi na uhalifu unaotendeka kwenye mashamba hayo.

"Kwa kweli wanaokata mikarafuu kwa ajili ya kuni ao mbao wanatuumiza, kwa sababu zao la karafuu ndio tegemeo letu linalotupatia fedha za kujikimu na maisha.

Naye Issa Mohamed Ali, mkazi wa Piki Wete, alisema ni vyema kwa kila anayekata mikarafuu na wanaonunua karafuu kwa wananchi mitaani wakachukuliwa hatua za kisheria kwa haraka, kwani wanarudisha nyuma maendeleo ya wakulima wa zao hilo na Taifa kwa ujumla.

Distributed via ippmedia



Fundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Ubungo, Oscar Godwin, akirekebisha bomba la inchi nane katika eneo la Luguruni, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam juzi, kwa lengo la kuongeza kasi ya upatikanaji na uboreshaji wa huduma ya maji. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Viongozi wa dini waasa wanawake rushwa uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini wamewaasa wanawake kujitenga na rushwa ya ngono, hususan katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maaskofu na Mashekhe ya Maadili, Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini, Askofu William Mwamalanga, amewataka wanawake kujiepusha na rushwa hiyo, pamoja na kuwaonya kuhusu dhambi ya rushwa.

Aliyasema hayo kwenye kongamano la siku mbili linalofanyika jijini Dar es Salaam na kuwahusisha wanawake wawekezaji kutoka mikoa tofauti.

"Siku zote mama ni mama hata kwa baba au mzee mwenye cheo, huu ni wakati wa wanaweke kuwekeza kwenye sekta zote za kimaendeleo na kupinga vitendo vya rushwa za ngono ambavyo vinamdhalilisha sana mwanamke kila uchao, kemeeni wanawake wanaotoa rushwa ya ngono kupata vyeo kwenye ajira serikalini na taasisi binafsi, siasa," aliema Mwamalanga.

Askofu Mwamalanga alisema anasikitishwa na kushamili kwa wasichana wadogo kujiingiza kwenye biashara ya ngono mitaani huku taasisi za wanawake zikiwa kimya, huku sababu kuu ikitajwa umasikini

"Rais Magufuli ametoa fursa kwa wafanyabiashara wadogo kuuza bidhaa kila mahali ili mradi kuna wateja, wanawake jishughulisheni."

Shekhe Ramadhani Mohamed amewataka wanawake kutoka kwenye madhehebu ya dini zote nchini kushirikiana na maaskofu na mashekhe kufichua vitendo hivyo ambavyo kimsingi vinarudisha nyuma maendeleo.

Kongamano hilo limewashirikisha wanawake 3,400 kutoka madhehebu mbalimbali ya kidini na mikoa yote ya Tanzania Bara.

## HABARI KIMATAIFA

# Ukatili wa polisi waibua hasira

**NAIROBI,** Kenya

UKATILI kwa wanafunzi unaodaiwa kufanywa na polisi nchini Kenya umeibua hasira kali miongoni mwa wananchi na katika mitandao ya kijamii.

Kumekuwa na wimbi la ghadhabu kwenye mitandao ya kijamii nchini Kenya kufuatia mashambulio ya kikatili yanayofanywa na polisi dhidi ya wanafunzi.

Hasira hiyo imeibuka baada ya video iliyosambazwa mitandaoni ya maofisa wa polisi walioonekana wakimpiga kwa ukatili mwanafunzi wa chuo kikuu.

Video hiyo ya sekunde 22 iliyorekodiwa kutoka kwenye jengo la ghorofa Jumatatu ilionyesha polisi wanne wakimpiga mateke, kumpiga na kumkanyaga mwanafunzi ambaye alikuwa amelala chini.

Waliorekodi video hiyo wanasikika wakielezea kushitushwa na tukio, ambapo mmoja wao alilia wakati Ofisa wa Polisi akimpiga mateke mwanafunzi kichwani.Video hiyo inamalizika kwa kuonyesha mwanafunzi huyo akichukuliwa na polisi.

**Mashambulizi ya ukatili ya polisi dhidi ya wanafunzi wa vyuo vikuu limekuwa ni jambo la kawaida miongoni mwa mataifa ya Afrika Mashariki.**

Mmoja wa wahariri wakuu wa chombo cha habari nchini Kenya alituma video hiyo kwenye mtandao wa Twitter:

Polisi walipelekwa katika Chuo kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Jomo Kenyatta (JKUAT) jijini Nairobi, baada ya wanafunzi kufanya maandamano dhidi ya ongezeko la matukio ya ukosefu wa usalama.

Inspekta wa polisi nchini Kenya Hilary Mutyambai, hata hivyo alisema kuwa maofisa wa usalama walipelekwa kwenye chuo hicho "kurejesha utulivu" baada ya wanafunzi kufunga barabara kuu na kuanza "kuwanyanyasa madereva wa magari na watumiaji wengine wa barabara".

"Ni muhimu kujua kuwa maofisa wote wa polisi wamepitia katika mafunzo ya kitaaluma katika udhibiti wa ghasia na mikusanyiko isiyo ya kisheria. Matumizi ya nguvu lazima yawe ni ya kisheria na ya muhimu kulingana na mahitaji ya kisheria ," aliongeza.

Ujumbe wa Twitter wa Waziri wa Mambo ya Ndani, Fred Matiang'i alioutuma Jumatatu wiki hii ulisema maofisa wa polisi waliokiuka sheria watachukuliwa hatua:

Taarifa ya ukatili wa polisi dhidi ya wanafunzi imeibua hisia kali mtandaoni huku Wakenya kupitia 'hashtag' #StopPoliceBrutality au #SimamishaUkatili waPolisi wakituma ujumbe kwenye mtandao wa Twitter na kusambaza video ya wanafunzi wa JKUAT wakishambuliwa na polisi.

Maofisa wa chuo hicho waliagiza kufungwa kwa taasisi hiyo ya elimu "kwa muda usiojulikana".

Mashambulizi ya ukatili ya polisi dhidi ya wanafunzi wa vyuo vikuu limekuwa ni jambo la kawaida miongoni mwa mataifa ya Afrika Mashariki.

Tukio hili linakuja baada ya wanafunzi wa vyuo vikuu kama vingine kama vile Chuo Kikuu cha Moi, Masinde Mulilo na Maseno kuandamana kwa sababu mbalimbali wakitaja ukosefu wa usalama.

Wanafunzi wamekuwa wakishambuliwa na maofisa wa usalama kila wanapofanya maandamano, jambo ambalo linalaaniwa na Wakenya.

Mwezi uliopita wanafunzi nchini Uganda waliripotiwa kujeruhiwa baada ya jeshi la nchi hiyo kufanya uvamizi wa usiku katika mabweni yao katika Chuo Kikuu cha Makerere kilichopo katikati ya mji mkuu wa nchi hiyo, Kampala. **BBC**

## Watafiti wa dawa wasahau Waafrika

**LAGOS ,** Nigeria

IMEELEZWA kuwa Waafrika wenye rangi nyeusi wanapata wakati mgumu pale wanapohitaji tiba ya dawa kwa sababu taarifa za vinasaba zinazotumika kutengeneza dawa ni chache.

Kwa ujumla Weusi wanawakilisha asilimia mbili tu ya sampuli ya vinasaba iliyotumika kwenye utafiti wa kutengeneza dawa.

Hata hivyo kampuni mpya ya Nigeria inataka kubadili mfumo huo na kuhakikisha kuwa Waafrika wanapata dawa na kutibiwa.

Uhaba wa utafiti kuhusu watu wa aina fulani unahatarisha kuenea kwa magonjwa duniani kote.

Kwa mujibu wa muasisi na mkurugenzi wa kampuni inayotafiti biolojia ya vinasaba ya 54gene' , Dk. Ene-Obong, watu wenye rangi nyeusi wana tofauti za kimaumbile na watu wengine duniani, hivyo kutengeneza taarifa zao za vina saba kunahitaji rasilimali kubwa zaidi ili zipatikane.

Alisema amefanya utafiti wa vinasaba katika maabara ya nchini Nigeria katika mji wa Lagos, ambapo timu yake ina mpango wa kufanyia utafiti wa vinasaba 4,000 vya sampuli zitakazokusanywa kwa mwaka 2019, kwa malengo ya kufikia watu 100,000 ifikapo 2020.

Dokta Obong alisema kuwa ufahamu wa jukumu la vinasaba katika magonjwa litasaidia katika uhusiano wa maradhi na tiba . **BBC**



Mgonjwa akimeza dawa. Licha ya kuwapo tiba inaelezwa kuwa nasaba za Waafrika hazijahusishwa kwenye kutengeneza dawa hizo.



Umma katika mji wa Ghaza ukiubeba mwili wa kamanda Baha Abu Al-Atta aliyeuawa na Israel jana. **PICHA : MTANDAO.**

# Kamanda Islamic Jihad auawa

**DAMSCUS,** Syria

ISRAEL imetangaza kumuua Kamanda wa kundi la wanamgambo wanaoungwa mkono na Iran la Islamic Jihad katika shambulio lililofanywa kwenye Ukanda wa Gaza jana.


Aidha, wakati wa kumuua ilimshutumu kwa kufanya mashambulizi kadhaa katika mpaka wake na kupanga mashambulizi zaidi dhidi ya Israel.

Shirika la habari la Syria lilisema kwamba Israel pia imefanya shambulio la kombora lililolenga nyumba ya ofisa wa kundi hilo mjini Damscus na kumuua mmoja kati ya watoto wake.

Kwa mujibu wa shirika hilo kuuawa kwa Baha Abu Al-Atta (picha ndogo), katika nyumba yake mjini Gaza kunaonekana kutoa changamoto mpya kwa kundi la Hamas linalotawala ukanda wa Gaza.

Hamasa imekuwa ikijaribu kuendeleza hatua ya kusitisha mapigano na Israel tangu katika vita vya mwaka 2014.

Kundi la Islamic Jihad lilisema mke wa Al-Atta pia, aliuawa katika mlipuko huo ambao uliharibu jengo hilo mjini Gaza katika wilaya ya Shejaia mapema alfajiri ya jana. **DW**



# Jaji Mkuu afunguka athari maandalizi hafifu mashtaka

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amesema maandalizi hafifu ya hati ya mashtaka katika kesi yanaweza kusababisha upelelezi wa kesi kutofanyika na kuwa chanzo cha kutotendeka kwa haki.

Aidha, jambo hilo husababisha mfumo wa sheria kutoaminiwa na wananchi.

Akizungumza katika ziara ya kikazi mkoani Rukwa, Jaji Mkuu aliishauri serikali kufanya tathmini ya kazi inayofanywa na wapelelezi pamoja na waendesha mashtaka katika kesi iwapo wanatekeleza wajibu wao ipasavyo.

Alisema Mahakama ya Tanzania inakabiliwa na changamoto ya kesi kutomalizika kwa wakati na wakati mwingine haki kutotendeka kutokana na wapelelezi pamoja na waendesha mashtaka kutotekeleza wajibu wao ipasavyo.

Aidha, aliishauri serikali kuwabana wapelelezi na waendesha mashitaka ili wawe wanajiandaa vizuri katika kesi mbalimbali.

Kwa mujibu wa Jaji Mkuu, endapo kutakuwa na maandalizi hafifu ya hati ya mashtaka katika kesi husababisha upelelezi wa kesi hiyo kutofanyika inavyotakiwa, hivyo wakati mwingine kusababisha haki kutotendeka na kusababisha mfumo wa sheria kutoaminiwa na wananchi.

Alisema matumizi ya Tehama katika kesi yatarahisha na kusaidia haki kutendeka na kesi kumalizika kwa wakati, huku akitolea mfano wa matumizi ya kipimo cha vinasaba kwenye kesi kubwa kama za mauaji na ubakaji.

Akitolea mfano wa kesi kwenye Mahakama ya Rufani, Jaji Mkuu alisema wakati mwingine Majaji hukutana na changamoto ya maandalizi hafifu ya hati ya mashtaka kwa kuwa inakuwa haiendani na tukio lenyewe.

Alisema kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia, wapelelezi hawanabudi kuchukua maungamo ya kesi kwa njia ya picha za video.

"Upelelezi bado uko karne ya 16 wakati wahalifu wako karne ya 21," alisema Jaji Mkuu.

Kuhusu Mahakama kuanza kutoa hukumu kwa lugha ya Kiswahili, Jaji Mkuu alisema suala hilo ni muhimu na Mahakama italifanyia kazi.

Aliongeza kuwa hivi sasa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, kinatoa mafunzo kwa Mahakimu ya uandishi wa hukumu kwa lugha nyepesi na inayoeleweka zaidi.




Meneja Masoko wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Alina Maria Kimaryo (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa droo ya kwanza ya kampeni ya akaunti ya 'Malengo', ambapo wateja watano, walijishindia zawadi ya bodaboda kila mmoja. Wengine ni maofisa wa benki hiyo na mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wazalishaji wa mkaa mbadala washauriwa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imewataka wazalishaji wa mkaa mbadala kuhakikisha wanaboresha bidhaa hiyo ili ikidhi viwango na kuongeza watumiaji ambao sasa wanatumia mkaa unaoharibu mazingira.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Mradi wa kuwezesha wazalishaji kuzalisha mkaa mbadala, Deogratius Nyangu, kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kamati hiyo ambayo ipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais juzi ilikaa kupitia taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa mradi huo ambao unatekelezwa baada ya kupatikana washindi watatu wanaozalisha mkaa mbadala na majiko.

Mradi huo unasimamiwa na Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED) na kufadhiliwa na kampuni ya Shell Exploration and Production Tanzania ambapo mshindi wa kwanza alipata Sh. milioni 300, mshindi wa pili Sh. milioni 200 na mshindi wa mwisho Sh. milioni 100.

Nyangu alisema mradi huo ambao unatekelezwa kwa miaka mitatu mpaka sasa washindi wameshapatiwa fedha kwa awamu mbili na iliyobaki ni awamu ya mwisho.

Alisema wamejiwekea kabla ya kutoa fedha, wamekuwa wakikutana hupitia taarifa za washindi hao kujua changamoto na mafanikio waliyopata baada ya kuwezeshwa kifedha.

Mkurugenzi wa Taasisi ya IMED, Dk. Donath Olomi, alisema licha ya uzalishaji wa mkaa mbadala kuongezeka, bado baadhi ya watu wana uelewa mdogo wa matumizi yake.

Alisema wazalishaji hao wa mkaa na majiko yake kwa sasa soko lao kubwa lipo kwenye taasisi za umma, vyuoni na wafanyabiashara wanaojihusisha na upikiaji wa vyakula.

# Dawa ya wanaotesa wanyama yapatikana

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

KAMA ulizoea kutompa chakula, maji, kumsababishia maumivu, majeraha au woga mnyama unayemfuga kwa makusudi na nia mbaya, ukikutwa kiwango cha faini kuanzia Sh. 500,000 hadi 1,000,000 itakuhusu.

Wabunge walipitisha adhabu hiyo jana mjini Dodoma baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Prof. Adelardus Kilangi, kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali namba 7 wa mwaka 2019.

Muswada huo ulipendekeza kufanya marekebisho katika sheria 11 ikiwamo Sheria ya Ustawi wa wanyama, kifungu cha 59 ili kuongeza idadi ya vitendo ambavyo ni makosa chini ya sheria hiyo.

"Kwa mujibu wa marekebisho hayo, itakuwa ni kosa mtu asipohakikisha kuwa wanyama walio chini ya uangalizi wake wanaishi bila njaa, kiu, woga, maumivu au majeraha," alisema Prof. Kilangi na kuongea:

"Sheria inapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza ukubwa wa adhabu kwa makosa mbalimbali yaliyoanishwa chini ya sheria na kuongeza kiwango cha fedha ambacho Mkurugenzi anaweza kuagiza mtu alipe palepale wakati amefililisha makosa," alisema Prof. Kilangi.

Alisema katika Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Sura ya 156, kifungu cha 62 kinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kuhuisha upya adhabu na makosa mbalimbali chini ya sheria hiyo.

Alisema kifungu cha 62A kimeongezwa ili kuweka mfumo wa kufililisha makosa, jambo ambalo litaepusha mchakato mrefu wa mashtaka na hivyo kuokoa gharama na muda na kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani kwa makosa madogo ambayo yanaweza kufililishwa.

MAZISHI YA VIONGOZI

Prof. Kilangi alisema Muswada huo umependekeza marekebisho katika sheria ya mazishi ya viongozi wa kitaifa, sura ya 419, kwamba marekebisho ya jumla yanafanyika kwa kuondoa masharti yanayohusu uanzishwaji wa makaburi ya kitaifa na usimamizi wake.

Alisema msingi wa marekebisho hayo ni kuwawezesha viongozi au familia zao kuwa huru kuchagua mahala pa kuzikwa kwa kuheshimu tamaduni, mila na dini zao.

"Vifungu vya 5, 7, 13, 20 na 21(2) vinarekebishwa kwa lengo la kutambua viongozi wa kitaifa wa Zanzibar katika masharti mbalimbali ya Sheria hii yanayohusu taratibu za mazishi ya viongozi, kuainisha muda wa maombolezo wa Rais wa Zanzibar na Rais Mstaafu wa Zanzibar na kuimarisha ushiriki wa viongozi wa Zanzibar katika Kamati Tendaji," alisema Prof Kilangi na kuongeza:

"Aidha, kifungu cha 9 kinarekebishwa kwa lengo la kuainisha kipindi cha maombolezo pale wakati Spika au Jaji Mkuu atafariki. Sheria ilivyo sasa haijaainisha muda wa maombolezo kwa viongozi hao. Kifungu cha 11 kinarekebishwa kwa kumfanya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Mazishi."

Alisema lengo la marekebisho hayo ni kuruhusu kiongozi wa kitaifa kuzikwa katika eneo ambalo familia yake itaamua azikwe au kwa kuzingatia wosia wake.

Alisema pamoja na kuruhusu hilo, mazishi yatafanyika kwa taratibu za mazishi ya kitaifa au kiserikali kama zilivyoainishwa kwenye sheria.

Akichangia muswada huo, Mbunge wa viti maalum (Chadema), Suzan Lyimo alisema kwa mila za Watanzania hakuna ndugu watakaokubali kwenda kuzika kwenye makabuli ya kitaifa.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele njengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

## NAFASI ZA KAZI

**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Mawasiliano piga 0714 634 046. Piga simu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni tu.

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**


## MCHANGANYIKO

**GENERATE MONEY AND JOBS* Learn DESIGNING** winning project proposals *Find DONORS *Establish NGO 0784505108 /0769505108.

**MONKAL I INSULIN**:Inawasaidia wagonjwa waliogua kisukari kwa muda mrefu,inarejesha kongosho ktk utoaji ute mchungu na sukari kuwa normal balance 4- 5- 6, iko katika mfumo wa maji na vidonge,husaidia mmengenyo wa chakula,tiba lishe,gout,uzazi,tumbo la vidonda na kuunguruma na kujaa gesi n.k :0713293988/0758078280.

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe***

## KUPOTEA KWA CHETI




**EMMANUEL PAULO THOMAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S4847/0038** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari PEACE LAND mwaka 2015.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/KIJ/RB/466448/2019.**

115514702

## KUPOTEA KWA CHETI



**Huston J. Mrangu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3948/0112** kilichotolewa na Baraza ka Mithihani la taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari Enduimet.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: DAR/SEL/RB/462154/2019**

115514202


## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**GASPER LUCAS MIRAJI** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.3885/0559/2019** iliyotolewa na WENDA HIGH SCHOOL mwaka 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Control No. 991230678934.**

115514902

## KUPOTEA KWA VYETI



**FROLIAN JOSEPH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0304-0092** kilichotolewa na BUKOBA SEKONDARI mwaka 2005.

Cheti cha kidato cha sita kilichotolewa na **MKANDAWILE HIGH SCHOOL** mwaka 2008.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: KMR/B.I/I/VOL. IX/65.**

115514602

## KUPOTEA KWA VYETI




**DEVOTHA NZUNDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0538-0013 kilichotolewa na VWAWA SEKONDARI mwaka 2003. Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0203-0527** kilichotolewa na IRINGA GIRLS SEKONDARI mwaka 2006. Cheti cha Chuo S/N 4997 kilichotolewa na Mzumbe University mwaka 2009.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
NJ/A.17/14/VOL **XX/102.**

115514502

## KUPOTEA KWA CHETI



**Irene Joseph Siame** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2768-0014** kilichotolewa na Baraza ka Mithihani la taifa mwaka2014 katika Shule ya Sekondari Ulongoni.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/STA/RB/465840/2019**

115514802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**


**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;223/2019**

**Ombi la ARUSIA BALELE SHOSHA**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu**
**SALAWA MAGOMBALO ZIZI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/11/2019



115514302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOHN KISAK BENJAMINE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 526 AMA** Chassis namba **AT1910033206.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/TR/43656/2019**

115513902

## KUPOTEA KWA CHETI



**Tausi Emmanuel Namtamwa** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0989-0029 kilichotolewa na Baraza ka Mithihani la taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Kibara. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/314714/2019**

115513702

## KUPOTEA KWA CHETI



**DORIS JONAS KANWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1481/003** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari YOMBO mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/463647/2019.**

115514002

## WACHIMBAJI VISIMA TANZANIA.

Tunachimba visima virefu na vifupi katika mikoa yote Tanzania kwa gharama nafuu!!,

Simu: 0623 528 465/ 0657 746 365/ 0692 006 546.




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# PULISIC AONDOLEWA KIKOSI CHA MAREKANI



**LONDON,** England

NYOTA wa Chelsea, Christian Pulisic ameondolewa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Marekani, kutokana na maumivu ya nyama za paja na kiuno.

Winga huyo alikuwa sehemu ya kikosi cha awali kwa ajili ya Ligi ya Mataifa ya CONCACAF dhidi ya Canada na Cuba mwezi huu.

Hata hivyo, kocha Gregg Berhalter amethibitisha kwamba baada ya makubaliano ya wao wawili wameamua kutoongeza hatari ya kuumia zaidi kwa Pulisic na hivyo kuachwa kikosini.

"Christian kwa sasa ameondolewa kwenye kikosi. Hayo yalikuwa makubaliano ya klabu, tukiangalia na ufiti wa mchezaji mwenyewe," alisema.

"Maamuzi hayo mara zote ni magumu kwa sababu kundi la benchi la ufundi na wachezaji wanataka kumuona Christian hapa, lakini ingekuwa hatari kumjumuisha kwenye kikosi kwa wakati huu."

Pulisic amekuwa kwenye kiwango kizuri pale Chelsea ambako kwa sasa wanashika nafasi ya tatu kwenye msimamo, akiwa amefunga mabao matano katika mechi tisa alizocheza tangu alipoanza kucheza pale Stamford Bridge.

# Mancini: Balotelli ana nafasi Italia

**ROME,** Italia

ROBERTO Mancini hatamuita Mario Balotelli kwenye kikosi cha Italia kwa sababu ya kuzima kelele za ubaguzi, kwani ataitwa pale atakapokuwa kwenye kiwango bora.

Na pia Mancini amesema mshambuliaji huyo wa klabu ya Brescia bado ni kijana na ana nafasi kwenye kikosi cha Azzurri.

Balotelli mwenye umri wa miaka 29, alipigiwa kelele za ubaguzi na mashabiki wa Hellas Verona wakati wakishinda 2-1 mwezi huu na alitishia kuondoka uwanjani.

Verona ilipewa adhabu ya kucheza mchezo mmoja wa ligi bila mashabiki, huku klabu hiyo ikimfungia kocha mkuu, Luca Castellini kutojihusisha na soka kwa kipindi cha miaka 11, baada ya kufanya mahojiano na redio moja na kuonyesha kuwaunga mkono mashabiki kwa ubaguzi wa rangi.

Balotelli alirudi nchini Italia mwaka 2018 baada ya kucheza nje kwa miaka minne na hajakuwapo kwenye kikosi cha timu ya taifa tangu alipocheza kwenye sare ya 1-1 dhidi ya Poland Septemba mwaka huu.

Mancini, kocha ambaye alimpa nafasi ya kucheza Balotelli kwenye kikosi cha Inter mwaka 2007, amesisitiza kwamba bado anaiona nafasi ya nyota huyo kwenye kikosi cha timu hiyo, kama tu kiwango chake kitaimarika.

"Soka ni mchezo ambao unaunganisha watu na sio kuharibiwa na watu wachache. Nitamuuita Balotelli kikosi cha Italia pale tu kiwango chake kitakapokuwa kimeimarika zaidi," alisema Mancini akiwaambia waandishi wanahabari.

"Nampenda Mario. Nilimpa nafasi ya kucheza kwa mara ya kwanza akiwa kijana mdogo. Bado ni kijana kutosha na anaweza kupata nafasi kwa siku za usoni, lakini kwangu mimi nitamuita tu pale ambapo kiwango chake kitakuwa kimeimarika."





# *Emery ahakikishiwa Arsenal akionywa*

**LONDON,** England

UNAI Emery ameungwa mkono hadharani na viongozi wa juu wa Arsenal, lakini ameonywa kuhakikisha timu inapata matokeo.

Nafasi ya Emery pale kwenye Uwanja wa Emirates imekuwa katika sintofahamu baada ya kushinda mechi mbili tu kati ya 10 zilizopita za Ligi Kuu ya England.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Soka wa Arsenal, Raul Sanllehi na Mkurugenzi Mkuu, Vinai Venkatesham wamesema kwa sasa hawana mpango wa haraka wa kubadilisha kocha.

"Bado tuna imani na Unai kwamba ni mtu sahihi kwa kazi hii," waliwaambia viongozi wa Arsenal kwenye kikako chao.

"Wote haturidhishwi na matokeo kama ilivyo kwa shabiki mwingine yeyote pamoja na kiwango cha timu.

"Tunajua hisia za mashabiki na pia sisi hatujaridhishwa na kiwango cha timu, kwani wengi walikuwa na matarajio makubwa na Unai.

"Lakini kwa sasa hatuna mpango wa kufanya mabadiliko ya kocha, kwani tunachokitaka kutoka kwake ni kuhakikisha matokeo yanaimarika uwanjani ili kufikia malengo yetu ya msimu huu."

## HABARI MICHEZO

# Deschamps: Martial ana nafasi Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

ANTHONY Martial bado yupo kwenye sehemu ya mipango ya kikosi cha Ufaransa licha ya kwamba, mshambuliaji huyo hajachaguliwa kwenye timu yake, amesema kocha, Didier Deschamps.

Nyota huyo wa Manchester United amekuwa kwenye kiwango kizuri tangu arudi dimbani akiwa na 'Mashetani Wekundu' hao baada ya kupona nyama za paja ambapo alikaa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi miwili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefunga mabao matatu kwenye mechi sita zilizopita na amekuwa akichezeshwa kwa pamoja na Marcus Rashford na Daniel James pale Old Trafford.

Hata hivyo, Martial – ambaye alichezea kwa mara ya mwisho Ufaransa kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Urusi, Machi 2018 – ameondolewa kwenye mchezo wa kufuzu Euro 2020 dhidi ya Moldova na Albania.

Lakini Deschamps amesema kwamba, ataweza kumtumia kwa siku za usoni.

"Alikuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa lakini hivi karibuni amekuwa akiumia mara kwa mara," alisema.

"Alirudi lakini si kwa muda mrefu na bado anaendelea vizuri kwa nafasi yake ya ushambuliaji wa kati pale Manchester United.

"Lakini atakuwapo kwenye kikosi cha wachezaji ambao wataitwa mara kwa mara kwenye kikosi hicho."

Olivier Giroud amejumuishwa kwenye kikosi cha Ufaransa licha ya mshambuliaji huyo kutokuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara pale Chelsea msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amecheza mechi sita tu kwa dakika 120 kwenye Ligi Kuu msimu huu.





# GUENDOUZI ACHUKUA NAFASI YA MATUIDI

**PARIS,** Ufaransa

UFARANSA imemjumuisha kiungo wa Arsenal, Matteo Guendouzi kuchukua nafasi ya Blaise Matuidi ambaye ni majeruhi kwa ajili ya mechi za mwisho za kufuzu kwa Euro 2020.

Nyota wa Juventus, Matuidi alifanyiwa uchunguzi Jumatatu jijini Turin na alicheza kwa dakika 70 Jumapili wakati wakiibuka na ushindi wa 1-0 kwenye mchezo wa Serie A dhidi ya AC Milan.

"Kiungo alifanyiwa vipimo vya MRI, ambapo ulionyesha kwamba ameumia mbavu," ilisema taarifa ya klabu ya Juve.

"Kwa bahati mbaya nipo nje ya kikosi," aliandika Matuidi kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter.

"Lakini naamini Ufaransa itafuzu kwenye michuano hii. Naangalia uwezekano wa kurudi kwenye kikosi siku zijazo."

Shirikisho la Soka la Ufaransa, limethibitisha kwamba Guendouzi alijiunga na kikosi cha Ufaransa pale kwenye kambi ya Clairefontaine juzi Jumatatu.

Mabingwa hao wa dunia watafuzu Euro 2020 kutoka kwenye Kundi H kama wataifunga Moldova jijini Paris kesho Alhamisi, au kama Iceland haitashinda dhidi ya Uturuki.

Ufaransa itamaliza mchezo wake wa mwisho wa kufuzu kwa Euro dhidi ya Albania Novemba 17, mwaka huu.

# Kompany apinga City kusajili beki wa kati

**LONDON,** England

VINCENT Kompany amesisitiza Manchester City haihitaji kusajili beki wa kati kwenye kipindi cha usajili wa dirisha dogo Januari mwakani.

Kompany, nahodha wa zamani wa City na beki wa kati, aliondoka na kwenda kujiunga na Anderlecht kipindi cha majira ya joto kilichopita bila kupata mbadala wake na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu wamepoteza beki mwingine, Aymeric Laporte, ambaye atakuwa nje ya dimba kwa muda mrefu.

Imewaacha wao na beki wa kati wawili tu ambao ni John Stones na Nicolas Otamendi.

Hata hivyo, Kompany anahisi kwamba, City hawahitaji beki kwa sasa licha ya kuwa nyuma kwa pointi tisa kutoka kwa vinara wa ligi hiyo, Liverpool baada ya kufungwa Jumapili mabao 3-1 pale kwenye Uwanja wa Anfield.

"Sidhani kama wanahitaji kumsajili beki," alisema Kompany akisema akiiambia Sky Sports.

"Mara zote tulikuwa tunapata tabu sana pale Anfield. Nilisema kwenye mchezo wa Jumapili wanatafuta kumaliza miaka 25 bila kushinda mchezo wowote Anfield na vigumu, kucheza na timu ambayo kishitoria inakunyanyasa.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GOMEZ CHANZO SOUTHGATE KUMTEMA STERLING ENGLAND

FA inaweza kuthibitisha kuwa Alhamisi hatajumuishwa katika kikosi kitakachocheza mechi ya...

**LONDON,** England

RAHEEM Sterling hatajumuishwa katika kikosi cha England kitakachocheza mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Montenegro kufuatia taarifa ya mpasuko uliopo kati ya mshambuliaji huyo wa Manchester City na beki wa Liverpool, Joe Gomez.

**Sterling na Gomez inaelezwa walitibuana na kutaka kukwidana wakati England ikiwa mazoezini St George's Park.**

Tukio hilo linaelezwa lilichochewa baada ya Liverpool kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya City kwenye mchezo wa Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Anfield.

Imeripotiwa kuwa wachezaji wenza wa England walilazimika kuwatenganisha wawili hao, ambao kabla hapo Jumapili walitibuana wakati Liverpool ikizidi kujichimbia kileleni kwa pointi nane zaidi.

Sterling ataendelea kubaki na kikosi cha England, ambacho kinahitaji pointi moja tu ili kujihakikishia nafasi ya kufuzu michuano hiyo, lakini taarifa ya Chama cha Soka England imethibitisha hatacheza dhidi ya Montenegro.

"FA inaweza kuthibitisha kuwa Alhamisi Raheem Sterling hatajumuishwa katika kikosi kitakachocheza mechi ya kuwania kufuzu EURO 2020 dhidi ya Montenegro itakayopigwa Uwanja wa Wembley kama matokeo ya usumbufu katika eneo la timu binafsi kwenye Uwanja wa St. George leo [jana]. Atabaki na kikosi," taarifa ilisomeka.

Kocha wa England "Three Lions", Gareth Southgate aliongeza: "Tumechukua uamuzi wa kutomjumuisha Raheem katika mechi dhidi ya Montenegro Alhamisi.

"Changamoto moja kubwa na nguvu, tumeweza kutenganisha uhasama uliopo katika klabu na timu ya taifa. Kwa bahati mbaya hisia za mchezo wa jana zilikuwa bado mbichi.

"Hisia zangu ni kwamba jambo sahihi kwa timu ni hatua ambayo tumeichukua.

"Sasa uamuzi umeshafanywa na makubaliano ya kikosi kizima, ni muhimu kwamba tunawasapoti wachezaji na kuangazia Alhamisi usiku."

Sterling amekuwa katika kiwango cha kuvutia kwa England wakati wa mechi za kuwania kufuzu, akifunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho tano.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliendelea kuonyesha ubora dhidi ya Liverpool, lakini City ilishindwa kujibu kipigo cha mabao kutoka kwa Fabinho, Mohamed Salah na Sadio Mane huku wakipata la kufutia machozi kupitia kwa Bernardo Silva dakika ya 77 ambalo halikuwasaidi kuwazuia wapinzani wao kuibuka na pointi tatu.

Baada ya mechi hiyo na Montenegro kwenye Uwanja wa Wembley, kikosi hicho cha Southgate kitahitimisha mechi zake za kuwania kufuzu Euro dhidi ya Kosovo itakayopigwa Pristina Jumapili.

## ZISIKUPITE

### EMERY APEWA MECHI SITA

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery atapewa mechi sita zijazo kuthibitisha kwamba bado ni mtu sahihi wa kuinoa miamba hiyo ya Emirates. ***(Standard)***

### UNITED KURUDI KWA ZAHA

MANCHESTER United ipo katika mchakato wa majira ya joto kumsajili mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, 26, kwa mara ya pili na ipo tayari kulipa pauni milioni 70 kwa nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, ambaye aliitumikia kati ya mwaka 2013 na 2015. ***(Sun)***

### LIVER HESABU KWA FRASER

LIVERPOOl ipo katika nafasi ya kupiga hatua ya kufanya mazungumzo ya kumsajili winga wa Scotland, Ryan Fraser, 25, kutoka Bournemouth katika dirisha la Januari. ***(Talksport)***

### SPURS YAJIPANGA KWA DEPAY

TOTTENHAM ipo tayari kutoa ofa ya pauni milioni 50 kwa kiungo wa Lyon, Memphis Depay, 25, ambaye aliichezea Manchester United kati ya mwaka 2015 na 2017. ***(Mirror)***

### ALONSO, POCHETTINO WATAJWA

KIUNGO wa Liverpool, Xabi Alonso, 37, na kocha wa sasa wa Tottenham, Mauricio Pochettino, 47, wapo katika orodha ya wanaotarajiwa kuwa kocha mkuu ajaye wa Bayern Munich. ***(Star)***

### ENRIQUE SASA HATAKI KAZI

KOCHA wa zamani wa Hispania, Luis Enrique, ambaye amekuwa akielezwa kama mtu sahihi wa kutwaa mikoba ya Unai Emery katika kikosi cha Arsenal, hafikirii kurudi kazini katika kipindi cha hivi karibuni. ***(ESPN)***

### IBRAHIMOVIC KUSUBIRISHWA

MANCHESTER United haitajaribu kumsajili mshambuliaji wao wa zamani Zlatan Ibrahimovic, 38. Ibrahimovic atapatikana kama mchezaji huru mkataba wake na LA Galaxy utakapomalizika. ***(Sky Sports)***

### CHELSEA VITANI KWA DIALLO

TOTTENHAM, Chelsea, Watford na Norwich zipo tayari kutoa ofa kwa mshambuliaji wa Metz, Habib Diallo katika dirisha la usajili la Januari. Nyota huyo wa kimataifa wa Senegal, 34, amefunga mabao nane kwenye mechi 13 alizocheza msimu huu. ***(Teamtalk)***

### LENO AMULIKWA BAYERN

KIPA wa Arsenal, Bernd Leno, 27, yupo katika rada za Bayern Munich akitakiwa kuwa mlinda mlango namba moja kwa kurithi mikoba ya Manuel Neuer, 33. ***(Sun)***

### AKOMALIWA DORTMUND

BORUSSIA Dortmund bado inamhitaji kiungo mshambuliaji wa Everton, Anthony Gordon, 18, licha ya majira ya joto kutoa ofa ambayo ilikataliwa kwa nyota huyo wa kimataifa wa England U-19. ***(Football Insider)***

### LONGSTAFF KUJIFUNGA

KIUNGO wa Newcastle, Matty Longstaff, 19, atasaini mkataba mpya wiki chache zijazo, lakini kaka yake, Sean amekuwa akimueleza kwamba anapaswa kufanya makubwa zaidi kwa miezi 12 ijayo ili kuweza kupata dili hilo mpya. ***(Telegraph)***

## HABARI MICHEZO

# MASOUD ANUKIA KMC IKIMKANA RASMI ZAHERA

Na Shufaa Lyimo

WAKATI uongozi wa KMC FC ukikana rasmi kutokuwa na mpango wa kumwajiri aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, taarifa zimezidi kueleza kuwa klabu hiyo ya Manispaa ya Kinondoni tayari imekubaliana na kocha wa zamani wa Simba, Mrundi Masoud Djuma.

Baada ya Zahera kutemwa na Yanga kufuatia mwenendo mbaya katika klabu hiyo hususan kufanya vibaya kwenye michuano ya kimataifa, tetesi zimekuwa zikiihusisha klabu hiyo na kocha huyo raia wa DR Congo, lakini katika orodha hiyo Djuma akionekana kuongoza mbio hizo.

Hata hivyo, uongozi wa KMC FC ambao upo sokoni kumwinda kocha wa kubeba mikoba ya Mganda Jackson Mayanja aliyetupiwa virago vyake wiki iliyopita, umeweka wazi kuwa katu, hauna mpango wa kumwajiri Zahera.

**Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa KMC, Benjamini Sitta, alisema hamna ukweli wowote juu ya taarifa hizo na kudai hajazungumza wala kukutana na Zahera na kuwataka wadau wa soka wawe wanazungumza vitu vyenye uhakika.**

"Hakuna ukweli wowote kuwa tuna mpango wa kufanya kazi na Zahera, hizo habari si za kweli tunaomba watu wawe wanatoa taarifa ambazo zina uhakika," alisema Benjamini.

Na alipoulizwa kuhusu Djuma, Sitta hakutaka kuwa wazi na badala yake moja kwa moja aligeukia mpango wao wa kukiandaa kikosi hicho katika kipindi hiki ambacho ligi imesimama kupisha mapumziko ya mechi za kimataifa zilizopo katika Kalenda ya Fifa.

"Tutakitumia vizuri kipindi hiki ambacho ligi imesimama lengo letu ni kuhakikisha hatushuki daraja, tunaomba mashabiki wetu wazidi kutupa ushirikiano kama walivyotufanyia msimu uliopita," alisema mwenyekiti huyo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam jana, inadaiwa tayari Djuma amekubaliana na KMC kuinoa kwa mkataba wa mwaka mmoja.


Distributed via ippmedia

Meneja Masoko wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Anitha Msangi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kutangaza udhamini wa mashindano ya Waitara Gofu 2019, yanayotarajiwa kufanyika Jumamosi katika viwanja vya Lugalo. Wengine ni Mwenyekiti wa Klabu ya Lugalo Gofu, Brigedia Generali Mstaafu, Michael Luwongo (katikati) na Nahodha wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Kapt. Japhet Masai. **NA MPIGAPICHA WETU**

# SBL yajitosa kudhamini Waitara Gofu 2019

Na Mwandishi Wetu

JUMLA ya wachezaji 120 wa gofu kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini, wanatarajiwa kuchuana vikali mwishoni mwa wiki katika mashindano ya Waitara Gofu 2019, yanayodhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL).

Mashindano hayo ya siku moja, yatafanyika Jumamosi katika viwanja vya Gofu vya Lugalo jijini Dar es Salaam.

Akitangaza udhamini huo jijini Dar es Salaam jana, Meneja Masoko wa SBL, Anitha Msangi, aliwaambia waandishi wa habari kuwa udhamini wa SBL kwenye mashindano hayo maarufu, unalenga kuendeleza mchezo wa gofu nchini.

"Kampuni ya SBL kupitia bia yake pendwa ya Serengeti Premium Lager inayofuraha kuwa mdhamini mkuu wa mashindano ya gofu ya Waitara ya mwaka huu. Udhamini huu unaonyesha nia yetu ya dhati ya kuendeleza michezo hapa nchini," alisema Anitha.

Kupitia Bia ya Serengeti Premium Lager, Kampuni ya SBL ni mdhamini mkuu wa timu ya Taifa, 'Taifa Stars' na pia inadhamini Ligi ya Taifa ya Wanawake kupitia bia yake ya Serengeti Lite.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Brigedia Jenerali mstaafu Michael Luwongo, aliishukuru Kampuni ya SBL kwa udhamini huo na kuzitaka kampuni na taasisi nyingine kuiga mfano wa SBL na kujitokeza kusaidia mchezo wa gofu nchini.

"Tunaishukuru sana Kampuni ya SBL kwa mchango wake kwenye kusaidia maendeleo ya michezo hapa nchini na hususan gofu. SBL imekuwa mdhamini mkubwa wa mashindano haya," alisema.

Mashindano ya Waitara Gofu hufanyika kila mwaka yakilenga kutambua mchango wa Jenerali mstaafu George Waitara aliyekuwa mkuu wa majeshi kwa kuanzisha Klabu ya Gofu ya Lugalo.

Klabu ya Gofu ya Lugalo ilianza mwaka 2006 kutokana na mchango mkubwa wa Waitara ambapo pia uliendelezwa na Jenerali Davis Mwamunyange ambaye alimfuatia baada ya kustaafu.

# Julio, Malale wafunguka makocha kutimuliwa

Na Mwandishi Wetu

WAKATI Ligi Kuu Bara ndiyo kwanza ikiwa raundi ya 11 na baadhi ya timu zikiwa na viporo vingi mkononi, tayari makocha takriban watano wametimuliwa msimu huu kuzinoa klabu zao, suala ambalo Kocha wa zamani wa Simba, Jamhuri Kihwelu 'Julio' na Malale Hamsini aliyetimuliwa Ndanda FC wamefunguka tatizo linalowakumba.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kupitia redio moja jijini Dar es Salaam, kwa upande wa Malale ambaye msimu huu alitimuliwa kuinoa Ndanda FC, alisema kazi ya ukocha ni ngumu na ndiye anayebeba mzigo timu ikipoteza lakini tatizo huwa hapewi kila kitu ili baadaye aweze kubebeshwa lawama.

"Mwalimu inabidi apewe kila kitu ikiwa ni pamoja na mapendekezo yake ya wachezaji anaowataka kusajiliwa, lakini unakuta unaingiliwa katika majukumu yako, huku timu ikitakiwa kupata matokeo jambo ambalo ni vigumu kulitekeleza katika mazingira kama hayo," alisema.

Kwa upande wake Julio alisema, uswahili ni mwingi katika klabu za hapa nchini hususan hizi kubwa za Simba na Yanga, huku akifafanua kwamba utaratibu mzima wa viongozi wa klabu hizo hususan wakati wa usajili ndilo linalochangia makocha kutimuliwa kutokana na kutopewa nafasi ya kufanya usajili.

Alisema makocha wengi wanaajiriwa wakati timu ikiwa imeshasajili na hata kama kocha yupo na akatoa mapendekezo yake, huwa hayafuatwi na kamati zinazojiita za usajili katika klabu mbalimbali za hapa nchini.

"Ni kweli wanasema kocha anaajiriwa ili afukuzwe, lakini tukubali kama tatizo hawasikilizwi na viongozi na tambua mchezaji wewe hukutoa mapendekezo asajiliwe ni vigumu kuwa katika malengo yako na wenyewe ndio wanaweza kucheza vibaya kwa lengo la kukufukuzisha.

"Kamati hizi za usajili mara nyingi hazifuati mapendekezo ya makocha, na mara nyingine kocha anaajiriwa na kukabidhiwa wachezaji ambao tayari wamewasajili kwa matakwa yao, hivyo ni vigumu kupata matokeo ya haraka kutokana na aina ya wachezaji ambao hukuwahitaji," alisema.

Timu ambazo zimetimua makocha wao msimu huu hadi sasa ni KMC FC, Alliance FC, Ndanda FC, Biashara United na Yanga, huku Azam FC ikiachana kwa mikono miwili na Etienne Ndayiragije ambaye ameajiriwa kuwa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa, Taifa Stars.

# Michezo

Jumatano Novemba 13, 2019

Nipashe




Pulisic aondolewa kikosi cha Marekani UKURASA 28

## KELVIN NDANI LEICESTER...



Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Kelvin John (kushoto) akiwa na chipukizi mwenzake wa akademi ya Leicester City ya England katika kambi yao, Holmes Park, Belvoir Drive Training Complex juzi. Kelvin amejiunga na Academy ya Leicester City kufuatia kwenda England kwa masomo. **PICHA: MTANDAO**

## Samatta: Aionya Stars ya Lesotho

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU akikiri kutowafahamu Equatorial Guinea wala wachezaji wa kikosi hicho, nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta amewaonya wachezaji wenzake akiwataka kutowadharau wapinzani wao hao ili kuepuka balaa lililowakuta mwaka jana dhidi ya Lesotho.

Stars itashuka Uwanja wa Taifa keshokutwa, Ijumaa kuikaribisha Equatorial Guinea kwenye mechi ya kwanza ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Cameroon 2021.

Hata hivyo, Stars itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare nyumbani na kisha kupoteza ugenini dhidi ya Lesotho iliyokuwa ikitajwa kama kibonde, kwenye mechi ya kwanza ya kundi lao ya kuwania kufuzu Afcon 2019 iliyofanyika Juni nchini Misri.

Katika kundi hilo, lililokuwa likijumuisha Lesotho, Uganda na Cape Verde, Tanzania ilifuzu kwa mbinde kwa kuwafunga Waganda hao kwenye mechi ya mwisho huku maombi ya Watanzania kwa Lesotho kupoteza dhidi ya Wacape Verde yakipokelewa.

Kutokana na kuitambua presha waliyoipata katika kuwania kufuzu fainali hizo, Samatta alimwambia mwandishi wetu kuwa kamwe hawapaswi kuidharau Equatorial Guinea ambayo hawaifahamu vema.

"Binafsi siifahamu Equatorial Guinea wala wachezaji wake, lakini hatutakiwi kuidharau yasije yakatukuta kama yale ya Lesotho mwaka jana hapa nyumbani, tunapaswa kucheza kwa kujituma ili kushinda nyumbani," alisema Samatta ambaye aliifungia timu yake ya KRC Genk ya Ubelgiji bao pekee wakati wakichezea kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Liverpool kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita.

# MKWASA: HIKI NDICHO KINACHOITESA YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

### Asema wachezaji wengi wamekata tamaa, hivyo kazi kubwa ni kuwajenga kisaikolojia na kuwarejeshea...

WAKATI akiendelea kukiimarisha kikosi chake baada ya kukiongoza kuibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Ndanda FC, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, amesema tayari amebaini 'gonjwa' linalowatesa wachezaji wa timu hiyo, hivyo anafanya kazi kubwa ya kuwarejesha mchezoni.

Baada ya Ijumaa iliyopita kuibuka na ushindi huo katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara, Mkwasa ameendelea kukijenga kikosi chake kufuatia juzi kucheza mechi ya pili ya kirafiki dhidi ya Mkuti Market FC ya Masasi ikiwa ni siku moja baada ya kuvaana na Komabini ya Nanyumbu.

Katika mechi dhidi ya Mkuti Market FC iliyopigwa Uwanja wa Boma, Masasi mkoani Mtwara, Yanga ilikubali kipigo cha bao 1-0, ikikumbana na dhahama hiyo baada ya kuichapa Komabini ya Nanyumbu mabao 5-0 katika mchezo wake wa kwanza uliopigwa dimba la Halmashauri ya Wilaya Nanyumbu mkoani Mtwara.

**Hata hivyo, Mkwasa alimwambia mwandishi wetu kuwa tatizo kubwa alilol-ibaini katika kikosi cha Yanga ni wachezaji wengi kukata tamaa, jambo ambalo anatumia muda mwingi kuwajengea matumaini mapya ili kuwarejesha mchezoni.**

"Tatizo kubwa ni wachezaji wengi kukata tamaa, hivyo ninachofanya kwa sasa ni kuwajenga kwa kuwarudishia matumaini ili kuweza kufanya vizuri uwanjani," alisema kocha huyo wa zamani wa Taifa Stars, Mkwasa.

Mkwasa ambaye aliwahi kuwa katibu mkuu wa klabu hiyo, alipoulizwa kuhusu malengo yake ya muda mrefu, alisema anachokisaka kwa sasa ni matokeo ya uwanjani kwa kuwa yeye ni kocha wa muda mfupi.

"Mimi sijapewa mipango ya muda mrefu, kwa sababu ni kocha wa muda, hapa ninachokitaka kwanza ni matokeo ya uwanjani na kuitengeneza timu ili kocha ajaye aweze kuendelea hapa nilipoishia ikiwa ni pamoja na kuandaa mipango yake ya muda mrefu," alisema.

Jumatano iliyopita, Yanga ilitangaza kuachana rasmi na aliyekuwa Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera pamoja na kulivunja benchi zima la ufundi huku ikimtangaza Mkwasa kukaimu nafasi hiyo kwa muda wakati ikiendelea na mchakato wa kumsaka kocha mpya.

Zahera alitimuliwa ikiwa ni siku chache baada ya timu hiyo kutolewa na Pyramids FC ya Misri kwa jumla ya mabao 5-1 kwenye mechi ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, akitangaza uamuzi wa kuachana na Zahera na kuvunja benchi zima la ufundi, alisema ni baada ya kuona timu inakwenda vibaya, jambo ambalo walikaa na Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo na kufikia uamuzi huo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >